

REPUBLIC OF KENYA

LOWER PRIMARY LEVEL DESIGNS

VOLUME ONE

SUBJECTS:

KISWAHILI, LITERACY AND INDIGENOUS LANGUAGES AND ENGLISH ACTIVITIES

KENYA INSTITUTE OF CURRICULUM DEVELOPMENT

AUGUST 2017

First Published in 2017

All rights reserves. No part of this book may be reproduced, stored in a retrieval system or transcribed, in any form or by any means, electronic, mechanical, photocopy, recording or otherwise, without the prior written permission of the publisher.

ISBN:978-9966-31-714-8

Published and printed by Kenya Institute of Curriculum Development

FOREWORD

The Basic Education Curriculum Framework (BECF) outlines the vision and mission for the curriculum reforms. The Vision of the curriculum reforms is to develop “An engaged, an empowered and ethical citizen “while the mission is to “To nurture the potential of every learner”.

The framework adopts a Competency Based Curriculum and has identified seven core competences, namely; communication and collaboration, critical thinking and problem solving, creativity and imagination, citizenship, digital literacy, learning to learn, and self-efficacy. It provides a variety of opportunities for identification and nurturing of learner’s potentials and talents in preparation for life and the world of work. It is geared towards making learning enjoyable.

The curriculum designs are developed to enable implementation of the Basic Education Curriculum Framework. The design contain the National Goals of Education and outline the Early Years Education (EYE), subject general and specific learning outcomes. It also suggests a variety of learning experiences, assessment and links the topics to values, Pertinent and Contemporary Issues (PCI) and to other activity areas.

It is my hope that all educators in Early Years Education level will anchor their delivery to these Curriculum Designs.

Fred Matiang’i, PhD, EGH
CABINET SECRETARY
MINISTRY OF EDUCATION

TABLE OF CONTENTS

Foreword	i
Introduction	iii
Learning Areas Time Allocation	v
National Goals of Education	vi
General Learning Outcomes for Early Years Education	viii
KISWAHILI ACTIVITIES	1
Gredi ya Kwanza.....	8
Gredi ya Pili	38
Gredi ya Tatu	76
LITERACY ACTIVITIES	119
Grade One	121
Grade Two	147
Grade Three	171
ENGLISH ACTIVITIES	186
Grade One.....	188
Grade Two	228
Grade Three	268

INTRODUCTION

The Lower Primary designs are meant for learners in Grade 1 to 3. They have taken cognisance of the various aspects of development of learners of that age cohort. The designs are comprehensive enough to guide the teachers to effectively deliver the curriculum.

The teacher must understand the learning outcomes and be able to use the suggested learning experiences to achieve the outcomes. The teacher can also design own learning experiences as long as they achieve the designed learning outcomes. A variety of learning experiences will ensure that learners are engaged in the learning experience. Practical experiences will allow learners to retain more in the learning process. The designs allow the teachers to use a variety of assessment methods but in the end they must evaluate the achievement of the learning outcomes.

The curriculum designs are very critical and teachers must make reference to them consistently.

The Curriculum Designs for Lower Primary are in four volumes:

Volume One

- Kiswahili Activities
- Literacy Activities
- English Activities

Volume Two

- Mathematics Activities
- Environmental Activities
- Hygiene and Nutrition Activities

Volume Three

- Christian Religious Education
- Hindu Religious Education
- Islamic Religious Education

Volume Four

- Movement and Creative Activities

LEARNING AREAS TIME ALLOCATION

	Learning Area	Lessons Per Week
1	Literacy Activities	5
2	Kiswahili Language Activities/Kenya Sign Language	3
3	English Language Activities	3
4	Mathematical Activities	5
5	Environmental Activities	5
6	Hygiene and Nutrition Activities	2
7	Religious Activities	3
8	Movement and Creative Activities	8(*** 5 for PE)
9	Pastoral Programme of Instruction	1
	Total Lesson Per Week	35

NATIONAL GOALS OF EDUCATION

1. Foster nationalism, patriotism, and promote national unity

Kenya's people belong to different communities, races and religions and should be able to live and interact as one people. Education should enable the learner acquire a sense of nationhood and patriotism. It should also promote peace and mutual respect for harmonious co-existence.

2. Promote social, economic, technological and industrial needs for national development

Education should prepare the learner to play an effective and productive role in the nation.

a) Social Needs

Education should instil social and adaptive skills in the learner for effective participation in community and national development.

b) Economic Needs

Education should prepare a learner with requisite competences that support a modern and independent growing economy. This should translate into high standards of living for every individual.

c) Technological and Industrial Needs

Education should provide the learner with necessary competences for technological and industrial development in tandem with changing global trends.

3. Promote individual development and self-fulfilment

Education should provide opportunities for the learner to develop to the fullest potential. This includes development of one's interests, talents and character for positive contribution to the society.

4 Promote sound moral and religious values

Education should promote acquisition of national values as enshrined in the Constitution. It should be geared towards developing a self-disciplined and ethical citizen with sound moral and religious values.

5. Promote social equity and responsibility

Education should promote social equity and responsibility. It should provide inclusive and equitable access to quality and differentiated education; including learners with special educational needs and disabilities. Education should also provide the learner with opportunities for shared responsibility and accountability through service learning.

6. Promote respect for and development of Kenya's rich and varied cultures

Education should instil in the learner appreciation of Kenya's rich and diverse cultural heritage. The learner should value own and respect other people's culture as well as embrace positive cultural practices in a dynamic society.

7. Promote international consciousness and foster positive attitudes towards other nations

Kenya is part of the interdependent network of diverse peoples and nations. Education should therefore enable the learner to respect, appreciate and participate in the opportunities within the international community. Education should also facilitate the learner to operate within the international community with full knowledge of the obligations, responsibilities, rights and benefits that this membership entails.

8. Good health and environmental protection

Education should inculcate in the learner the value of physical and psychological well-being for self and others. It should promote environmental preservation and conservation, including animal welfare for sustainable development.

GENERAL LEARNING OUTCOMES FOR EARLY YEARS EDUCATION

By the end of early years' education, the learner should be able to:

1. Demonstrate basic literacy and numeracy skills for learning.
2. Communicate appropriately using verbal and/or non-verbal modes in a variety of contexts.
3. Demonstrate appropriate etiquette in social relationships.
4. Apply creativity and critical thinking skills in problem solving.
5. Explore the immediate environment for learning and enjoyment.
6. Practice hygiene, nutrition, sanitation, safety skills to promote health and wellbeing.
7. Demonstrate the acquisition of emotional, physical, spiritual, aesthetic and moral development for balanced living.
8. Demonstrate appreciation of the country's rich and diverse cultural heritage for harmonious co-existence.
9. Apply digital literacy skills for learning and enjoyment.

KISWAHILI ACTIVITIES

UTANGULIZI

Umuhimu wa Somo la Kiswahili

Kiswahili ni lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya. Ni lugha ya mawasiliano katika eneo la Afrika Mashariki na Kati. Wakenya wengi hujifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Ni muhimu wanafunzi wapate umilisi wa kuwasiliana kwa Kiswahili mapema hasa katika kiwango cha kwanza cha elimu. Aidha, somo la Kiswahili katika kiwango hiki humwandaa mwanafunzi kwa mafunzo ya viwango vya juu na baadaye katika ajira.

Umilisi wa Kimsingi

Mtaala mpya umejumuishia masuala tofauti na ambayo ni muhimu kwa kila mwanafunzi. Miongoni mwa masuala haya ni pamoja na umilisi wa kimsingi. Mtaala mpya umetambua umilisi tofauti ambao anapaswa kujengwa, mwanafunzi anapoendeleza masomo yake. Umilisi huu ni pamoja na:

- mawasiliano na ushirikiano
- uwazaji kina na utatuzi wa matatizo
- ubunifu
- uraia
- ujuzi wa kidijitali
- hamu ya kuendelea kujifunza
- kujiamini.

Inaaminika kwamba, mwanafunzi akipata umilisi ufaao, ataweza kufaa katika jamii inaobadilika kila uchao. Kutokana na imani hii, kazi katika mtaala huu imepunguzwa ili mwalimu apate nafasi murua kumsaidia mwanafunzi kujenga umilisi huu. Pamoja na haya, mtaala umempa mwanafunzi nafasi kubwa ya kushiriki katika masimulizi, usomaji na kufanya kazi katika vikundi. Vilevile, vifaa vya kidigitali vimependekezwa katika kila mada.

Maadili ya Kimsingi

Pamoja na umilisi wa kimsingi ni maadili ya kimsingi. Jamii isiyokuwa na maadili ni jamii ambayo imejaa uozo. Maadili katika jamii yanahakikisha kuwa raia wanaishi vizuri na kunawiri katika kila nyanja. Mtaala umetaja maadili ya kimsingi yafuatayo:

- mapenzi
- heshima
- uaminifu
- uwajibikaji
- uzalendo

- haki za Kijamii
- umoja
- amani.

Maadili haya yametokana na katiba ya Kenya na yanadhamiriwa kujumuishwa katika kila kipindi na kila somo. Hii ndiyo njia mwafaka ya kuhakikisha kuwa watoto na vijana wetu wametayarishwa kuwa raia waadilifu baada ya maisha shuleni.

Masuala Mtambuko

Haya ni masuala muhimu na ambayo mwanafunzi anatakiwa kuyaelewa na kujua jinsi ya kuyakabili katika maisha ya kila siku. Licha ya mtalaa kuhusisha masuala, masuala zaidi yaweza kujitokeza darasani. Mwalimu ahakikishe kuwa anayasisitiza anapoendelea na shughuli zake darasani. Akumbuke kuwa mbinu atakazozijumuisha katika kufundisha zaweza kuimarisha msisitizo wa masuala haya au zikakwamiza juhudi zilizowekwa kuhakikisha kwamba masuala haya hayapuuzwi. Miongoni mwa masuala yanayolengwa katika mtalaa ni pamoja na uwazi, kushirikisha wazazi katika masomo, uwazi, usalama, lishe bora na afya na elimu ya maendeleo endelevu.

Uhusiano na Masomo Mengine

Ni wazi kuwa, kila mada katika somo lolote huwa na uhusiano na mada nyingine katika masomo tofauti. Mtalaa huu umeundwa kwa njia ambapo mwalimu na mwanafunzi wataweza kurejelea masomo mengine na hivyo kujenga umilisi unaodhamiriwa kwa njia bora zaidi. Vilevile, kusisitiza uhusiano huu kunadhamiriwa kuangazia umuhimu wa ushirikiano wa wanafunzi wanaonawiri katika masomo tofauti na pia walimu wanaofunza masomo husika kwa lengo moja tu ambalo ni kufaulisha elimu.

Uhusiano na Shughuli za Huduma kwa Kijamii Zinazochangia Ujifunzaji

Kila somo sharti liwe na maana kwa mwanafunzi. Umuhimu wa mada yoyote ndio chanzo cha umakinifu darasani. Sababu kuu ya kusisitiza umilisi wa kimsingi ni kuhakikisha kwamba kuna uhusiano kati ya kinachofunzwa shuleni na maisha ya kila siku nje na ndani ya shule. Kutokana na hayo, katika kila mada, mapendekezo yametolewa ya jinsi mwanafunzi anaweza kuhamisha alichojifunza darasani hadi nyumbani. Ni muhimu uhusiano huu usisitizwe ili kuonyesha maana na umuhimu wa elimu.

Uhusiano na Shughuli Zingine Zilizoratibiwa za Ujifunzaji

Ni wazi kuwa mwanafunzi hujifunza kutokana na shughuli tofauti tofauti ndani ya darasa na nje ya darasa. Kuna shughuli nyingi ambazo huchangia pakubwa katika ujifunzaji. Mtalaa mpya umeongeza msisitizo wa shughuli hizi kutoka na umuhimu wake katika kufaulisha ujifunzaji. Shughuli hizi ni pamoja na vikundi vya ushirika shuleni, michezo ya kuigiza, kukariri na kuimba mashairi miongoni mwa mengine. Ni muhimu wanafunzi wahusishwe katika shughuli hizi ambazo kwazo zitachangia pakubwa katika kufaulisha shughuli za ujifunzaji.

Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

Mfumo mpya wa elimu unadhamiria kuhakikisha kuwa matokeo ya mafunzo ni ujenzi wa umilisi utakaomwezesha mwanafunzi kutumia ujuzi wake kujiendeleza. Kutokana na hayo, mfumo huu unadhamiria kupunguza usisitizo wa mtihamu wa mwisho wa viwango mbalimbali. Inatarajiwa kuwa mwanafunzi ataendelea kutathminiwa huku akiendelea kupata mafunzo zaidi. Mtalaa huu umependekeza mfumo wa kukadiria kiwango cha mwanafunzi. Mwanafunzi hatakuwa akilinganishwa na wenzake bali uwezo wake utakadiriwa kulingana na viwango vilivyopendekezwa. Kigezo hiki kimeorodhesha viwango vinne katika kukadiria uwezo wa mwanafunzi: anayezidisha matarajio; anayefikia matarajio; anayekaribia matarajio na aliye mbali na matarajio. Inatarajiwa kuwa mwalimu atajaribu mbinu tofauti baada ya tathmini yoyote ile kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanafikia matarajio kwa mujibu wa matokeo maalum yanayotarajiwa katika kila mada.

Jinsi Mtalaa huu Ulivyopangwa

Mtalaa huu umejumuishia stadi zote zinazofaa kufunzwa katika gredi ya kwanza, ya pili na ya tatu. Lugha yoyote ile ina stadi nne ambazo ni kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Inajulikana wazi kwamba, ili anayejifunza lugha aweze kupata umilisi ufaao, stadi hizi sharti zifunzwe pamoja. Hata hivyo, kwa vile wanafunzi wengi wanaingia shuleni bila kujua lugha ya Kiswahili, imeamuliwa kuwa wanafunzi wa gredi ya kwanza wasifunzwe kusoma na kuandika katika muhula wa kwanza ili kujenga umilisi wa kusikiliza na kuzungumza kwanza. Utafiti umeonyesha wazi kwamba mtu anapoelewa kuzungumza lugha yoyote ile, inakuwa rahisi kwa mtu yuyo huyo kusoma na kuandika katika lugha husika. Kutokana na haya, mtalaa huu imepangwa kwa kutumia mada zilizochaguliwa kwa msingi ya kimaudhui. Kila gredi imetengewa mada zake. Kila mada nayo ina mada ndogo kadhaa ambazo zimejikita katika stadi nne za lugha pamoja na msamiati na sarufi. Inatarajiwa kuwa, kadri inavyowezekana, yatakayojumuishwa katika kila mada ndogo yajikite katika maudhui lengwa.

Kusikiliza na Kuzungumza

Stadi hii inalenga mawasiliano kwa kutumia mdomo. Ili kujenga stadi hii, ni muhimu mwanafunzi kushirikishwa katika mazungumzo. Miongoni mwa mada zinazolenga mazungumzo ni pamoja na maamkizi, maagizo, msamiati, maagano, masimulizi na maelezo. Katika kuelekeza wanafunzi katika mada hizi, mwalimu anatakiwa kumpa mwanafunzi nafasi ya kujieleza, ashirikishwe katika maigizo na mijadala darasani. Ikumbukwe kuwa, kila neno analotamka mwanafunzi linachangia katika kujenga umilisi wa lugha. Mwalimu asilenge wanafunzi wanaochukuliwa kuwa werevu darasani tu. Licha ya mada ya kusoma kushirikishwa katika muhula wa kwanza, mada hii inadhamiriwa kujenga umilisi wa kusikiliza miongoni mwa wanafunzi. Mwanafunzi anaposikiliza hadithi ikisomwa, ataweza kuanza kuthamini usomaji. Hata hivyo, mijadala atakaoshirikishwa baada ya kusikiliza hadithi ikisomwa na mwalimu utamsaidia kuanza kuwa makini na vilevile kumpa nafasi ya kutumia Kiswahili katika mazungumzo.

Kusoma

Katika kila mada ya hadithi baada ya muhula wa kwanza gredi ya kwanza, mwanafunzi anatakiwa kusikiliza hadithi ikisomwa na mwalimu na vile vile kuna hadithi yake ambayo ataongozwa na mwalimu kusoma. Wakati mwalimu anaposoma hadithi na ambayo haitakuwa katika kitabu cha mwanafunzi, mwalimu anatakiwa kujua kuwa jinsi anavyosoma ndivyo mwanafunzi wake atakavyosoma baadaye. Ni muhimu kufanya mazoezi ya kutosha ili kuimarisha matamshi na ufasaha. Lazima ahakikishe kuwa kasi katika kusoma kwake ni ya kadri ili kuwafaa mwanafunzi katika kiwango chake. Mwalimu ahakikishe kwamba anamhusisha mwanafunzi katika hadithi yake kwa kumwongoza kujadili msamiati, picha, kutabiri, kuthibitisha utabiri na kuwauliza maswali anapoendelea kusoma. Ili kupima kiwango cha ufahamu wa mwanafunzi, mwalimu anatarajiwa kuwa atawauliza maswali baada ya kusoma na vilevile kumpa nafasi kutoa muhtasari wa hadithi na kujadili mafunzo katika hadithi.

Kuandika

Stadi ya kuandika ni muhimu katika mawasiliano. Kuzungumza na kuandika ndizo stadi mbili zinazomwezesha mwanafunzi kuwasiliana na wengine. Mazungumzo hufaa tu mzungumziwa anapokuwa karibu au kupitia mbinu za kiteknolojia kama vile simu. Stadi hii kwa hivyo ni muhimu katika mawasiliano na mtu aliye mbali kupitia kwa barua ya kawaida au barua pepe pamoja na kuweka kumbukumbu mambo muhimu. Umilisi wa kuandika umeanza kujengwa katika gredi ya kwanza muhula wa pili. Stadi hii imejikita katika mada za sauti, msamiati, majibu ya maswali ya hadithi katika maandishi na sarufi ambayo, pamoja na kujadiliwa darasani, inapendekezwa kwamba mazoezi ya kisarufi yaandikwe katika madaftari ya wanafunzi. Inakisiwa kuwa mwanafunzi afikapo katika gredi ya tatu, atakuwa na umilisi wa kutosha wa kuanza kuandika visa vifupi kutegemea mada inayolengwa.

Gredi ya tatu vilevile imejumuisha hatua tano za uandishi kama njia ya kumwelekeza mwanafunzi katika kujenga stadi ya uandishi. Hatua hizi ni: maandalizi, nakala ya kwanza, marejeleo, uhariri na uchapishaji. Hatua hizi zinadhamiriwa kuhakikisha kuwa mwanafunzi anashirikiana na wenzake katika kila hatu na hivyo kuweza kuandika kisa kifupi na sentensi chache haraka iwezekanavyo. Mwanafunzi anapofikia kiwango cha uchapishaji ambapo utungo wake unaweza kupachikwa kwenye ukuta kwa kila mwanafunzi kuusoma, atakuwa ameanza kujiamini katika utunzi. Utunzi unaofuata hatua hizi waweza kufunzwa kama kazi mradi.

Msamiati

Msamiati ni idadi ya maneno katika lugha. Msamiati humsaidia mwanafunzi katika kujenga hazina yake ya maneno anayoweza kutumia katika mawasiliano. Katika mtalaa huu, kila mada kuu ina msamiati unaohusiana nayo. Mwalimu ahusishe mwanafunzi katika kujifunza matumizi ya msamiati unaolengwa. Ikumbukwe kuwa, lengo si kutaja idadi kubwa ya maneno darasani. Mwalimu alenge kuhakikisha kuwa mwanafunzi amepata umilisi wa kutumia neno lililofunzwa katika mawasiliano ya kila siku. Zifuatazo ni hatua zinazofaa katika kufunza msamiati:

- onyesha neno unalofunza
- muulize mwanafunzi iwapo amewahi kulisikia neno hilo
- iwapo amewahi kulisikia, muulize iwapo anajua maana

- toa maana ya neno kwa kuigiza, kuonyehsa picha au kifaa halisi, kutumia neno lingine rahisi lenye maana sawa na neno unalolenga au kufafanua maana kwa maneno mepesi ya kiwango cha mwanafunzi
- tumia neno lengwa katika sentensi ili mwanafunzi aweze kujua maana kimktadha
- mshirikishe mwanafunzi katika kutunga sentensi akitumia neno lengwa.

Yafaa ieleweke kuwa kadri inavyowezekana, mada ya msamiati inafunzwa kabla ya masimulizi na hadithi ili kuhakikisha kuwa mwanafunzi anayaelewa maana ya maneno husika kabla hajahusishwa katika kusoma au masimulizi. Jambo hili linampa mwanafunzi nafasi murua ya kutumia msamiati aliojifunza katika muktadha halisi.

Sauti na Majina ya Herufi za Kiswahili

Ni wazi kuwa binadamu amezungumza kwa miaka mingi zaidi ikilinganishwa na miaka ambayo binadamu amekuwa akisoma na kuandika. Kutokana na hayo, ni muhimu kutilia mkazo sauti. Umilisi katika kutamka sauti utamsaidia mwanafunzi kuwasiliana katika mazungumzo kwa urahisi. Utafiti umeonyesha kwamba, zipo sauti ambazo jamii husika hutumia mara nyingi katika mazungumzo na maandishi. Kwa mfano, watoto wengi kuanza kwa kutamka sauti **/m/** kwa kuwa neno **mama** huwa ndilo neno la kwanza kutamkwa miongoni mwa jamii nyingi zinazotumia Kiswahili nchini. Kutokana na haya, pendekezo lililotolewa la utaratibu wa kujifunza sauti na herufi umetokana na umuhimu na wingi wa matumizi ya sauti lengwa katika mawasiliano. Hili litamwezesha mwanafunzi kuweza kusoma kwa haraka kwa vile sauti na herufi anayofunzwa mwanzo ni ile ameizoea katika mazungumzo. Mpangilio wa jinsi sauti zinavyofunzwa usichukuliwe kuwa kama njia ya kupuuzwa alfabeti kama tunavyojua. Mpangilio huu ni wa kumwezesha mwanafunzi kuzungumza na kusoma mapema. Alfabeti imeingizwa baadaye mwanafunzi anapojitayarisha kuanza kutumia kamusi. Sauti na herufi hizi zimepangwa katika makundi matatu.

Makundi haya ni:

- sauti zinazowakilishwa na herufi moja
- sauti zinazowakilishwa na herufi mbili
- sauti mbili zinazotamkwa pamoja katika neno

Katika kufunza sauti hizi, mwanafunzi ataelekezwa kuzisikiliza, kuzitamka, kuzitambua katika maneno, kuandika herufi zinazozwakilisha na pia kufanyishwa mazoezi ya kuzitamka sauti hizo anaposikiliza na kusoma hadithi yenye maneno yanayozijumuisha. Katika kufunza sauti, mwalimu ahakikishe kuwa amezitamka sauti hizo kwa usahihi. Kwa vile kila binadamu ana upungufu wake, mwalimu asione haya kumwalika mwalimu mwenzake au mgeni darasani kumsaidia kutamka sauti zinazomtataza. Vifaa vya kiteknolojia vilivyo na sauti zilizohifadhiwa vilevile vitamsaidia kuzisikiliza sauti lengwa na kuzitamka ipasavyo ili kumfaidi mwanafunzi anayemtagea kwa matamshi bora.

Sarufi

Sarufi inahusu matumizi ya lugha. Kila lugha ina sheria zinazoitawala. Ni kutokana na sheria hizi ambapo kila mzungumzaji wa lugha anaweza kujua anapotumia lugha vilivyo na anapotumia lugha kimakosa. Mtalaa umeundwa kwa njia ambayo mwanafunzi atajifunza sarufi katika muktadha wa matumizi. Vilevile, sarufi katika kiwango hiki imepunguzwa na kupewa vipindi vitakavyomwezesha mwanafunzi kufanya mazoezi zaidi kwa lengo la kujenga umilisi ufaao. Miongoni mwa vipengee vya sarufi vilivyojumuishwa ni pamoja na nafsi, nyakati na ukanusho, viashiria, vivumishi, vinyume, umoja na wingi.

Matokeo ya Kijumla Yanayotarajiwa Katika Kiwango cha Kwanza cha Masomo

Kufikia mwisho wa kiwango cha kwanza cha masomo, mwanafunzi aweze:

- a) kutumia mbinu zifaazo za usikivu katika mawasiliano kwenye mazingira yake
- b) kudhihirisha ufasaha wa kuzungumza kwa Kiswahili
- c) kusoma kwa ufasaha na kufahamu aina zozote za maandishi ya Kiswahili
- d) kuelezea mawazo, hisia na tajiriba kwa maandishi ya mkono au mbinu nyingine yoyote ya uwasilishaji
- e) kutumia sarufi ipasavyo katika mawasiliano
- f) kutumia msamiati ufaao katika mazingira yake kuwasiliana
- g) kuonyesha ukakamavu katika kuwasilisha masuala yanayokabili na yanayokabili mazingira yake.

GREDI YA KWANZA

MADA	MADA NDOGO	MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA	MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI	MASWALI DADISI
Karibu Darasani	Kusikiliza na Kuzungumza: Maamkuzi (Vipindi 3)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: a) kutambua maneno yatumiwayo katika maamkuzi b) kuamkua na kuitikia maamkuzi ili kujenga stadi ya kuzungumza c) kutambua umuhimu wa salamu katika mawasiliano d) kufurahia kushiriki katika maamkuzi.	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aigize maamkuzi kama vile hujambo? Sijambo; Hamjambo? Hatujambo darasani • Mwanafunzi ajadili mchoro wa watu wawili wakisalimiana • Wanafunzi wasalimiana na kisha washirikishwe katika mjadala kuhusu maamkuzi • Wanafunzi waweza kuwekwa katika vikundi ili wajadili kuhusu umuhimu wa maamkuzi • Wanafunzi wawili waweza kushirikishwa katika kuigiza maamkuzi mepesi • Wanafunzi waweza kuigiza maamkuzi darasani wakiwa wawili wawili 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Tunatumia maneno gani katika salamu? 2) Tunatakiwa kusalimiana vipi? 3) Kwa nini tunasalimiana?
	Kusikiliza na Kuzungumza: Maagizo (Vipindi 2)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: a) kutambua maagizo mepesi yanapotolewa darasani b) kutoa na kufuata maagizo mepesi yanayotumiwa darasani c) kubainisha maagizo yanayopaswa kufuatwa katika mazingira yake d) kuthamini umuhimu wa maagizo katika maisha ya kila siku.	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi ashiriki katika kutoa na kufuata maagizo kama vile simama, keti, andika na chora • Mwanafunzi aweza kuonyeshwa video ya jinsi ya kutoa na kufuata maagizo • Mwanafunzi ashiriki katika mjadala wa maagizo yafaayo na yasiyofaa kufuatwa • Mwanafunzi afafanue umuhimu wa maagizo • Mwanafunzi aweza kushirikishwa katika masimulizi ya matokeo ya kufuata na kutofuata maagizo • Mwanafunzi aweza kushirikishwa katika kuimba nyimbo na kukariri mashairi yanayohusu maagizo 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Umewahi kuambiwa ufanye jambo lolote? 2) Ni nani anayetakiwa kutoa maagizo? 3) Ni maagizo yepi yanayotakiwa kufuatwa na yasiyotakiwa kufuatwa? 4) Kufuata maagizo kuna umuhimu gani?

<p>Kusikiliza na Kuzungumza: Msamiati (Vipindi 2)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua kwa majina vifaa vinavyopatikana darasani ili kurahisisha mawasiliano</p> <p>b) kutumia majina ya vifaa vya darasani katika sentensi ili kuwezesha mazungumzo</p> <p>c) kufurahia kutumia na kutunza vifaa vinavyopatikana darasani.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi ataje vifaa halisi k.v. dawati, kitabu, kalamu na kifutio • Mwanafunzi aweza kuonyeshwa picha za vifaa halisi na kutaja majina • Mwanafunzi achore maumbo ya vifaa vya darasani • Wanafunzi waweza kuambatanisha kadi za maneno na vifaa halisi darasani wakiwa katika vikundi. • Mwanafunzi ajibizane na mwenzake kuhusu vifaa vya darasani k.m. Hii ni nini? Hii ni kalamu. 	<p>1) Je, wajua vitu unavyotumia darasani?</p> <p>2) Je, wajua umoja na wingi wa vitu vya darasani?</p>
<p>Kusoma: Hadithi (Vipindi 3)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze;</p> <p>a) kutambua msamiati uliotumika katika hadithi ili kuimarisha ufahamu</p> <p>b) kusikiliza hadithi zikisomwa na mwalimu ili kujenga usikivu</p> <p>c) kufahamu hadithi aliyosomewa darasani katika kuimarisha stadi ya kusoma</p> <p>d) kuchangamkia hadithi katika maisha ya kila siku.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi ajadili picha zilozajumuishwa kwenye hadithi • Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi • Mwanafunzi athibitisha utabiri wake baada ya kusomewa hadithi • Mwanafunzi aeleze matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi • Mwanafunzi aulize na kujibu maswali. • Wanafunzi waweza kujadiliana kuhusu hadithi wakiwa wawili wawili • Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi ikisomwa kwa kutumia tarakilishi na projekta 	<p>1) Kwa nini unapenda picha?</p> <p>2) Unapenda hadithi?</p> <p>3) Kwa nini unapenda hadithi?</p> <p>4) Unakumbuka hadithi uliyosikiliza?</p>
<p>Umilisi wa kimsingi unaokuzwa Mawasiliano na ushirikiano – Wutumie lugha faafu katika mazingira ya darasani na washiriki katika kazi ya vikundi Ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza</p>			
<p>Uhusiano na masuala mtambuko: Uraia: Utangamano wa kijamii; wanafunzi watangamana wanapoamkuana na kufanya kazi pamoja</p>		<p>Uhusiano na maadili: Heshima na adabu</p>	
<p>Uhusiano na masomo mengine: English Activities, Literacy and Indigenous Languages</p>		<p>Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji: Kuwaelezea wengine umuhimu wa kwenda shuleni.</p>	

Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji: Ugizaji wa maamkuzi Kazi ya vikundi	Mapendekezo ya tathmini: Kuchunguza mwanafunzi anavyoamkua na kupokea maamkuzi. Kuchunguza jinsi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi.
--	--

Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
Mwanafunzi, <ul style="list-style-type: none"> • anaamkua na kuitikia maamkuzi ifaavyo • anafuata maagizo kwa makini na kutoa maagizo kwa lugha sanifu • anatomia msamiati aliofunzwa kwa ubunifu katika mawasiliano • anafahamu hadithi na masimulizi aliyosimuliwa kwa wepesi. 	Mwanafunzi, <ul style="list-style-type: none"> • anaamkua na kuitikia maamkuzi ifaavyo • anafuata maagizo na kutoa maagizo kwa lugha sanifu • anatomia msamiati aliofunzwa katika mawasiliano • anafahamu hadithi na masimulizi aliyosimuliwa. 	Mwanafunzi, <ul style="list-style-type: none"> • anaamkua na kuitikia maamkuzi ifaavyo • anafuata maagizo lakini ana changamoto katika kutoa maagizo kwa lugha sanifu • ana changamoto katika kutumia baadhi ya msamiati aliofunzwa katika mawasiliano • anafahamu baadhi ya hadithi na masimulizi aliyosimuliwa. 	Mwanafunzi, <ul style="list-style-type: none"> • anaamkua na kuitikia baadhi ya maamkuzi • anafuata baadhi ya maagizo lakini ana changamoto katika kutoa maagizo • ana changamoto katika kutumia msamiati aliofunzwa katika mawasiliano • ana changamoto katika kufahamu hadithi na masimulizi aliyosimuliwa.

MADA	MADA NDOGO	MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA	MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI	MASWALI DADISI
Mimi na Wenzangu	Kusikiliza na Kuzungumza: Maelezo (Vipindi 3)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: a) kutambua wenzake darasani kwa majina, jinsia, miaka na gredi ili kuweza kuwaelezea b) kujieleza kwa kurejelea jina, jinsia, miaka na gredi kwa ufasaha katika mawasiliano ya kila siku	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi asikilize maelezo ya wengine. • Mwanafunzi aweza kusikiliza maelezo ya wenzake yaliyorekodiwa kwenye simu, kinasauiti, kipatakalishi n.k. • Wanafunzi watoleane maelezo kuwahusu katika vikundi. • Wanafunzi wakiwa wawili wawili waulizane. maswali na kujibizana k.m. Unaitwaje? • Mwanafunzi atoe maelezo yake akizingatia jina, jinsia, umri na gredi mbele ya darasa. 	1) Wewe ni nani? 2) Mwenzako ni nani? 3) Unapenda kufanya nini?

		<p>c) kutoa muhtasari wa maelezo aliyoyasikia katika mazingira yake</p> <p>d) kudhihirisha umakinifu wa kusikiliza katika mazingira yake</p> <p>e) kuchangamkia maelezo yake na ya wenzake katika kuimarisha mawasiliano</p> <p>f) kujivunia nafsi yake na wenzake katika miktadha mbalimbali.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aeleze maana ya msamiati unaotumiwa kujieleza k.v. umri, miaka, msichana, mvulana, gredi na rafiki. • Mwanafunzi atunge sentensi kwa kutumia maneno yanayotumiwa kujieleza na kueleza wenzake. • Wanafunzi waweza kujadiliana kuhusu maana na matumizi ya msamiati unaotumiwa k.m. umri, miaka, msichana, mvulana, gredi na rafiki katika vikundi. 	
	<p>Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (Vipindi 2)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kusimulia hadithi aliyosikiliza darasani ili kujenga stadi ya kusikiliza</p> <p>b) kufahamu hadithi aliyosimuliwa ili kupata ujumbe</p> <p>c) kuonyesha umakinifu wa kusikiliza katika miktadha mbalimbali</p> <p>d) kuchangamkia hadithi simulizi maishani.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aweze kuwa makini anaposimuliwa masimulizi. • Mwanafunzi asikilize masimulizi kupitia vifaa vya kiteknolojia k.m. simu, kinasa sauti, kipatakalishi n.k. • Mwanafunzi aweza kusikiliza mgeni mwalikwa akisimulia masimulizi. • Wanafunzi waweza kuwekwa katika vikundi na kutoleana muhtasari wa masimulizi yaliyosimulia. • Mwanafunzi aulize na kujibu maswali kutokana na masimulizi. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Umewahi kusimuliwa kisa kipi? 2) Unatarajiwa kufanya nini unaposimuliwa masimulizi? 3) Unakumbuka nini katika masimulizi uliyosimuliwa?
	<p>Kusoma: Hadithi (Vipindi 3)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua msamiati uliyotumika katika hadithi ili kuweza kuutumia katika mawasiliano</p> <p>b) kusikiliza hadithi zikisomwa ili kujenga usikivu</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi. • Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi. • Mwanafunzi athibitisha utabiri wake baada ya kusomewa hadithi. • Mwanafunzi aeleze matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Je, ni hadithi kusomewa? 2) Unatarajiwa kufanya nini unaposomewa hadithi? 3) Unakumbuka nini

		<p>c) kufahamu hadithi aliyosomewa darasani ili kupata ujumbe</p> <p>d) kuchangamkia kusikiliza hadithi kila siku.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Wanafunzi wajadiliane kuhusu hadithi waliosomewa katika vikundi. • Mwanafunzi aweza kushirikishwa kusikiliza hadithi zikisomwa kupitia vifaa vya teknolojia k.v. tarakilishi, projekta n.k. • Mwanafunzi aweza kuonyeshwa picha na kadi za msamiati uliotumiwa katika hadithi. • Mwanafunzi aulize na kujibu maswali kutokana na hadithi. 	<p>katika hadithi uliyosomewa?</p> <p>4) Unafikiria ni nini kitakachotokea katika hadithi hii?</p>
<p>Umilisi wa kimsingi unaokuzwa Mawasiliano na ushirikiano – Wanatumia lugha faafu katika kujieleza darasani. Vilevile wanashiriki katika kazi ya vikundi Ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza</p>				
<p>Uhusiano na masuala mtambuko: Stadi za maisha: kujitambua na kujithamini kijamii wanapojieleza</p>			<p>Uhusiano na Maadili: Heshima kwa wengine</p>	
<p>Uhusiano na masomo mengine: English Activities, Literacy and Indigenous Languages, Religious Activities</p>			<p>Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji: kujizatiti kuwajua wenzake shuleni na vijijini kuwafunzi wenzake umuhimu wa kuwajua watu kwa majina kwa usalama wao.</p>	
<p>Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji: kazi ya vikundi shughuli za vikundi vya ushirika shuleni.</p>			<p>Mapendekezo ya Tathmini: kuchunguza ukakamavu wa mwanafunzi anapojieleza kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi.</p>	

Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • anajieleza kwa ukakamavu na ufasaha • anaelezea wenzake kwa ukakamavu na 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • anajieleza kwa ufasaha • anaelezea wenzake kwa 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • anajieleza ifaavyo • anaelezea wenzake ifaavyo 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto za kujieleza ifaavyo • ana changamoto za kuelezea

ufasaha <ul style="list-style-type: none"> • anasimulia kisa kwa lugha ifaayo na yenye ubunifu • anajibu maswali ya ufahamu wa hadithi na masimulizi kwa ubunifu na usahihi • anatoa muhtasari wa hadithi aliyosimuliwa kwa ubunifu. 	ufasaha <ul style="list-style-type: none"> • anasimulia kisa kwa lugha ifaayo • anajibu maswali ya ufahamu kwa usahihi • anatoa muhtasari wa hadithi aliyosimuliwa. 	<ul style="list-style-type: none"> • anasimulia baadhi ya visa • ana changamoto za kujibu baadhi maswali kutokana na hadithi • ana changamoto za kutoa muhtasari wa hadithi aliyosimuliwa. 	wenzake ifaavyo <ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto katika kusimulia kisa • ana changamoto za kujibu maswali mengi kutokana na hadithi • ana changamoto za kutoa muhtasari wa hadithi aliyosimuliwa.
---	--	---	---

MADA	MADA NDOGO	MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA	MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI	MASWALI DADISI
Tarakimu	Kusikiliza na Kuzungumza: Msamiati (Vipindi 3)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: <ol style="list-style-type: none"> kutambua nambari moja hadi kumi (1-10) katika mazingira yake kuhesabu nambari 1-10 kwa mfuatano ili kujenga stadi ya kuzungumza kutaja majina ya nambari moja hadi kumi kwa mfululizo ili kujenga stadi ya kuzungumza kutumia majina ya nambari moja hadi kumi kutunga sentensi ili kujenga stadi ya kuzungumza kuthamini matumizi ya nambari katika maisha ya kila siku. 	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi anaweza kupewa kadi za nambari azitaje kwa maneno. • Mwanafunzi aweza kukariri mashairi kuhusu nambari hadi kumi. • Mwanafunzi aweza kushirikishwa kuimba nyimbo za tarakimu. • Wanafunzi waambatanishe nambari na maneno kwa kuonyeshwa nambari na kutaja jina la nambari husika. • Wanafunzi wahesabu vidole kwa Kiswahili wakiwa wawili wawili k.m. mmoja anachukua kidole kimoja na mwingine anataja jina la nambari, 'moja' n.k. • Wanafunzi wanaweza kupanga kadi za majina ya nambari hadi kumi kwa utaratibu. • Mwanafunzi aweza kuonyeshwa nambari na jina kwa kutumia tarakilishi na projekta. • Mwanafunzi aweza kuonyeshwa video ya wanafunzi wakisoma nambari hadi kumi kwa tarakilishi. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Unajua kuhesabu nambari ngapi? 2) Hesabu moja hadi kumi. 3) Unaweza kutumia majina yapi ya nambari moja hadi kumi katika sentensi? 4) Ni nini umuhimu wa nambari maishani?

	<p>Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (Vipindi 2)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <ol style="list-style-type: none"> kusikiliza visa vinavyohusiana na nambari ili kujenga umakinifu kufahamu masimulizi ya visa vinavyohusiana na nambari ili kupata ujumbe kuonyesha umakinifu wa kusikiliza katika mawasiliano kuchangamkia masimulizi katika maisha ya kila siku. 	<ul style="list-style-type: none"> Mwanafunzi asikilize kisa kikisimuliwa. Mwanafunzi ashiriki katika kusimulia kisa kinachohusisha nambari. Mwanafunzi atoe muhtasari wa matukio yaliyosimuliwa. Wanafunzi waweza kusimuliana visa vinavyojumuisha nambari wakiwa wawili wawili au katika vikundi. Mwanafunzi aweza kusikiliza masimulizi kupitia kwa vyombo vya kiteknolojia kama vile simu, kinasasauti na kipatakalishi vyaweza kutumiwa katika kusimulia visa mbalimbali. 	<ol style="list-style-type: none"> Nambari hutumiwaje? Unatarajiwa kufanya nini unaposimuliwa kisa? Unakumbuka nini katika kisa ulichosimuliwa?
	<p>Kusoma: Hadithi (Vipindi 3)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze;</p> <ol style="list-style-type: none"> kutambua msamiati uliotumika katika kurahisisha ufahamu kusikiliza hadithi zikisomwa na mwalimu ili kujenga stadi ya kusikiliza kufahamu hadithi aliyosomewa ili kupata ujumbe kuchangamkia kusikiliza hadithi kila siku ili kujenga ari ya kusoma baadaye. 	<ul style="list-style-type: none"> Mwanafunzi ashirikiane na wengine kujadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi. Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi. Mwanafunzi athibitisha utabiri wake baada ya kusoma hadithi. Mwanafunzi atunge sentensi akitumia msamiati uliotumika kwenye hadithi. Wanafunzi wajadiliane kuhusu hadithi waliosomewa katika vikundi. Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi zikisomwa kupitia vifaa vya kiteknolojia k.v. tarakilishi, projekta n.k. Mwanafunzi aulize na kujibu maswali kutokana na hadithi. 	<ol style="list-style-type: none"> Umewahi kusikiliza hadithi ipi? Unatarajiwa kufanya nini unaposomewa hadithi? Kwa nini unapenda picha? Unaweza kutabiri kitakachotokea katika hadithi? Unakumbuka hadithi uliyosomewa?

Umilisi wa kimsingi unaokuzwa Mawasiliano na ushirikiano – Wanatumia lugha faafu darasani. Vilevile wanashiriki katika kazi ya vikundi Ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi atapata hamu ya kuendelea kuhesabu kwa kutumia Kiswahili	
Uhusiano na masuala mtambuko: Stadi za maisha: kujitambua wanapohesabu viungo vya mwili.	Uhusiano na Maadili: uwajibikaji wa kutunza alichonacho na cha wenzake.
Uhusiano na masomo mengine: Mathematics Activities	Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji: kutumia ujuzi wa kuhesabu katika biashara hasa anapotumwa dukani au sokoni.
Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji: kazi ya vikundi shughuli za vikundi vya ushirika shuleni michezo.	Mapendekezo ya Tathmini: kuchunguza uwezo wa kuhesabu kwa Kiswahili kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa.

Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
Mwanafunzi , <ul style="list-style-type: none"> ana hesabu moja hadi kumi kwa haraka anatumia msamiati wa nambari kwa ubunifu katika sentensi anasimulia kisa kwa ufasaha na ubunifu anajibu maswali ya ufahamu hadithi na masimulizi kwa ubunifu na usahihi anatoa muhtasari wa hadithi aliyosimuliwa au kusomewa kwa ubunifu. 	Mwanafunzi , <ul style="list-style-type: none"> anahesabu moja hadi kumi anatumia msamiati wa nambari katika sentensi ifaavyo Anasimulia kisa kwa ufasaha. anajibu maswali ya ufahamu hadithi na masimulizi kwa usahihi anatoa muhtasari wa hadithi aliyosimuliwa au kusomewa. 	Mwanafunzi , <ul style="list-style-type: none"> ana changamoto chache hesabu moja hadi kumi ana changamoto za kutumia baadhi ya msamiati wa nambari katika sentensi anasimulia baadhi ya visa ana changamoto za kujibu baadhi ya maswali ya ufahamu wa hadithi na masimulizi anatoa muhtasari wa hadithi aliyosimuliwa au kusomewa. 	Mwanafunzi , <ul style="list-style-type: none"> ana changamoto nyingi katika kuhesabu moja hadi kumi ana changamoto za kutumia msamiati wa nambari katika sentensi ana changamoto katika kusimulia kisa ana changamoto za kujibu maswali mengi kutokana na hadithi na masimulizi ana changamoto za kutoa muhtasari wa hadithi aliyosimuliwa au kusomewa.

MADA	MADA NDOGO	MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA	MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI	MASWALI DADISI
Siku za wiki	Kusikiliza na Kuzungumza: Msamiati (Vipindi 3)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: a) kutambua siku za wiki katika mawasiliano ya kila siku b) kutaja majina ya siku za wiki kwa mfululizo ili kumsaidia kuratibu shughuli za siku c) kuelezea shughuli za siku mbalimbali za wiki ili kujenga stadi ya kuzungumza d) kutumia majina ya siku za wiki kutunga sentensi ili kuimarisha mawasiliano e) kuthamini kila siku ya wiki ili kutilia maanani shughuli za siku husika maishani.	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi atambue siku za wiki yaani: Jumatatu, Jumanne, Jumatano, Alhamisi, Ijumaa, Jumamosi na Jumapili kwa kutumia kadi za maneno. • Mwanafunzi aweza kuimba wimbo wa siku za wiki. • Mwanafunzi aweza kukariri mashairi kuhusu siku za wiki. • Mwanafunzi ashiriki katika majadiliano ya shughuli za siku za wiki k.m. Jumatatu naenda shule, Ijumaa, Jumamosi au Jumapili nashiriki ibada n.k. • Wanafunzi waweza kupanga kadi za majina ya siku za wiki kwa utaratibu wakiwa wawili wawili. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Wiki moja ina siku ngapi? 2) Unaenda shule siku gani? 3) Unaweza kutaja na kuandika majina yapi ya siku za wiki kwa mfuatano? 4) Waweza kutumia majina yapi ya siku za wiki katika sentensi?
	Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (Vipindi 2)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: a) kusimulia matukio katika siku tofauti za wiki ili kujenga stadi ya kuzungumza b) kufahamu masimulizi ya matukio ya siku za wiki aliyosimuliwa ili kupata ujumbe c) kuonyesha umakinifu wa kusikiliza katika mawasiliano d) kuchangamkia masimulizi maishani ili kuimarisha usikivu.	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi asimulie kisa darasani. • Mwanafunzi aonyeshe umakinifu anaposikiliza masimulizi ya mwalimu na wanafunzi wenzake. • Wanafunzi waweza kusimuliana matukio ya siku za wiki wakiwa wawili wawili. • Mwanafunzi asikilize masimulizi kuhusu matukio ya siku za wiki kupitia vifaa vya kiteknolojia k.m. simu, kinasasauti, kipakatalishi n.k. • Wanafunzi waweza kuwekwa katika vikundi na kutoleana muhtasari wa matukio yaliyosimuliwa hasa kwa kutumia vifaa vya teknolojia. • Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali kutokana na masimulizi aliyosikiliza. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Ni matukio yapi uliyowahi kushuhudia? 2) Unatarajiwa kufanya nini unaposimuliwa kisa? 3) Unakumbuka nini katika matukio uliyosimuliwa?

	<p>Kusoma Hadithi (Vipindi 3)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <ol style="list-style-type: none"> kutambua msamiati uliotumika katika hadithi ili kuimarisha ufahamu kusikiliza hadithi zikisomwa na mwalimu zinazojumuisha matukio ya siku za wiki ili kujenga umakinifu kufahamu hadithi aliyosomewa katika mada ili kupata ujumbe kuchangamkia kusikiliza hadithi kila siku. 	<ul style="list-style-type: none"> Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi. Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi. Mwanafunzi athibitisha utabiri wake baada ya kusomewa hadithi. Mwanafunzi asikilize hadithi ikisomwa na mwalimu. Mwanafunzi aeleze matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi. Mwanafunzi waweza kujadiliana kuhusu hadithi waliyosomewa katika vikundi. Mwanafunzi aweza kushirikishwa kusikiliza hadithi kwa kutumia vifaa vya teknolojia k.v. tarakilishi, projekta n.k. Mwanafunzi aweza kuonyeshwa picha na kadi za maneno yaliyotumiwa katika hadithi. Mwanafunzi ajibu na aulize maswali kutokana na hadithi. 	<ol style="list-style-type: none"> Umewahi kusikiliza hadithi ipi? Unatarajiwa kufanya nini unaposomewa hadithi? Unafikiri ni nini kitakachotokea katika hadithi? Unakumbuka hadithi ipi uliyosomewa?
<p>Umilisi wa kimsingi unaokuzwa Mawasiliano na ushirikiano – kazi za vikundi Ujuzi wa kidijitali : kuandika kwa vipakatalishi Ubunifu: kueleza namna ya kutumia kila siku aliyo nayo.</p>				
<p>Uhusiano na masuala mtambuko: stadi za Maisha (uwajibikaji) -kufanya uamuzi wa jinsi ya kutumia siku za wiki uzalendo: kushirikiana katika vikundi.</p>		<p>Uhusiano na Maadili: heshima kwa siku zilizotengewa shughuli za kidini.</p>		

<p>Uhusiano na Masomo mengine: Literacy activities na Mathematics Activities</p>	<p>Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji: kuisitiza umuhimu wa shughuli tofauti kwa mfano siku za kwenda shule, siku ya kupumzika na siku ya kwenda maabadini kwa wenzake na miongoni mwa wanajamii.</p>
<p>Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji: kazi ya vikundi shughuli za vikundi vya ushirika shuleni michezo.</p>	<p>Mapendekezo ya Tathmini:</p> <ul style="list-style-type: none"> • kuchunguza jinsi anavyoorodhesha siku za wiki na kuzitungia sentensi • kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa.

Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • anaorodhesha siku za wiki kwa haraka na ifaavyo • anatumia majina ya siku za wiki katika mawasiliano kwa ubunifu • anasimulia kisa kwa ufasaha na ubunifu • anajibu maswali ya ufahamu hadithi na masimulizi kwa ubunifu na usahihi. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • anaorodhesha siku za wiki ifaavyo • anatumia majina ya siku za wiki katika mawasiliano • anasimulia kisa kwa ufasaha • anajibu maswali ya ufahamu hadithi na masimulizi kwa usahihi. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto katika orodhesha siku za wiki ifaavyo • ana changamoto za kutumia majina ya siku za wiki katika mawasiliano • anasimulia baadhi ya visa • anajibu baadhi ya maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto nyingi katika kuorodhesha siku za wiki • ana changamoto nyingi katika kutumia majina ya siku za wiki katika mawasiliano • Ana changamoto katika kusimulia visa • Ana changamoto katika kujibu maswali ya ufahamu hadithi na masimulizi.

MADA	MADA NDOGO	MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA	MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI	MASWALI DADISI
Familia	Sauti na majina ya herufi za Kiswahili (Vipindi 8)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <ol style="list-style-type: none"> kutamka sauti nne za herufi moja ili kuimarisha mazungumzo kutambua sauti za herufi moja zilizofunzwa katika maneno ili kuimarisha mazungumzo kutambua majina ya herufi zinazowakilisha sauti lengwa katika kuimarisha stadi ya kusoma kusoma herufi za sauti moja katika kujenga stadi ya kusoma kusoma maneno kwa kutumia silabi zinazotokana na sauti lengwa katika kujenga stadi ya kusoma kusoma vifungu vilivyo na maneno yaliyo na sauti lengwa ili kujenga stadi ya kusoma kuandika maumbo ya herufi zinazowakilisha sauti lengwa katika kuimarisha stadi ya kuandika kuchangamkia kutumia maneno yanayojumuisha sauti zilizofunzwa katika mawasiliano ya kila siku. 	<ul style="list-style-type: none"> Mwanafunzi ashirikishwe kutambua sauti /m/, /a/, /u/ na /k katika maneno. Mwanafunzi asikilize mwalimu akitamka sauti lengwa, kisha watamke pamoja na mwalimu na mwishowe atamke akiwa peke yake, wawili wawili na katika darasa. Mwanafunzi atumie teknolojia (papaya) kutamkia sauti. Mwanafunzi atambue herufi inayowakilisha sauti lengwa kwa kutumia kadi za herufi. Mwanafunzi aambatanishe silabi kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa. Mwanafunzi atenganishe silabi katika kutambua sehemu mbalimbali za maneno. Wanafunzi waweza kushirikishwa kusikiliza mgeni mwalikwa mwenye umahiri wa kutamka sauti lengwa. Mwanafunzi asome maneno kwa kutumia silabi au kugawa maneno marefu zaidi vipande vipande. Wanafunzi wasome hadithi zilizo na maneno yaliyobeba sauti lengwa kama darasa au wawili wawili. Mwanafunzi asikilize na kusoma hadithi kupitia vifaa vya kiteknolojia kama vile tarakilishi, projekta n.k. Mwanafunzi afinyange na aandike maumbo ya herufi za sauti alizosoma hewani na vitabuni. Mwanafunzi aandike maneno yaliyo na herufi za sauti alizofunzwa kwa kunakili aliyoandika mwalimu. 	<ol style="list-style-type: none"> Ni sauti zipi unazojua kutamka? Unajua kusoma herufi na maneno yapi? Unajua kuandika herufi na maneno yapi?

	<p>Kusikiliza na Kuzungumza: Maneno ya heshima (Vipindi 2)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <ol style="list-style-type: none"> kutambua maneno ya heshima katika familia kutumia maneno ya heshima katika mawasiliano kuambatanisha maneno ya heshima na hisia zifaazo katika mawasiliano kuthamini matumizi ya maneno ya heshima katika mawasiliano ya kila siku. 	<ul style="list-style-type: none"> Wanafunzi waweza kuonyeshwa mchoro wa mtoto akipokea zawadi halafu wajadili neno linalofaa kutumiwa na anayepokea zawadi. Mwanafunzi aweza kuonyeshwa video inayoashiria matumizi ya maneno ya heshima k.m. Mtu akipokea zawadi au wageni wakimtembelea mgonjwa hospitalini. Mwanafunzi aweza kupewa ufafanuzi kuhusu maneno ya heshima kama vile “asante, pole na tafadhali.” Wanafunzi waweza kushirikishwa katika kuigiza vitendo vya heshima. Mwanafunzi ahusishwe katika mjadala kuhusu umuhimu wa kutumia maneno ya heshima. 	<ol style="list-style-type: none"> Unapopewa zawadi unatakiwa kusema nini? Mwenzako anapojikwaa utamwambiaje? Unapoomba ruhusu kutoka kwa mwalimu unatumia neno gani?
	<p>Kusoma: Hadithi (Vipindi 4)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <ol style="list-style-type: none"> kutambua msamiati uliotumika katika hadithi kusikiliza hadithi zikisomwa na mwalimu zinazohusu familia darasani kusoma hadithi kuhusu familia darasani kufahamu hadithi aliyosomewa kuhusu familia darasani kuchangamkia kusikiliza hadithi kila siku. 	<ul style="list-style-type: none"> Mwanafunzi aweza kujadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi. Mwanafunzi aweza kutabiri kitakachotokea kwenye hadithi. Mwanafunzi aweza kufuatilia hadithi ikisomwa na mwalimu, kisha asome pamoja na mwalimu na baadaye asome akiwa peke yake au wiwili wawili. Mwanafunzi aweza kueleza maana na matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi ukiwemo msamiati wa familia kama vile baba, mama, kaka na dada. Mwanafunzi aweza kusikiliza mwalimu anaposoma hadithi, asome pamoja na mwalimu na kisha asome peke yake, wawili wawili au katika vikundi. Mwanafunzi asikilize hadithi ya mwalimu au iliyorekodiwa inayojumuisha matumizi ya maneno ya heshima. 	<ol style="list-style-type: none"> Unatakiwa kufanya nini unaposomewa hadithi? Unakumbuka nini katika hadithi uliyosomewa? Unaweza kutabiri kitakachotokea katika hadithi? Unaweza kusoma hadithi? Kwa nini unapenda hadithi? Unakumbuka hadithi gani uliyosoma?

			<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aweza kutoa muhtasari wa hadithi aliyosoma au aliyosomewa. • Wanafunzi waweza kutunga sentensi wakitumia majina ya watu wa familia katika vikundi. • Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kwa kutumia jitabu mbele ya darasa. • Mwanafunzi aweza kuthibitisha utabiri wake baada ya kusomewa hadithi. • Wanafunzi waweza kushirikishwa katika kuuliza na kujibu maswali kutokana na hadithi darasani na vilevile kuyaandika kwenye madaftari yao. 	
	Sarufi: Nafsi ya kwanza wakati uliopo (Vipindi 3)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua maneno na viambishi vinavyotumika kuonyesha nafsi ya kwanza wakati uliopo hali ya umoja na wingi katika sentensi</p> <p>b) kusoma vifungu vya maneno vinavyoashiria nafsi ya kwanza wakati uliopo hali ya umoja na wingi</p> <p>c) kutumia nafsi ya kwanza wakati uliopo hali ya umoja na wingi katika sentensi</p> <p>d) kuandika vifungu vya maneno vinavyoashiria nafsi ya kwanza wakati uliopo hali ya umoja na wingi</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aweza kutumia nafsi ya kwanza wakati uliopo hali ya umoja na wingi katika mawasiliano. • Mwanafunzi aweza kutumia nafsi ya kwanza wakati uliopo hali ya umoja na wingi katika sentensi. • Mwanafunzi aweza kusoma sentensi zinazojumuisha matumizi ya nafsi ya kwanza wakati uliopo hali ya umoja na wingi. • Mwanafunzi aweza kujaza mapengo kwa kutumia maneno na viambishi vinavyowakilisha nafsi ya kwanza na wakati uliopo kama vile; mimi nina ; sisi tuna. • Wanafunzi waweza kuigiza nafsi ya kwanza wakati uliopo hali ya umoja na wingi katika vikundi kwa kutumia vifungu kama vile mimi ninaandika-sisi tunaandika, mimi ninasoma- sisi tunasoma baadaye waongozwe kuandika vifungu hivi kwenye madaftari yao. • Mwanafunzi aweza kupewa zoezi katika tarakilishi ili atumie mbinu ya kuburura majibu sahihi na kutia kapuni. 	<p>1) Je, unatumia maneno gani kujirejelea na mkiwa wengi?</p> <p>2) Ukiwa unafanya lolote sasa, utasemaje?</p>

	e) kufurahia kutumia nafsi ya kwanza wakati uliopo hali ya umoja na wingi katika mawasiliano.	
Umilisi wa kimsingi unaokuzwa: <ul style="list-style-type: none"> • Mawasiliano na ushirikiano – Kujadiliana kuhusu majukumu ya watu wa familia; Kufanya kazi kwa vikundi • Hamu ya ujifunzaji: Matumizi ya nafsi ya kwanza wakati uliopo • Ujuzi wa kidijitali :Kuna mapendekezo ya kutumia vifaa vya teknolojia kufunzia • Ubunifu: Utunzi wa sentensi kwa kutumia nafsi ya kwanza wakati uliopo. 		
Uhusiano na masuala mtambuko: <ul style="list-style-type: none"> • Uraia: uzalendo: kushirikiana katika vikundi • Utangamano wa kijamii - mahusiano katika familia. 	Mahusiano na Maadili: Mapenzi katika familia.	
Uhusiano na masomo mengine: Religious Studies, English Activities and Environmental Activities	Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji: kutembelea nyumba ya mayatima na kucheza nao kuwaelimisha wengine umuhimu wa familia katika ujenzi wa jamii.	
Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji: kazi ya vikundi shughuli za vikundi vya ushirika shuleni michezo.	Mapendekezo ya Tathmini: <ul style="list-style-type: none"> • kuchunguza jinsi anavyowatambua watu katika familia yake • kuchunguza anavyotamka sauti zilizofunzwa • kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa • kuchunguza jinsi anavyotumia nafsi ya kwanza wakati uliopo katika sentensi. 	

Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> anawataja watu wa familia zaidi ya aliyofunzwa anatumia majina ya watu wa familia kwa ubunifu katika sentensi anasoma hadithi kwa ufasaha anajibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa ubunifu na usahihi anatumia nafsi ya kwanza wakati uliopo kutunga sentensi zenye ubunifu anaandika kwa hati nadhifu. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> anawataja watu wa familia anatumia majina ya watu wa familia katika sentensi ifaavyo anasoma hadithi anajibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi anatumia nafsi ya kwanza wakati uliopo kutunga sentensi ifaavyo anaandika kwa hati inayosomeka. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> anawataja watu wa familia anatumia majina ya watu wa familia katika sentensi anasoma baadhi ya kazi anazopewa anajibu baadhi maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi ana changamoto za kutumia nafsi ya kwanza wakati uliopo kutunga sentensi anaandika kwa hati inayosomeka. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> anawataja watu wa familia ana changamoto za kutumia majina ya watu wa familia katika sentensi ana changamoto katika kusoma Ana changamoto katika kujibu maswali ya ufahamu hadithi na masimulizi kwa usahihi ana changamoto za kutumia nafsi ya kwanza wakati uliopo kutunga sentensi ana changamoto katika kuandika.

MADA	MADA NDOGO	MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA	MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI	MASWALI DADISI
Mwili Wangu	Sauti na majina ya herufi za Kiswahili (Vipindi 8)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <ol style="list-style-type: none"> kutamka sauti nne za herufi moja katika kuimarisha mazungumzo kutambua sauti za herufi moja zilizofunzwa katika maneno kutambua majina ya herufi zinazowakilisha sauti lengwa katika kuimarisha stadi ya kusoma 	<ul style="list-style-type: none"> Mwanafunzi atambue sauti /t/, /l/, /n/ na /o/ katika maneno. Mwanafunzi asikilize mwalimu anapotamka sauti lengwa, kisha atamke pamoja na mwalimu na mwishowe atamke akiwa peke yake, wawili wawili au kama darasa. Mwanafunzi atumie teknolojia (papaya) kutamkia sauti. Mwanafunzi atambue herufi inayowakilisha sauti lengwa kwa kutumia kadi za herufi. 	<ol style="list-style-type: none"> Ni sauti zipi unazojua kutamka? Unajua kusoma herufi na maneno? Unajua kuandika herufi na maneno?

		<p>d) kusoma herufi za sauti moja katika kujenga stadi ya kusoma</p> <p>e) kusoma maneno kwa kutumia silabi zinazotokana na sauti lengwa katika kujenga stadi ya kusoma</p> <p>f) kusoma vifungu vilivyo na maneno yaliyo na sauti lengwa ili kujenga stadi ya kusoma</p> <p>g) kuandika maumbo ya herufi zinazowakilisha sauti lengwa katika kuimarisha stadi ya kuandika</p> <p>h) kuchangamkia kutumia maneno yanayojumuisha sauti zilizofunzwa katika mawasiliano ya kila siku.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aambatanishe silabi kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa. • Mwanafunzi atenganishe silabi katika kutambua sehemu mbalimbali za maneno. • Wanafunzi waweza kushirikishwa kusikiliza mgeni mwalikwa mwenye umahiri wa kutamka sauti lengwa. • Mwanafunzi asome maneno kwa kutumia silabi na kuchanganua yaliyo marefu zaidi. • Wanafunzi wasome hadithi zilizo na maneno yaliyobeba sauti lengwa kama darasa au wawili wawili. • Mwanafunzi asikilize na kusoma hadithi kupitia vifaa vya kiteknolojia kama vile tarakilishi, projekta n.k. • Mwanafunzi afinyange na aandike maumbo ya herufi za sauti alizosoma hewani na vitabuni. • Mwanafunzi aandike maneno yaliyo na herufi za sauti alizofunzwa kwa kunakili aliyoandika mwalimu. 	
	Msamiati (Vipindi 3)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua sehemu za mwili katika mawasiliano</p> <p>b) kutumia majina ya sehemu za mwili katika kutunga sentensi</p> <p>c) kusoma majina ya sehemu za mwili katika kuimarisha stadi ya kusoma</p> <p>d) kuandika majina ya sehemu za mwili katika kuimarisha stadi ya kuandika</p> <p>e) kuchangamkia utunzaji wa sehemu za mwili katika kuimarisha afya.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aambanitishe kadi za maneno na sehemu za mwili za nje. • Mwanafunzi aweza kuonyeshwa video kuhusu sehemu za mwili za nje. • Mwanafunzi achore sehemu za mwili za nje. • Mwanafunzi afafanue maana ya msamiati wa sehemu za mwili. • Mwanafunzi asome hadithi baada ya mwalimu, kisha pamoja na mwalimu na baadaye akiwa peke yake au wawili wawili. • Mwanafunzi aweza kushirikishwa katika kuimba nyimbo na kukariri mashairi yanayohusu sehemu za mwili za nje. 	<p>1) Ni sehemu gani ya mwili unayoweza kuchora?</p> <p>2) Sehemu tofauti za mwili za nje zina umuhimu gani?</p>

			<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aandike majina ya sehemu za mwili za nje. • Mwanafunzi atunge sentensi kuhusu sehemu za mwili za nje. • Mwanafunzi achorewe sehemu za mwili kwenye tarakilishi ili atumie mbinu ya kuburura na kuweka kapuni ili kujazia mapengo. 	
	Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (Vipindi 2)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <ol style="list-style-type: none"> a) kutambua sehemu za mwili katika mawasiliano b) kueleza matumizi ya sehemu za mwili ili kuthamini mwili wake c) kusimulia visa kuhusu sehemu za mwili katika kujenga stadi ya kuzungumza d) kuthamini sehemu za mwili wake maishani. 	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi ataje sehemu za mwili za nje. • Mwanafunzi achore picha za sehemu mbalimbali za mwili za nje. • Wanafunzi wajaadili sehemu za mwili za nje na umuhimu wake katika vikundi. • Mwanafunzi atoe maelezo kuhusu sehemu za mwili za nje. • Mwanafunzi azungumzie sehemu zake za mwili za nje. • Mwanafunzi aweza kuimba nyimbo na kukariri mashairi mepesi kuhusu sehemu za mwili za nje. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Kuna sehemu ngapi za mwili za nje? 2) Sehemu za mwili za nje hutumiwa kufanya nini? 3) Ni sehemu ipi ya mwili ya nje iliyo muhimu zaidi?
	Sarufi: Umoja na wingi wa majina (Vipindi 3)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <ol style="list-style-type: none"> a) kutambua majina ya sehemu za mwili katika umoja na wingi ili kuimarisha mawasiliano b) kutumia majina ya sehemu za mwili kwenye sentensi katika umoja na wingi ili kuimarisha mawasiliano c) kusoma sentensi zinazojumuisha sehemu za mwili katika umoja na wingi ili kuimarisha stadi ya kusoma 	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi atunge sentensi kwa kurejelea sehemu za mwili katika umoja na wingi. • Mwanafunzi asome sentensi zinazorejelea sehemu za mwili katika umoja na wingi. • Mwanafunzi aandike sentensi zinazorejelea sehemu za mwili katika umoja na wingi. • Mwanafunzi aweza kujaza mapengo kwa kutumia majina ya sehemu za mwili katika umoja na wingi. • Mwanafunzi aweza kunakili sentensi katika umoja na wingi. • Wanafunzi watunge sentensi katika umoja na wingi kwa vikundi. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Je, ni sehemu gani za mwili unazoweza kutaja katika umoja na wingi? 2) Je, waweza kutumia majina gani ya sehemu za mwili katika sentensi?

		<p>d) kuandika sentensi zinazojumuisha sehemu za mwili katika umoja na wingi ili kuimarisha stadi ya kuandika</p> <p>e) kufurahia kurejelea sehemu za mwili katika umoja na wingi katika mawasiliano.</p>		
<p>Umilisi wa kimsingi unaokuzwa: Mawasiliano na ushirikiano – kupanga kujadiliana umuhimu wa sehemu za mwili; Kufanya kazi kwa vikundi Hamu ya ujifunzaji: hamu ya kutaka kujua vitu vingine katika umoja na wingi Ujuzi wa kidijitali :kuna mapendekezo ya kutumia vifaa vya teknolojia kufunzia Ubunifu: utunzi wa sentensi katika umoja na wingi.</p>				
<p>Uhusiano na masuala mtambuko na Maadili: stadi za maisha – kujitambua na kujithamini anapotaja sehemu zake za mwili; kujionea fahari kwa maumbile yake uraia: utangamano wa kijamii - kushirikiana katika vikundi.</p>		<p>Uhusiano na maadili: Uwajibikaji mapenzi kwa mwili wake.</p>		
<p>Uhusiano na Masomo mengine: English Activities, Environmental Activities na Religious Activities</p>		<p>Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji: kuisitiza kuhusu utunzaji wa mwili miongoni mwa wenzake kulinda usiri wa mwili wake.</p>		
<p>Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji: kazi ya vikundi shughuli za vikundi vya ushirika shuleni michezo.</p>		<p>Mapendekezo ya Tathmini:</p> <ul style="list-style-type: none"> • kuchunguza jinsi anavyotambua sehemu mbalimbali za mwili • kuchunguza anavyotamka sauti zilizofunzwa • kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa • kuchunguza jinsi anavyotumia umoja na wingi wa majina katika sentensi. 		

Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • anatamka sauti lengwa ifaavyo na kwa ukakamavu • anaelezea sehemu lengwa za mwili ifaavyo • anatumia majina ya sehemu lengwa za mwili kwa ubunifu katika sentensi • anasoma kwa ufasaha • anajibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa ubunifu na usahihi • anatumia umoja na wingi wa majina lengwa katika kutunga sentensi ifaavyo kila wakati • anaandika kwa hati nadhifu na kwa haraka. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • anatamka sauti lengwa vyema • anataja sehemu lengwa za mwili ifaavyo • anatumia majina ya sehemu lengwa za mwili ifaavyo katika sentensi • anasoma ifaavyo • anajibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi • anatumia umoja na wingi wa majina lengwa katika kutunga sentensi ifaavyo • anaandika kwa hati bora. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto za kutamka baadhi ya sauti lengwa • anataja sehemu lengwa za mwili • ana changamoto za kutumia baadhi ya majina ya sehemu lengwa za mwili ifaavyo katika sentensi • anasoma baadhi ya kazi anazopewa • anajibu baadhi ya maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi • ana changamoto za kutumia umoja na wingi wa baadhi ya majina lengwa kutunga sentensi • anaandika kwa hati zinazosomeka. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto za kutamka sauti lengwa • ana changamoto za kutaja baadhi ya sehemu lengwa za mwili • ana changamoto katika kusoma • ana changamoto za kutumia majina ya sehemu lengwa za mwili ifaavyo katika sentensi • ana changamoto katika kujibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi • ana changamoto za kutumia umoja na wingi wa majina lengwa kutunga sentensi • ana changamoto katika kuandika.

MADA	MADA NDOGO	MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA	MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI	MASWALI DADISI
Usafi wa Mwili	Sauti na majina ya herufi za Kiswahili (<i>Vipindi 8</i>)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutamka sauti nne za herufi moja katika kuimarisha mazungumzo</p> <p>b) kutambua sauti za herufi moja zilizofunzwa katika maneno ili kuimarisha mazungumzo</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi atambue sauti /w/, /e/, /i/ na /h/ katika maneno. • Mwanafunzi amsikilize mwalimu akitamka sauti lengwa, kisha atamke pamoja na mwalimu na mwishowe atamke akiwa peke yake, wawili wawili na kama darasa. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Ni sauti zipi unazojua kutamka? 2) Unajua kusoma herufi na maneno yapi? 3) Unajua kuandika herufi na maneno yapi?

		<p>c) kutambua majina ya herufi zinazowakilisha sauti lengwa katika kuimarisha stadi ya kusoma</p> <p>d) kusoma herufi za sauti moja katika kujenga stadi ya kusoma</p> <p>e) kusoma maneno kwa kutumia silabi zinazotokana na sauti lengwa katika kujenga stadi ya kusoma</p> <p>f) kusoma vifungu vilivyo na maneno yaliyo na sauti lengwa ili kujenga stadi ya kusoma</p> <p>g) kuandika maumbo ya herufi zinazowakilisha sauti lengwa katika kuimarisha stadi ya kuandika</p> <p>h) kuchangamkia kutumia maneno yanayojumuisha sauti zilizofunzwa katika mawasiliano ya kila siku.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi atumie teknolojia (papaya) kusikiliza matamshi ya sauti lengwa. • Mwanafunzi atambue herufi zinazowakilisha sauti lengwa kwa kutumia kadi za herufi. • Mwanafunzi aambatanishe silabi kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa. • Mwanafunzi atenganishe silabi katika kutambua sehemu mbalimbali za maneno. • Wanafunzi waweza kusikiliza mgeni mwalikwa mwenye umahiri wa kutamka sauti lengwa. • Mwanafunzi afinyange maumbo ya herufi za sauti lengwa. • Mwanafunzi aandike maumbo ya herufi za sauti alizosoma hewani na vitabuni. • Mwanafunzi asome maneno kwa kutumia silabi na kuchanganua yaliyo marefu zaidi. • Wanafunzi waweza kusoma hadithi zilizo na maneno yaliyobeba sauti lengwa kama darasa au wawili wawili. • Mwanafunzi aweza kusikiliza na kusoma hadithi kupitia vifaa vya kiteknolojia kama vile tarakilishi, projekta n.k. • Mwanafunzi aandike imla ya maneno yaliyo na herufi za sauti alizofunzwa na kuyaandika. 	
	Msamiati (<i>Vipindi 2</i>)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua msamiati wa usafi wa mwili katika kujenga msamiati kwa mawasiliano</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi atambue msamiati wa usafi wa mwili k.m. kukata kucha, kunyoa nywele, kusafisha nguo, kusugua meno, kunawa mikono, kuoga na kufuta kamasi. 	<p>1) Je, kwa nini unapenda kukaa ukiwa safi?</p> <p>2) Ni vitendo vipi vinavyotusaidia kukaa tukiwa safi?</p>

		<p>b) kueleza maana ya msamiati wa usafi wa mwili ili kuimarisha mawasiliano</p> <p>c) kusoma msamiati wa usafi wa mwili katika kuimarisha stadi ya kusoma</p> <p>d) kutumia msamiati wa usafi wa mwili katika sentensi</p> <p>e) kuandika maneno yanayohusiana na usafi wa mwili katika kuimarisha stadi ya kuandika</p> <p>f) kuthamini usafi wa mwili katika maisha ya kila siku.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi atumie msamiati uliyofunzwa katika sentensi sahihi. • Mwanafunzi aandike maneno yaliyofunzwa • Mwanafunzi aweza kupewa kadi za maneno asome kwa sauti. • Wanafunzi waweza kuambatanisha maneno waliofunzwa na michoro. • Wanafunzi waweza kuimba nyimbo na kukariri mashairi kuhusu usafi wa mwili. • Wanafunzi waweza kuwekwa katika vikundi wajiiliane kuhusu usafi wa mwili. • Wanafunzi waweza kutazama video kuhusu vitendo tofauti vya usafi wa mwili. 	
	<p>Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (Vipindi 2)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua sehemu za mwili zinazopaswa kuangaziwa zaidi katika usafi katika kuimarisha mazungumzo</p> <p>b) kusikiliza hadithi kuhusu usafi wa mwili katika kurejelea stadi ya kusikiliza</p> <p>c) kufahamu masimulizi aliyoyasikiliza katika kurejelea stadi ya kusikiliza</p> <p>d) kusimulia visa vinavyohusu usafi katika kurejelea stadi ya kuzungumza</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi asimuliwe hadithi kuhusu usafi kisha ashiriki katika mjadala kuhusu usafi wa mwili. • Wanafunzi wasimuliane visa kuhusu usafi. • Wanafunzi wajiiliane kuhusu sehemu za mwili zinazopaswa kuangaziwa zaidi katika usafi. • Wanafunzi wajiiliana kuhusu umuhimu wa usafi maishani. • Mwanafunzi aweza kusikiliza mgeni mwalikwa k.m daktari au nesi akizungumzia juu ya usafi. • Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali ya hadithi na maelezo aliyosikia kuhusu usafi. • Mwanafunzi aweza kuhusishwa katika kuimba nyimbo na kukariri mashairi kuhusu usafi wakiigiza vitendo vya usafi. 	<p>1) Je, ni sehemu zipi za mwili zinazopaswa kuangaziwa zaidi katika usafi?</p> <p>2) Je, usafi una umuhimu gani?</p> <p>3) Je, unaweza kusimulia kisa kuhusu usafi?</p>

		e) kufurahia masimulizi kuhusu usafi kila wakati katika mawasiliano.	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aweza kusikiliza nyimbo na mashairi yaliyorekodiwa kwenye vifaa vya kiteknolojia. 	
	Kusoma: Hadithi (Vipindi 3)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua msamiati uliotumiwa katika hadithi ili kuimarisha mawasiliano</p> <p>b) kusikiliza hadithi zikisomwa na mwalimu zinazohusu usafi wa mwili katika kujenga stadi ya kusoma</p> <p>c) kusoma hadithi zinazohusu usafi wa mwili katika kujenga stadi ya kusoma</p> <p>d) kufahamu hadithi aliyoisoma na aliyosomewa kuhusu usafi wa mwili ili kuimarisha mawasiliano</p> <p>e) kudumisha usafi katika maisha ya kila siku.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi ajadili picha zilozjumuishwa kwenye hadithi. • Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi. • Mwanafunzi athibitisha utabiri wake baada ya kusoma na kusomewa hadithi. • Mwanafunzi asome hadithi baada ya mwalimu, kisha pamoja na mwalimu na baadaye akiwa peke yake au wawili wawili. • Mwanafunzi aeleeze maana na matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi. • Mwanafunzi asikilize mwalimu anaposoma hadithi, asome pamoja na mwalimu kisha asome peke yake. • Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi ya mwalimu au hadithi iliyorekodiwa kuhusu usafi. • Mwanafunzi waweza kusomeana hadithi wakiwa wawili wawili na katika vikundi. • Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kupitia vifaa vya kiteknolojia kama vile tarakilishi, projekta n.k. • Mwanafunzi asome maneno yanayohusu usafi kwenye kadi. • Mwanafunzi aweza kuhusishwa katika kuigiza vitendo vinavyohusu usafi wa mwili. • Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kwa kutumia jitabu mbele ya darasa. • Mwanafunzi aweza kuonyeshwa picha zinazoashiria vitendo vya usafi wa mwili. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Je, ni nini maana ya usafi gani? 2) Je, ni matayarisho yapi unayofanya kabla ya kuja shuleni? 3) Unafikiri ni nini kitakachotokea katika hadithi hii? 4) Je, ni hadithi gani umewahi kusoma?

			<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aulize na kujibu maswali kutokana na hadithi. 	
	<p>Sarufi: Matumizi ya huyu na hawa (Vipindi 2)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua matumizi ya huyu na hawa katika mawasiliano</p> <p>b) kusoma sentensi zinazojumuisha huyu na hawa ili kuimarisha mawasiliano</p> <p>c) kutumia huyu na hawa katika sentensi katika kuimarisha mawasiliano</p> <p>d) kuandika sentensi kwa kutumia huyu na hawa katika kuimarisha stadi ya kuandika</p> <p>e) kuthamini utunzi wa sentensi sanifu katika mawasiliano.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi atunge sentensi zenye matumizi ya huyu na hawa k.m. Huyu anakata kucha - Hawa wanakata kucha; Huyu anachana nywele - Hawa wanachana nywele. • Mwanafunzi aandike sentensi zinazojumuisha matumizi ya huyu na hawa. • Mwanafunzi asome sentensi zinazojumuisha matumizi ya huyu na hawa. • Mwanafunzi aweza kujaza mapengo kwa kutumia huyu na hawa. • Mwanafunzi aweza kujaza mapengo kwenye tarakilishi kupitia mchezo wa kuburura na kutia kapuni. 	<p>1) Je, unajua ni kwa nini tunatumia huyu na hawa?</p> <p>2) Je, utatumia neno lipi kuonyesha kwamba mtu ni mmoja?</p> <p>3) Watu wakiwa wengi unaonyesha vipi?</p>
<p>Umilisi wa kimsingi unaokuzwa: Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashiriki katika makundi kuimba na kukariri mashairi, kusimulia na kujadiliana Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi atajenga msingi wa kusoma na kuchunguza zaidi kuhusu usafi Ujuzi wa kidijitali : vifaa vya teknolojia vinatumiwa katika kusimulia, kuimba na kukariri mashairi Ubunifu: mwanafunzi anajenga ubunifu wake anaposimulia na kutunga sentensi akitumia maneno ya vitendo.</p>				
<p>Uhusiano na masuala mtambuko: Elimu ya afya - usafi wa kibinafsi Wanapozingatia usafi wa mwili wao.</p>			<p>Uhusiano na Maadili: Uwajibikaji.</p>	
<p>Uhusiano na Masomo mengine: English Activities, Environmental Activities, Health and Nutrition na Religious Activities</p>			<p>Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji: kusesitiza kuhusu utunzaji wa mwili miongoni mwa wenzake kulinda usiri wa mwili wake.</p>	

<p>Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji: kazi ya vikundi shughuli za vikundi vya ushirika shuleni michezo nyimbo na mashairi kuhusu usafi wa mwili.</p>	<p>Mapendekezo ya Tathmini:</p> <ul style="list-style-type: none"> • kuuliza maswali kuhusu jinsi ya kuzingatia usafi wa mwili • kuchunguza anavyotamka sauti zilizofunzwa • kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa • kuchunguza jinsi anavyotumia huyu na hawa katika sentensi.
--	--

Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • anatamka sauti lengwa kwa ufasaha • anaelezea jinsi ya kuzingatia usafi wa mwili kwa ufasaha • anatumia msamiati wa usafi wa mwili kwa ubunifu katika sentensi • anasoma kwa ufasaha • anajibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa ubunifu na usahihi • anatumia huyu na hawa kutunga sentensi kwa ubunifu • anaandika kwa hati nadhifu. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • anatamka sauti lengwa vyema • anaelezea jinsi ya kuzingatia usafi wa mwili • anatumia msamiati unaotumika katika usafi wa mwili ifaavyo katika sentensi. • anasoma ifaavyo • anajibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi • anatumia huyu na hawa kutunga sentensi ifaavyo • anaandika kwa hati bora. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto za kutamka baadhi ya sauti lengwa vyema • anaelezea jinsi ya kuzingatia usafi wa mwili • ana changamoto za kutumia baadhi ya msamiati ya usafi wa mwili ifaavyo katika sentensi • anasoma baadhi ya kazi anazopewa • anajibu baadhi ya maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi • ana changamoto za kutumia umoja na wingi wa majina lengwa katika kutunga sentensi • anaandika kwa hati zinazosomeka. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto za kutamka sauti lengwa vyema • ana changamoto za kuelezea jinsi ya kuzingatia usafi wa mwili • ana changamoto za kutumia msamiati usafi wa mwili ifaavyo katika sentensi • ana changamoto katika kusoma • Ana changamoto katika kujibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi • ana changamoto katika kutumia umoja na wingi wa majina lengwa katika kutunga sentensi • ana changamoto katika kuandika.

MADA	MADA NDOGO	MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA	MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI	MASWALI DADISI
Vyakula vya kiasilia	Sauti na majina ya herufi za Kiswahili (Vipindi 8)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <ol style="list-style-type: none"> kutamka sauti nne za herufi moja katika kuimarisha stadi ya kuzungumza kutambua sauti za herufi moja zilizofunzwa katika maneno katika kuimarisha stadi ya kuzungumza kutambua majina ya herufi zinazowakilisha sauti lengwa katika kuimarisha stadi ya kusoma kusoma herufi za sauti moja katika kuimarisha stadi ya kusoma kusoma maneno kwa kutumia silabi zinazotokana na sauti lengwa katika kuimarisha stadi ya kusoma kusoma vifungu vilivyo na maneno yaliyo na sauti lengwa katika kuimarisha stadi ya kusoma kuandika maumbo ya herufi yanayowakilisha sauti lengwa 	<ul style="list-style-type: none"> Mwanafunzi atambue sauti lengwa /s/, /b/, /y/ na /z/ katika maneno. Mwanafunzi asikilize mwalimu akitamka sauti lengwa, kisha atamke pamoja na mwalimu na mwishowe atamke akiwa peke yake, wawili na kama darasa. Mwanafunzi atumie teknolojia (papaya) kutamkia sauti. Mwanafunzi atambue herufi zinazowakilisha sauti lengwa kwa kutumia kadi za herufi. Mwanafunzi aambatanishe silabi kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa. Mwanafunzi atenganishe silabi katika kutambua sehemu mbalimbali za maneno. Mwanafunzi waweza kushirikishwa kusikiliza mgeni mwalikwa mwenye umahiri wa kutamka sauti lengwa. Mwanafunzi aweza kufinyanga maumbo ya herufi inayowakilisha sauti iliyofunzwa. Mwanafunzi aandike maumbo ya herufi za sauti alizosoma hewani na vitabuni. Mwanafunzi asome maneno kwa kutumia silabi au kwa kugawa maneno marefu katika sehemu ndogo ndogo ili kuyasoma kwa urahisi. Mwanafunzi wasome hadithi zilizo na maneno yanayobeba sauti lengwa kama darasa au wawili wawili. 	<ol style="list-style-type: none"> Ni sauti zipi unazoweza kutamka? Unajua kusoma herufi na maneno yapi? Unajua kuandika herufi na maneno yapi?

		katika kuimarisha stadi ya kusoma h) kuchangamkia kutumia maneno yanayojumuisha sauti lengwa katika mawasiliano ya kila siku.	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi anaweza kushirikishwa kusikiliza na kusoma hadithi kupitia vifaa vya kiteknolojia kama vile tarakilishi, projekta n.k. • Mwanafunzi ashirikishwe katika kuandika imla ya maneno yaliyo na herufi za sauti alizofunzwa na kuyaandika. 	
	Msamiati (Vipindi 2)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: a) kutambua vyakula vya kiasili ili kuimarisha lishe bora b) kusoma majina ya vyakula mbalimbali ili kuimarisha stadi ya kusoma c) kuandika majina ya vyakula katika kuimarisha stadi ya kuandika d) kutumia majina ya vyakula katika sentensi sahihi e) kuthamini vyakula vya kiasili katika maisha ya kila siku.	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi atambue vyakula mbalimbali vya kiasili kwa kutumia vyakula halisi, picha na michoro kama vile mihogo, viazi, mahindi, maharagwe, mboga na matunda. • Mwanafunzi atumie msamiati aliyofunzwa kutunga sentensi. • Mwanafunzi aandike maneno aliofunzwa. • Mwanafunzi aweza kupewa kadi za majina ya vyakula vya kiasili asome kwa sauti. • Wanafunzi waweza kuambatanisha majina ya vyakula halisi au michoro na majina yavyo. • Wanafunzi waweza kuimba nyimbo na kukariri mashairi kuhusu vyakula vya kiasili. • Wanafunzi waweza kuandika majina ya vyakula wanavyovijua katika vikundi. • Wanafunzi waweza kutazama picha za vyakula mbalimbali kupitia kwa vifaa vya kiteknolojia. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Unapenda waweza kutaja chakula kipi? 2) Vyakula vipi hukuzwa shambani?
	Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (Vipindi 2)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: a) kusikiliza masimulizi kuhusu vyakula vya kiasili katika kuimarisha stadi ya kusikiliza b) kusimulia visa vinavyohusu	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi asimulie hadithi kuhusu vyakula vya kiasili. • Wanafunzi wajaadiliane kuhusu umuhimu wa vyakula vya kiasili. • Wanafunzi wasimuliane visa kuhusu vyakula vya kiasili. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Kwa nini tunakula chakula? 2) Je, umuhimu wa vyakula vya kiasili ni upi?

		<p>vyakula vya kiasili katika kuimarisha stadi ya kuzungumza</p> <p>c) kufahamu masimulizi aliyosikiliza katika kuimarisha stadi ya kusikiliza</p> <p>d) kufurahia vyakula vya kiasili katika maisha ya kila siku.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mtaalamu wa lische bora aweza kualikwa kuzungumzia juu ya vyakula vya kiasili. • Mwanafunzi aulize na kujibu maswali kutokana na maelezo aliyosikia kuhusu vyakula vya kiasili. • Mwanafunzi aweza kuhusishwa katika kuimba nyimbo na kukariri mashairi kuhusu vyakula vya kiasili. • Mwanafunzi aweza kusikiliza nyimbo na mashairi yaliyorekodiwa kwenye vifaa vya kiteknolojia kuhusu vyakula vya kiasili. 	
	<p>Kusoma: Hadithi (Vipindi 3)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua msamiati uliotumiwa katika hadithi aliyosoma au kusomewa ili kuimarisha mawasiliano</p> <p>b) kusikiliza hadithi zikisomwa na mwalimu kuhusu vyakula vya kiasili ili kuimarisha stadi ya kusoma</p> <p>c) kusoma hadithi kuhusu vyakula vya kiasili katika kuimarisha stadi ya kusoma</p> <p>d) kufahamu hadithi aliyosoma na kusomewa kuhusu vyakula vya kiasili ili kupata ujumbe unaolengwa</p> <p>e) kufurahia vyakula vya kiasili maishani.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi. • Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi. • Mwanafunzi afahamu matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi. • Mwanafunzi asikilize mwalimu anaposoma hadithi, asome pamoja na mwalimu kisha asome peke yake, wawili wawili au katika vikundi. • Mwanafunzi asikilize hadithi ya mwalimu au hadithi iliyorekodiwa kuhusu vyakula vya kiasili. • Mwanafunzi aweza kusoma na kusomewa hadithi kupitia vifaa vya kiteknolojia kama vile tarakilishi, projekta n.k. • Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kwa kutumia jitabu mbele ya darasa. • Mwanafunzi athibitishe utabiri wake baada ya kusoma na kusomewa hadithi. • Mwanafunzi atoe muhtasari wa hadithi. • Mwanafunzi aulize na kujibu maswali kutokana na 	<p>1) Je, unaona nini katika picha?</p> <p>2) Unadhani ni nini kitakachotokea katika hadithi?</p> <p>3) Unakumbuka hadithi gani uliyoisoma?</p>

			hadithi.	
	Sarufi: Matumizi na – angu na – etu (Vipindi 2)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: a) kutambua matumizi ya – angu na – etu katika mawasiliano b) kutumia – angu na – etu katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano c) kufurahia kutumia – angu na – etu katika mawasiliano.	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi atunge sentensi zenye matumizi ya –angu na –etu. • Mwanafunzi aandike sentensi zenye kuhusisha –angu na –etu. • Mwanafunzi asome sentensi zenye kutumia maneno –angu na –etu. • Mwanafunzi aweza kujaza mapengo kwa kutumia –angu na –etu. • Mwanafunzi aweza kupewa zoezi la kujaza mapengo kwa tarakilishi (mchezo wa kuvuta na kutia kapuni). 	1) Je, ni maneno gani tunayotumia kuonyesha kuwa kitu ni chako au ni chenu?
Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:				
<ul style="list-style-type: none"> • Mawasiliano na ushirikiano – kujadili katika makundi au wawili wawili • Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi atajenga msingi wa kujua vyakula zaidi • Ujuzi wa kidijitali –matumizi ya vifaa vya kiteknolojia. 				
Uhusiano na masuala mtambuko: elimu ya afya: magonjwa yanayohusiana na vyakula – kuthamini vyakula vya kiasili.			Uhusiano na Maadili: uwajibikaji	
Uhusiano na Masomo mengine: Health and Nutrition Activities na Environmental Activities			Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji: kuwahamasisha wengine katika jamii kuhusu umuhimu wa vyakula vya kiasili.	
Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji: <ul style="list-style-type: none"> • kazi ya vikundi • michezo • nyimbo na Mashairi kuhusu usafi wa mwili. 			Mapendekezo ya Tathmini: <ul style="list-style-type: none"> • kuuliza maswali kuhusu vyakula vya kiasili • kuchunguza anavyotamka sauti zilizofunzwa • kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa • kuchunguza jinsi anavyotumia –angu na –etu katika sentensi. 	

Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • anatamka sauti lengwa kwa ufasaha • anaelezea mifano ya vyakula vya kiasili • anatumia msamiati wa vyakula vya kiasili kwa ubunifu katika sentensi • anasoma kwa ufasaha • anajibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa ubunifu na usahihi • anatumia -angu na -etu kutunga sentensi ifaavyo • anaandika kwa hati nadhifu. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • anatamka sauti lengwa vyema • anataja mifano ya vyakula vya kiasili • anatumia msamiati wa vyakula vya kiasili ifaavyo katika sentensi • Anasoma ifaavyo • anajibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi • anatumia -angu na -etu kutunga sentensi ifaavyo • Anaandika kwa hati bora. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto za kutamka baadhi ya sauti lengwa vyema • anataja mifano ya vyakula vya kiasili • ana changamoto za kutumia baadhi ya msamiati wa vyakula vya kiasili katika sentensi • anasoma baadhi ya kazi anazopewa • anajibu baadhi ya maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi • ana changamoto za kutumia -angu na -etu kutunga sentensi ifaavyo • ana changamoto katika kusoma. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto za kutamka sauti lengwa vyema • ana changamoto za kutaja mifano ya vyakula vya kiasili • ana changamoto za kutumia msamiati wa vyakula vya kiasili katika sentensi • ana changamoto katika kusoma • ana changamoto katika kujibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi • ana changamoto za kutumia -angu na -etu kutunga sentensi ifaavyo • ana changamoto katika kuandika.

GREDI YA PILI

MADA	MADA NDOGO	MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA	MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI	MASWALI DADISI
Shuleni	Sauti na majina ya herufi za Kiswahili (Vipindi 8)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutamka sauti nne za herufi moja ili kuimarisha mazungumzo</p> <p>b) kutambua sauti za herufi moja zilizofunzwa katika kujenga stadi ya kusikiliza</p> <p>c) kutambua majina ya herufi zinazowakilisha sauti lengwa katika kujenga stadi ya kusikiliza</p> <p>d) kusoma herufi za sauti moja katika kujenga stadi ya kusoma</p> <p>e) kusoma maneno kwa kutumia silabi zinazotokana na sauti lengwa katika kujenga stadi ya kusoma</p> <p>f) kusoma vifungu vilivyo na maneno yaliyo na sauti lengwa katika kujenga stadi ya kusoma</p> <p>g) kuandika herufi zinazowakilishwa na sauti lengwa katika kujenga stadi ya kuandika</p> <p>h) kuchangamkia kutumia maneno yanayojumuisha sauti zilizofunzwa katika mawasiliano ya kila siku.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aweza kutambua sauti /g/, /d/, /j/, na /r/ katika maneno. • Mwanafunzi asikilize mwalimu akitamka sauti lengwa, kisha atamke pamoja na mwalimu na mwishowe atamke akiwa peke yake, wawili wawili na kama darasa. • Mwanafunzi atambue sauti alizosoma katika maneno. • Mwanafunzi aweza kutumia teknolojia (papaya) kusikiliza matamshi ya sauti lengwa. • Mwanafunzi atambue herufi zinazowakilisha sauti lengwa kwa kutumia kadi za herufi. • Mwanafunzi aambatanishe silabi kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa. • Mwanafunzi atenganishe silabi katika kutambua sehemu mbalimbali za maneno. • Mwanafunzi aweza kumsikiliza mgeni mwalikwa akitamka sauti lengwa. • Mwanafunzi asome maneno kwa kutumia silabi au kwa kuyagawa maneno marefu katika sehemu fupi fupi. • Mwanafunzi aandike herufi za sauti alizosoma hewani na vitabuni. • Mwanafunzi aweza kufinyanga maumbo ya herufi. 	<p>1) Je, ni sauti zipi unazojua kutamka?</p> <p>2) Unajua kusoma herufi na maneno gani?</p> <p>3) Unajua kuandika herufi na maneno gani?</p>

			<ul style="list-style-type: none"> • Wanafunzi wasome hadithi zilizo na maneno yaliyobeba sauti lengwa wakiwa wawili wawili. • Mwanafunzi aweza kutumia vifaa vya kiteknolojia kama vile tarakilishi, projekta na kipasa sauti kusikiliza na kusoma hadithi. • Mwanafunzi anakili herufi na maneno yanayotokana na sauti alizofunzwa. • Mwanafunzi aandike maumbo ya herufi na maneno yaliyo na herufi za sauti alizofunzwa. • Mwanafunzi asikilize imla inayojumuisha maneno yaliyo na herufi za sauti lengwa na kuyaandika. 	
	<p>Kusikiliza na Kuzungumza: Maamkuzi ya nyakati za siku. (Vipindi 2)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <ol style="list-style-type: none"> a) kutambua maneno yatumiwayo katika maamkuzi ya nyakati za siku shuleni kwa mawasiliano mwafaka b) kuamkua na kuitikia maamkuzi ya nyakati za siku shuleni katika kuimarisha mawasiliano c) kusoma maneno yanayotumiwa katika maamkuzi shuleni katika kuimarisha stadi ya kusoma d) kufafanua umuhimu wa salamu shuleni ili kuimarisha mawasiliano e) kufurahia kuamkua wenzake, wafanyakazi na walimu shuleni katika kujenga mshikamano wa jamii. 	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aigize maamkuzi mbalimbali ya nyakati za siku k.m habari ya asubuhi, jioni, mchana, umeamkaje na umeshindaje. • Mwanafunzi aweza kuonyeshwa mchoro wa watu wawili wakisalimiana halafu aongozwe katika kujadili picha. • Wanafunzi wasalimiane na kisha washirikishwe katika mjadala kuhusu maamkuzi. • Wanafunzi waweza kuwekwa katika vikundi ili wjadili umuhimu wa maamkuzi. • Mwanafunzi aweza kutazama video inayoonyesha watu wakitumia maamkuzi ya nyakati za siku. • Mwanafunzi asome maamkuzi ya nyakati za siku katika kadi na chati. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Tunaamkuana vipi wakati wa asubuhi, mchana na jioni? 2) Kwa nini tunasalimiana shuleni?

	<p>Msamiati (Vipindi 2)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua kwa kutaja msamiati wa shuleni katika kuimarisha umilisi wa lugha</p> <p>b) kutumia msamiati wa shuleni katika mawasiliano ya kila siku</p> <p>c) kusoma maneno na sentensi zinazojumuisha msamiati wa shuleni katika kuimarisha stadi ya kusoma</p> <p>d) kuandika maneno na sentensi fupi kuhusu shule ili kuimarisha stadi ya kuandika</p> <p>e) kufurahia kutumia msamiati wa shule katika mawasiliano ya kila siku.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aonyeshwe vifaa halisi, picha au michoro ya vitu vinavyopatikana shuleni kama vile ofisi, maktaba, vyoo, darasa, bendera na gwaride. • Mwanafunzi achore maumbo ya vifaa vinavyopatikana shuleni. • Wanafunzi waambatanishe kadi za maneno na vifaa halisi wakiwa katika vikundi. • Wanafunzi waweza kushiriki katika nyimbo na mashairi kuhusu shule. • Mwanafunzi aandike majina ya vitu vinavyopatikana shuleni. • Mwanafunzi asome msamiati wa shuleni katika kadi au chati. • Mwanafunzi atunge na asoma sentensi akitumia msamiati wa shuleni. 	<p>1) Je, unajua vifaa gani vinavyopatikana shuleni?</p> <p>2) Taja vifaa mbalimbali vinavyopatikana shuleni na umuhimu wake.</p>
	<p>Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (Vipindi 2)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutaja majina ya vitu vinavyopatikana shuleni ili kuimarisha stadi ya kuzungumza</p> <p>b) kuelezea vitu vinavyopatikana shuleni ili kuimarisha stadi ya kusikiliza</p> <p>c) kusikiliza kwa makini masimulizi ili kuimarisha stadi ya kusikiliza</p> <p>d) kusimulia kuhusu vitu mbalimbali vinavyopatikana shuleni ili kuimarisha stadi ya kusikiliza</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi asimulie kisa kuhusu shule. • Mwanafunzi ashiriki katika mjadala kuhusu vifaa vinavyopatika shuleni. • Mwanafunzi afanue umuhimu wa vitu vinavyopatika shuleni. • Mwanafunzi aweza kushiriki katika nyimbo au mashairi kuhusu vifaa vinavyopatika shuleni. • Mwanafunzi atazame picha na michoro inayoonyesha vifaa vinavyopatika shuleni wajadiliane katika vikundi. 	<p>1) Ni vifaa vipi vinavyopatikana shuleni?</p> <p>2) Ni nani anayetumia vifaa hivyo?</p>

		e) kuthamini umuhimu wa vitu vinavyopatikana shuleni.		
	Kusoma: Hadithi (<i>Vipindi 3</i>)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: a) kutambua picha za vitu vinavyopatikana shuleni katika kujenga stadi ya kusoma b) kuelezea picha katika hadithi ili kuimarisha stadi ya kuzungumza c) kusikiliza hadithi zikisomwa na mwalimu kuhusu vitu vinavyopatikana shuleni ili kuimarisha umakinifu d) kusoma hadithi kuhusu shule ili kuimarisha stadi ya kusoma e) kufahamu hadithi aliyosoma na aliyosomewa katika kupata mafunzo ya hadithi f) kuchangamkia kusoma hadithi kuhusu shule.	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi. • Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi. • Mwanafunzi afahamu matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi. • Mwanafunzi asikize mwalimu anaposoma hadithi kisha asome pamoja na mwalimu na baadaye asome peke yake kwa sauti. • Wanafunzi wasomeane hadithi wakiwa wawili wawili au katika vikundi. • Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi ikisomwa kwenye vifaa vya teknolojia k.v. tarakilishi na kinasasauti na kufuatilia yanayosomwa kwenye projekta. • Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kutoka kwa jitabu mbele ya darasa. • Mwanafunzi athibitisha utabiri wake baada ya kusoma hadithi. • Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali yanayotokana na hadithi aliyosoma na kusomewa. • Mwanafunzi atoe muhtasari wa hadithi aliyosoma au kusomewa. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Unaona nini katika picha? 2) Ni nini kitatendeka katika hadithi? 3) Ni nani wahusika katika hadithi?
	Msamiati: Nambari 11-50 (<i>Vipindi 3</i>)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: a) kutambua nambari 11-50 kwa maneno ili kuimarisha mawasiliano	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi asome majina ya nambari 11-50. • Wanafunzi wasome kadi za nambari 11-50 na majina yake ili kuziambatanisha katika vikundi. • Mwanafunzi aandike nambari 11-50. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Andika nambari gani kati ya 11 hadi 50? 2) Taja 11-50 kwa Kiswahili.

		<p>b) kusoma nambari 11-50 kwa maneno ili kujenga stadi ya kusoma</p> <p>c) kuandika nambari 11-50 kwa maneno ili kujenga stadi ya kuandika</p> <p>d) kuchangamkia kutumia nambari 11-50 kwa maneno katika mazungumzo yake.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Wanafunzi waweza kupanga upya majina yaliyoparaganywa ya nambari 11-50 wakiwa wawili wawili au katika vikundi. • Mwanafunzi atunge sentensi akitumia majina ya nambari 11-50. • Mwanafunzi aweza kutazama vibonzo vikitaja nambari 11 hadi 50 kwenye tarakilishi. 	<p>3) Tumia nambari 11-50 katika sentensi.</p>
	<p>Sarufi: Matumizi ya – ako na -enu (Vipindi 2)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze;</p> <p>a) kutambua matumizi yafaayo ya -ako na -enu katika mawasiliano</p> <p>b) kusoma sentensi zinazojumuisha -- ako na -enu katika kujenga stadi ya kusoma</p> <p>c) kutumia -ako na -enu katika sentensi katika kuimarisha mawasiliano</p> <p>d) kuandika sentensi zinazohusisha – ako na -enu katika kuimarisha stadi ya kuandika</p> <p>e) kuthamini matumizi ya -ako na – enu katika mawasiliano ya kila siku.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi atunge sentensi zenye matumizi ya -ako na -enu. • Mwanafunzi aandike sentensi zinazohusisha -ako na -enu. • Mwanafunzi asome sentensi zenye kutumia maneno – -ako na -enu. • Mwanafunzi aweza kujaza mapengo kwa kutumia -ako na -enu. • Mwanafunzi aweza kupewa zoezi la kujaza mapengo kwa tarakilishi (mchezo wa kuburura na kutia kapuni). 	<p>1) Je, ni maneno gani unayoweza kutumia kuonyesha kitu ni cha mwenzako?</p>
<p>Umilisi wa kimsingi unaokuzwa: Mawasiliano na ushirikiano – wanafunzi wanashiriki katika makundi Ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza Kujiamini/kujithamini - kuigiza na kusimulia.</p>				

<p>Uhusiano na masuala mtambuko na maadili: uraia – utangamano wa kijamii wanafunzi watangamane na kufanya kazi pamoja.</p>	<p>Uhusiano na Maadili: Uwajibikaji.</p>
<p>Uhusiano na masomo mengine: English Activities, Literacy and Indigenous Languages, Environmental activities.</p>	<p>Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji: kuwahamasisha wengine katika jamii kuhusu umuhimu wa shule.</p>
<p>Mapendekezo ya shughuli zingine zilioratibiwa za ujifunzaji:</p> <ul style="list-style-type: none"> • kazi ya vikundi • michezo • nyimbo na mashairi kuhusu usafi wa mwili. 	<p>Mapendekezo ya Tathmini:</p> <ul style="list-style-type: none"> • kuuliza maswali kuhusu shuleni • kuchunguza anavyotamka sauti zilizofunzwa • kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa • kuchunguza jinsi anavyotumia -ako na -enu katika sentensi.

Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • anatamka sauti lengwa kwa ukakamavu na ufasaha • anatumia msamiati wa shuleni katika sentensi ifaavyo na kwa ubunifu • anasoma kwa ufasaha • anatumia nambari kumi na moja hadi hamsini kwa ubunifu katika sentensi • anajibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa ubunifu na usahihi 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • anatamka sauti lengwa vyema • anatumia msamiati wa shuleni ifaavyo katika sentensi • anasoma ifaavyo. • anatumia nambari kumi na moja hadi hamsini ifaavyo katika sentensi • anajibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto katika kutamka baadhi ya sauti lengwa vyema • ana changamoto katika kutumia baadhi ya msamiati wa shuleni katika sentensi • ana changamoto kiasi katika kusoma • ana changamoto za kutumia baadhi ya nambari kutoka kumi na moja hadi hamsini katika sentensi • anajibu baadhi ya maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto katika kutamka sauti lengwa • ana changamoto katika kutumia msamiati wa shuleni katika sentensi • ana changamoto nyingi katika kusoma • ana changamoto za kutumia majina ya nambari kutoka kumi na moja hadi hamsini katika sentensi • ana changamoto katika kujibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi

<ul style="list-style-type: none"> • anatumia -ako na -enu kutunga sentensi ifaavyo kila wakati • anaandika kwa hati nadhifu na kwa haraka. 	<ul style="list-style-type: none"> • anatumia -ako na -enu kutunga sentensi ifaavyo • anaandika kwa hati zinazosomeka. 	<ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto katika kutumia -ako na -enu kutunga sentensi ifaavyo • anaandika kwa hati zinayosomeka. 	<ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto katika kutumia -ako na -enu kutunga sentensi ifaavyo • ana changamoto katika kuandika.
---	--	---	--

MADA	MADA NDOGO	MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA	MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI	MASWALI DADISI
Haki Zangu	Sauti na majina ya herufi za Kiswahili (Vipindi 6)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <ol style="list-style-type: none"> kutamka sauti nne za herufi moja katika kuimarisha stadi ya kuzungumza kutambua sauti za herufi moja zilizofunzwa katika maneno ili kuimarisha stadi ya kuzungumza kutambua majina ya herufi zinazowakilisha sauti lengwa katika kuimarisha stadi ya kusoma kusoma herufi za sauti moja kwa ufasaha ili kuimarisha stadi ya kusoma kusoma maneno kwa kutumia silabi zinazotokana na sauti lengwa kwa ufasaha ili kuimarisha stadi ya kusoma kusoma vifungu vilivyo na maneno yaliyo na sauti lengwa ili kuimarisha stadi ya kusoma kuandika herufi zinazowakilishwa na sauti lengwa ili kuimarisha stadi ya kuandika 	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aweza kutambua sauti /p/, /f/ na /v/ katika maneno. • Mwanafunzi asikilize mwalimu akitamka sauti lengwa, kisha atamke pamoja na mwalimu na mwishowe atamke akiwa peke yake, wawili wawili na kama darasa. • Mwanafunzi atambue sauti alizosoma katika maneno. • Mwanafunzi aweza kutumia teknolojia (papaya) kusikiliza matamshi ya sauti lengwa. • Mwanafunzi atambue herufi zinazowakilisha sauti lengwa kwa kutumia kadi za herufi. • Mwanafunzi aambatanishe silabi kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa. • Mwanafunzi atenganishe silabi katika kutambua sehemu mbalimbali za maneno. • Mwanafunzi aweza kumsikiliza mgeni mwalikwa akitamka sauti lengwa. • Mwanafunzi asome maneno kwa kutumia silabi au kwa kugawa maneno marefu katika sehemu ndogo ndogo. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Ni sauti zipi unazojua kutamka? 2) Unajua kusoma herufi na maneno gani? 3) Unajua kuandika herufi na maneno gani?

		<p>h) kuchangamkia kutumia maneno yanayojumuisha sauti zilizofunzwa katika mawasiliano ya kila siku.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aweza kufinyanga maumbo ya herufi. • Mwanafunzi aandike herufi za sauti alizosoma hewani na vitabuni. • Wanafunzi wasome hadithi zilizo na maneno yaliyobeba sauti lengwa wakiwa wawili wawili. • Mwanafunzi aweza kutumia vifaa vya kiteknolojia kama vile tarakilishi, projekta na kipasasauti kusikiliza na kusoma hadithi. • Mwanafunzi anakili herufi na maneno yanayotokana na sauti alizofunzwa. • Mwanafunzi aandike maumbo ya herufi na maneno yaliyo na herufi za sauti alizofunzwa. • Mwanafunzi asikilize imla inayojumuisha maneno yaliyo na herufi za sauti lengwa na kuyaandika. 	
	<p>Msamiati (Vipindi 3)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <ol style="list-style-type: none"> a) kutambua haki za watoto bila tatizo ili kukabiliana na maisha vilivyo b) kusoma msamiati kuhusu haki za watoto ili kuimarisha stadi ya kusoma c) kutunga sentensi akitumia msamiati wa haki za watoto ili kuwasiliana ifaavyo d) kuandika maneno na sentensi akitumia msamiati wa haki za watoto ili kuimarisha stadi ya kuandika e) kuthamini haki za watoto katika maisha ya kila siku. 	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi afafanue msamiati kuhusu haki za watoto k.v. ajira, kuishi, haki, kuelimisha, kupewa malezi bora, matibabu, kutoteswa, kupewa jina, chakula na mavazi. • Mwanafunzi ajadaliane na wenzake kuhusu maana za msamiati wa haki za watoto. • Mwanafunzi aandike msamiati wa haki za watoto. • Mwanafunzi atunge sentensi kwa kutumia msamiati wa haki za watoto. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Ni haki gani za watoto unazozijua? 2) Ni msamiati gani wa haki za watoto unaoweza kutumia katika sentensi?

	<p>Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (Vipindi 2)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <ol style="list-style-type: none"> kutaja haki zake ili kuimarisha ujuzi wa masuala yanayomwathiri kueleza umuhimu wa haki za watoto ili kutetea haki zake zinapokiukwa kusimulia kuhusu haki zake ili kujenga stadi ya kuzungumza kusikiliza masimulizi kuhusu haki za watoto ili kuimarisha umakinifu kuthamini haki za watoto ili kuzitetea maishani. 	<ul style="list-style-type: none"> Mwanafunzi ataje haki zake k.v. kuishi, elimu, kupewa malezi bora, matibabu, kutoteswa, kupewa jina, chakula na mavazi. Wanafunzi wajadili michoro, chati au picha zinazozingatia haki za watoto. Mwanafunzi aweza kusimulia kisa kuhusu haki za watoto. Mwanafunzi aweza kuimba nyimbo na kukariri mashairi kuhusu haki za watoto. Mwanafunzi aweza kutazama video kuhusu haki za watoto. Mwanafunzi aweza kusikiliza mgeni mwalikwa akizungumza kuhusu haki za watoto. Wanafunzi waweza kujadiliana kuhusu haki za watoto. 	<ol style="list-style-type: none"> Je, unajua haki zipi? zinazokuhusu? Haki za watoto zinakusaidiaje?
	<p>Kusoma: Hadithi (Vipindi 3)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <ol style="list-style-type: none"> kutambua picha kuhusu haki za watoto ili kuifahamu hadithi vizuri kusikiliza hadithi za mwalimu kuhusu haki za watoto katika kuimarisha stadi za kusikiliza na kusoma kusoma hadithi kuhusu haki za watoto katika kuimarisha stadi ya kusoma kufahamu hadithi aliyoisoma au aliyosomewa ili kupata mafunzo yanayolengwa 	<ul style="list-style-type: none"> Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi. Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi. Mwanafunzi athibitisha utabiri wake baada ya kusoma hadithi. Mwanafunzi adhihirishe ufahamu wa matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi. Mwanafunzi aweza kusikiliza mwalimu anaposoma hadithi kisha asome na mwalimu na baadaye asome peke yake, wakiwa wawili wawili au katika vikundi. 	<ol style="list-style-type: none"> Ni masuala yapi uliyojifunza katika hadithi uliyosoma? Ni haki zipi za watoto zimezingatiwa katika hadithi?

		e) kuchangamkia kusoma hadithi kuhusu haki za watoto ili kuendeleza stadi ya kusoma.	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi ikisomwa kwa kutumia vifaa vya kiteknolojia k.m. tarakilishi na projekta. • Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kutoka kwa jitabu mbele ya darasa. • Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali yanayotokana na hadithi aliyosoma au kusomewa. • Mwanafunzi atoe muhtasari wa hadithi aliyosoma au kusomewa. 	
	Sarufi: Matumizi ya vizuri na vibaya (Vipindi 2)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua matumizi yafaayo ya vizuri na vibaya katika mawasiliano</p> <p>b) kutumia vizuri na vibaya katika sentensi sahihi ili kuimarisha mawasiliano</p> <p>c) kusoma sentensi zinazojumuisha vizuri na vibaya ili kuimarisha usomaji bora</p> <p>d) kuandika sentensi kwa kujumuisha vizuri na vibaya ili kuimarisha uandishi mwafaka</p> <p>e) kuchangamkia matumizi ya vizuri na vibaya katika kuimarisha mawasiliano.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aweza kujaza mapengo kwa kutumia vizuri na vibaya. • Mwanafunzi aweza kubainisha matumizi ya vielezi lengwa kwa kutumia vifaa vya teknolojia. • Mwanafunzi arejeele vitendo mbalimbali kwa kutumia vizuri na vibaya k.m Mtoto amesoma vizuri. • Mwanafunzi aandike sentensi zinazojumuisha vizuri na vibaya. 	1) Unatumia maneno yapi kuelezea vile mtu alivyofanya jambo?
Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:				
mawasiliano na ushirikiano – wanafunzi wanashiriki katika makundi ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza.				
Uhusiano na masuala mtambuko: Uraia – haki za watoto -wanafunzi wanahamasishwa kuhusu haki zake.			Uhusiano na Maadili: uwajibikaji, haki za kijamii, heshima.	

<p>Uhusiano na Masomo mengine: Environmental Activities</p>	<p>Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji: kuwahamasisha wengine katika jamii kuhusu haki za watoto.</p>
<p>Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:</p> <ul style="list-style-type: none"> • kazi ya vikundi • michezo • nyimbo na mashairi kuhusu usafi wa mwili. 	<p>Mapendekezo ya Tathmini:</p> <ul style="list-style-type: none"> • kuchunguza anavyotamka sauti zilizofunzwa • kuuliza maswali kuhusu haki za watoto • kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa • kuchunguza jinsi anavyotumia vizuri na vibaya katika sentensi.

Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • anatamka sauti lengwa vyema na kwa ukakamavu • anatambua haki za watoto na kuzitilia maanani katika mawasiliano • anatumia msamiati wa haki za watoto kwa ubunifu katika sentensi • anasoma kwa ufasaha • anatetea haki za watoto kwa ukakamavu • anajibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa ubunifu na usahihi • anatumia vivumishi vizuri na vibaya kutunga sentensi ifaavyo na kwa ubunifu wa hali ya juu. • anaandika kwa hati nadhifu. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • anatamka sauti lengwa vyema • anatambua haki za watoto • anatumia msamiati wa haki za watoto ifaavyo katika sentensi • anasoma ifaavyo • anatetea haki za watoto • anajibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi • anatumia vivumishi vizuri na vibaya kutunga sentensi ifaavyo • anaandika kwa hati bora. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto za kutamka baadhi ya sauti lengwa vyema • anatambua haki za watoto • ana changamoto za kutumia baadhi ya msamiati wa haki za watoto katika sentensi • anasoma baadhi ya kazi anazopewa • anajibu baadhi ya maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi • ana changamoto katika kutumia vivumishi vizuri na vibaya kutunga sentensi ifaavyo • anaandika kwa hati zinazosomeka. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto za kutamka sauti lengwa • ana changamoto katika kutambua haki za watoto • ana changamoto za kutumia msamiati wa haki za watoto katika sentensi • ana changamoto katika kusoma kazi anazopewa • ana changamoto katika kujibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi • ana changamoto za kutumia vivumishi vizuri na vibaya kutunga sentensi ifaavyo

- ana changamoto katika kusoma.

MADA	MADA NDOGO	MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA	MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI	MASWALI DADISI
Usafiri	Sauti za herufi mbili za Kiswahili (Vipindi 4)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua sauti za herufi mbili zilizofunzwa ili kuimarisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza</p> <p>b) kutamka sauti lengwa za herufi mbili katika kuimarisha stadi ya kuzungumza</p> <p>c) kusoma herufi za sauti mbili ili kuimarisha usomaji bora</p> <p>d) kusoma maneno kwa kutumia silabi zinazotokana na sauti lengwa ili kuimarisha usomaji bora</p> <p>e) kusoma hadithi fupi zilizo na maneno yaliyo na sauti lengwa ili kuimarisha usomaji bora</p> <p>f) kuandika maneno kutokana na herufi alizofunzwa ili kuimarisha stadi ya kuandika</p> <p>g) kufurahia kutumia sauti zilizofunzwa katika mawasiliano.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi atambue sauti /ch/ na /dh/ katika maneno. • Mwanafunzi asikilize sauti lengwa zikitamkwa na mwalimu kisha atamke pamoja na mwalimu na mwishowe atamke akiwa peke yake, wawili wawili na kama darasa. • Mwanafunzi aweza kutumia vifaa vya kiteknolojia kama vile papaya na DVD kusikiliza sauti zikitamkwa. • Mwanafunzi atambue herufi zinazowakilisha sauti lengwa kwa kutumia kadi za herufi. • Mwanafunzi aambatanishe silabi kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa. • Mwanafunzi atenganishe silabi katika kutambua sehemu mbalimbali za maneno. • Mwanafunzi aweza kumsikiliza mgeni mwalikwa akitamka sauti lengwa. • Mwanafunzi aandike herufi za sauti alizosoma hewani na vitabuni. • Mwanafunzi asome maneno kwa kutumia silabi na kuchanganua yaliyo marefu zaidi. • Mwanafunzi wasome hadithi zilizo na maneno yaliyobeba sauti lengwa wakiwa wawili wawili. • Mwanafunzi aweza kutumia vifaa vya kiteknolojia kama vile tarakilishi, projekta na kipasasauti na rununu kusikiliza na kusoma hadithi. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Ni sauti zipi unazojua kutamka? 2) Unajua kusoma silabi na maneno yapi? 3) Unajua kuandika silabi na maneno yapi?

			<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aweza kufinyanga maumbo ya herufi inayowakilisha sauti lengwa. • Mwanafunzi anakili herufi na maneno yanayotokana na sauti alizofunzwa. 	
	Msamiati (Vipindi 2)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua baadhi ya majina ya vyombo vya usafiri katika kuimarisha mawasiliano</p> <p>b) kusoma majina ya vyombo vya usafiri na msamiati mwingine wa usafiri katika sentensi ili kuimarisha usomaji bora</p> <p>c) kutumia msamiati wa usafiri kutungia sentensi katika kuimarisha stadi ya kuzungumza na kuandika</p> <p>d) kuandika majina ya vyombo vya usafiri na msamiati mwingine wa usafiri ili kuimarisha stadi ya kuandika</p> <p>e) kuthamini vyombo vya usafiri katika maisha ya kila siku.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi atunge sentensi sahihi akitumia msamiati wa vyombo vya usafiri k.v matatu, basi, lori, pikipiki, garimoshi, gari dogo, ndege na meli. • Mwanafunzi atoe maana ya msamiati unaohusu usafiri. • Mwanafunzi aweza kutazama michoro na picha zinazolenga usafiri. • Mwanafunzi achore baadhi ya vyombo vya usafiri na kuvitambua kwa majina • Mwanafunzi aweza kutazama video kuhusu shughuli za usafiri. • Wanafunzi wajadiliane kuhusu umuhimu wa vyombo vya usafiri. 	<p>1) Umewahi kutumia chombo kipi cha kusafiria?</p> <p>2) Unajua vyombo gani vingine vya usafiri?</p> <p>3) Je, ni maneno gani yanayotumiwa usafiri?</p>
	Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (Vipindi 2)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua kwa kutaja vyombo mbalimbali vya usafiri ili kuimarisha mawasiliano</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi atambue aina mbalimbali za vyombo vya usafiri k.v. matatu, basi, lori, pikipiki, garimoshi, gari dogo, ndege na meli kwa kutumia picha au vyombo vya kiteknolojia. • Mwanafunzi asimulie kuhusu vyombo vya usafiri, kwa mfano; Mimi nilisafiri kwa matatu. 	<p>1) Je, ni safari gani umewahi kufanya?</p> <p>2) Je, unasafiria chombo gani?</p>

		<p>b) kuzungumza kuhusu vyombo vya usafiri ili kuimarisha uwezo wa kujieleza</p> <p>c) kusikiliza visa kuhusu usafiri ili kuimarisha umakinifu</p> <p>d) kusikiliza kisa kuhusu usafiri ili kuimarisha ukakamavu katika kujieleza</p> <p>e) kufurahia masimulizi kuhusu vyombo vya usafiri ili kuimarisha mawasiliano.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi ashiriki katika mjadala darasani au katika vikundi kuhusu vyombo mbalimbali vya usafiri. • Mwanafunzi aweza kusikiliza masimulizi kuhusu vyombo vya usafiri kwa kutumia video au kinasa sauti. 	
	<p>Kusoma: Hadithi (Vipindi 3)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua picha za vyombo mbalimbali vya usafiri ili kuimarisha ufahamu wa hadithi</p> <p>b) kuelezea maana ya maneno yaliyotumiwa katika hadithi ili kuimarisha ufahamu wa hadithi</p> <p>c) kusikiliza hadithi inaposomwa na mwalimu ili kuimarisha umakinifu</p> <p>d) kusoma hadithi zinazohusu usafiri kujenga stadi ya kusoma</p> <p>e) kufahamu hadithi aliyoisoma kuhusu usafiri ili kupata ujumbe katika hadithi</p> <p>f) kuchangamkia kusoma hadithi katika maisha ya kila siku ili</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi. • Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi • Mwanafunzi afahamu matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi. • Mwanafunzi aweza kusikiliza mwalimu anaposoma hadithi kisha asome na mwalimu na baadaye asome peke yake, wakiwa wawili wawili au katika vikundi. • Mwanafunzi asimulie hadithi aliyoisoma au kusomewa kwa kutumia maneno yake mwenyewe. • Mwanafunzi aweza kurekodiwa akisoma vizuri kwa video au kinasa sauti ili wanafunzi waweze kutazama na kusikiliza jinsi ya kusoma hadithi kwa ufasaha. • Mwanafunzi aweza kufanya ziara ya kwenda kuona vyombo vya usafiri kwenye vituo vya usafiri. • Mwanafunzi ajibu maswali ya ufahamu akiwa peke yake, wawili wawili au katika vikundi. 	<p>1) Umewahi kusoma hadithi ipi?</p> <p>2) Ni hadithi ipi iliyokufurahisha zaidi?</p> <p>3) Unamkumbuka mhusika gani katika hadithi uliyosoma?</p>

		kujenga ari ya usomaji huru.		
	Sarufi: Matumizi ya herufi kubwa (Vipindi 2)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: a) kubainisha matumizi ya herufi kubwa ili kuimarisha mawasiliano andishi b) kusoma sentensi zilizo na matumizi ya herufi kubwa katika kuimarisha stadi za kusoma na kuandika c) kuandika sentensi akitumia herufi kubwa katika kuimarisha uandishi bora d) kuthamini matumizi ya herufi kubwa katika kufanikisha mawasiliano.	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aelezee matumizi ya herufi kubwa. • Wanafunzi waweza kushirikishwa kusoma sentensi zinazotumia herufi kubwa wakiwa wawili wawili. • Mwanafunzi aweza kutofautisha kati ya herufi ndogo na herufi kubwa. • Mwanafunzi aakifishe sentensi kwa kutumia herufi kubwa. • Wanafunzi waweza kuakifisha sentensi mbali mbali wakitumia herufi kubwa wakiwa wawili wawili au katika vikundi. 	1) Je, herufi kubwa hutumiwa wapi?
<p>Umilisi wa kimsingi unaokuzwa: mawasiliano na ushirikiano – wanafunzi wanashiriki katika vikundi ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza hamu ya kujifunza: mwanafunzi atapata hamu ya kutaka kutumia vipengee vilivyofunzwa vya sarufi kwenye mawasiliano ubunifu – mwanafunzi anatumia ubunifu katika kutunga sentensi na masimulizi.</p>				
<p>Uhusiano na masuala Mtambuko: elimu ya maendeleo endelevu- usalama katika usafiri –wanashughulikia vyombo vya usafiri.</p>		<p>Uhusiano na Maadili: uwajibikaji heshima.</p>		
<p>Uhusiano na Masomo Mengine: Environmental Activities; English Activities</p>		<p>Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji: kuwahamasisha wengine kuhusu usalama barabarani.</p>		
<p>Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:</p> <ul style="list-style-type: none"> • kazi ya vikundi • michezo 		<p>Mapendekezo ya Tathmini:</p> <ul style="list-style-type: none"> • kuchunguza anavyotamka sauti zilizofunzwa • kuuliza maswali kuhusu vyombo vya usafiri • kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa • kuchunguza jinsi anavyotumia herufi kubwa kuakifisha maneno na sentensi. 		

Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • anatamka sauti lengwa kwa ufasaha • anataja majina ya vyombo vya usafiri kwa wepesi • anatumia msamiati wa usafiri kwa ubunifu katika sentensi • anasoma kwa ufasaha. • anafahamu kwa urahisi hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma na kusomewa • anatumia herufi kubwa ipasavyo katika kuakifisha maneno na sentensi kwa wakati • anaandika kwa hati nadhifu na kwa haraka. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • anatamka sauti lengwa vyema • anataja majina ya vyombo vya usafiri • anatumia msamiati wa usafiri ifaavyo katika sentensi • anasoma ifaavyo • anafahamu hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma na kusomewa • anatumia herufi kubwa ipasavyo katika kuakifisha maneno na sentensi • anaandika kwa hati bora. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto za kutamka baadhi ya sauti lengwa vyema • anataja baadhi ya majina ya vyombo vya usafiri • ana changamoto za kutumia baadhi ya msamiati wa usafiri katika sentensi • anasoma baadhi ya kazi anazopewa • anafahamu baadhi ya hadithi alizosimuliwa, aliyosoma au kusomewa • ana changamoto za kutumia herufi kubwa katika kuakifisha maneno na sentensi • anaandika kwa hati zinazosomeka. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto za kutamka sauti lengwa • ana changamoto ya kutaja baadhi ya majina ya vyombo vya usafiri • ana changamoto za kutumia msamiati wa usafiri katika sentensi • ana changamoto katika kusoma • ana changamoto katika kufahamu hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma au kusomewa • ana changamoto za kutumia herufi kubwa katika kuakifisha maneno na sentensi • ana changamoto katika kuandika.

MADA	MADA NDOGO	MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA	MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI	MASWALI DADISI
Familia	Sauti za herufi mbili za Kiswahili (<i>Vipindi 6</i>)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua sauti za herufi mbili zilizofunzwa ili kuimarisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza</p> <p>b) kutamka sauti lengwa za herufi mbili katika kuimarisha stadi ya</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi atambue sauti /gh/, /ny/ na /ng'/ katika maneno. • Mwanafunzi asikilize mwalimu akitamka sauti lengwa /gh/, /ny/ na /ng'/ kisha atamke pamoja na mwalimu na mwishowe atamke akiwa peke yake, wawili wawili na kama darasa. • Mwanafunzi aweza kutumia teknolojia kama vile 	<p>1) Unaweza kutamka sauti zipi ulizofunzwa awali?</p> <p>2) Unaweza kutambua sauti gani za herufi</p>

		<p>kuzungumza</p> <p>c) kusoma herufi za sauti mbili ili kuimarisha usomaji bora</p> <p>d) kusoma maneno kwa kutumia silabi zinazotokana na sauti lengwa ili kuimarisha usomaji bora</p> <p>e) kusoma hadithi fupi zilizo na maneno yaliyo na sauti lengwa ili kuimarisha usomaji bora</p> <p>f) kuandika maneno kutokana na herufi alizofunzwa ili kuimarisha stadi ya kuandika</p> <p>g) kufurahia kutumia sauti zilizofunzwa katika mawasiliano.</p>	<p>papaya kusikiliza sauti lengwa ikitamkwa.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi atambue herufi zinazowakilisha sauti lengwa kwa kutumia kadi za herufi. • Mwanafunzi aambatanishe silabi kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa. • Mwanafunzi atenganishe silabi katika kutambua sehemu mbalimbali za maneno. • Mwanafunzi aweza kumsikiliza mgeni mwalikwa akitamka sauti lengwa. • Mwanafunzi aandike herufi za sauti alizosoma hewani na vitabuni. • Mwanafunzi asome maneno kwa kutumia silabi na kuchanganua yaliyo marefu zaidi. • Mwanafunzi wasome hadithi zilizo na maneno yaliyobeba sauti lengwa wakiwa wawili wawili. • Mwanafunzi aweza kutumia vifaa vya kiteknolojia kama vile tarakilishi, projekta na kipasa sauti kusikiliza na kusoma hadithi. • Mwanafunzi aweza kufinyanga maumbo ya herufi inayowakilisha sauti lengwa. • Mwanafunzi anakili herufi na maneno yanayotokana na sauti alizofunzwa. 	<p>mbili katika maneno?</p> <p>3) Unaweza kuunda maneno yapi kwa kutumia sauti za herufi mbili?</p>
<p>Kusikiliza na Kuzungumza: Maneno ya heshima na adabu. (Vipindi 2)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua maneno ya heshima na adabu ili kuimarisha stadi ya kuzungumza</p> <p>b) kutumia maneno ya heshima na adabu katika mawasiliano</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aelezee matumizi ya maneno ya heshima na adabu k.v. hodi, karibu, naomba, nisamehe na nashukuru. • Mwanafunzi waigize vitendo vya heshima na adabu wakiwa wawili wawili au katika vikundi. • Mwanafunzi atazame michoro na picha ya watu wakidhihirisha vitendo vya heshima na adabu. 	<p>1) Unapotaka kuingia ndani ya nyumba ya jirani unafanyaje?</p> <p>2) Mgeni anapobisha mlango unaitikia vipi?</p>	

		<p>c) kuonyesha vitendo vya heshima na adabu anapowasiliana katika mazingira yake</p> <p>d) kuthamini matumizi ya maneno ya heshima na adabu katika mazingira yake.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Wanafunzi wajiadili maneno ya heshima na adabu katika vikundi. • Mwanafunzi aweza kutazama video inayowasilisha vitendo vya heshima na adabu. • Mwanafunzi asome maneno ya heshima na adabu. • Mwanafunzi aelezee maneno ya heshima na adabu. 	<p>3) Mtu akikutendea wema unamwambiaje?</p> <p>4) Ukifanya kosa utasemaje?</p>
	Msamiati (Vipindi 3)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutumia msamiati wa familia katika mawasiliano ya kila siku</p> <p>b) kutunga sentensi akitumia msamiati wa familia uliofunzwa ili kuimarisha stadi ya mazungumzo na uandishi</p> <p>c) kusoma maneno na sentensi kuhusu familia ili kuimarisha stadi ya kusoma</p> <p>d) kuandika maneno na sentensi kuhusu familia ili kuimarisha stadi ya kuandika</p> <p>e) kufurahia kuwarejelea watu wa familia kwa majina yao mwafaka ili kuimarisha mawasiliano.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi ataje majina ya watu wa familia k.v babu, nyanya, mjomba, ami/amu, shangazi, binamu na halati. • Mwanafunzi atazame picha au michoro ya watu wa familia. • Wanafunzi wasome majina ya watu wa familia kwenye kadi au chati. • Wanafunzi waweza kushiriki katika nyimbo na mashairi kuhusu watu wa familia. • Mwanafunzi aandike majina ya familia. • Mwanafunzi asome msamiati wa watu wa familia katika kadi au chati. • Mwanafunzi atunge na kusoma sentensi akitumia msamiati wa familia. 	<p>1) Wazazi wa baba/mama wanaitwaje?</p> <p>2) Dada yake mama anaitwaje?</p> <p>3) Dada yake baba anaitwaje?</p> <p>4) Kaka yake baba anaitwaje?</p> <p>5) Wtoto wa amu/ami na shangazi anaitwaje?</p>
	Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (Vipindi 2)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutaja majina ya watu wa familia katika kujenga umilisi wa kuzungumza</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi arejeele watu wa karibu katika familia aliofunzwa awali. • Mwanafunzi asimulie kuhusu familia. • Mwanafunzi azungumzie kuhusu familia. • Mwanafunzi aelezee maana ya majina ya watu wa familia. 	<p>1) Je, familia yenu ina watu wangapi?</p> <p>2) Je, unajua majina gani ya watu wa familia yako?</p>

		<p>b) kusikiliza kwa makini masimulizi kuhusu watu wa familia ili kujenga umakinifu</p> <p>c) kuelezea kuhusu watu wa familia katika kuimarisha uwezo wa kuwaelezea watu katika mazingira yake</p> <p>d) kuthamini umuhimu wa familia katika kuendeleza mshikamano wa kijamii.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aweza kushirikishwa katika nyimbo au mashairi kuhusu watu wa familia. • Mwanafunzi aweza kutazama video picha au michoro inayoonyesha watu wa familia ili wjadiliane katika vikundi. 	
	<p>Kusoma: Hadithi (Vipindi 3)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua picha za watu wa familia ili kuimarisha ufahamu wa hadithi</p> <p>b) kusikiliza hadithi za mwalimu kuhusu watu wa familia ili kuimarisha umakinifu</p> <p>c) kusoma hadithi kuhusu watu wa familia ili kuimarisha usomaji bora</p> <p>d) kufahamu hadithi aliyosoma na aliyosomewa ili kupata ujumbe</p> <p>e) kuchangamkia kusoma hadithi kuhusu watu wa familia katika kujenga ari ya usomaji bora.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi. • Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi. • Mwanafunzi afahamu matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi. • Mwanafunzi asikilize mwalimu anaposoma hadithi kisha asome na mwalimu na baadaye asome peke yake, wawili wawili au katika vikundi. • Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi ikisomwa kwa kutumia tarakilishi na projekta. • Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kutoka kwa jitabu mbele ya darasa. • Mwanafunzi athibitisha utabiri wake baada ya kusoma hadithi. • Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali kutokana na hadithi. • Mwanafunzi atoe muhtasari wa hadithi aliyosoma au kusomewa. 	<p>1) Unaweza kutambua watu gani katika picha?</p> <p>2) Hadithi inahusu watu gani?</p>

	Sarufi: Matumizi ya maneno yanayoashiria vitendo (Vipindi 2)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze; a) kutambua maneno yanayoashiria vitendo ili kuimarisha mawasiliano b) kusoma maneno yanayoashiria vitendo ili kujenga usomaji bora c) kutumia maneno yanayoashiria vitendo katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano d) kuandika sentensi sahihi akitumia maneno yanayoashiria vitendo katika kuimarisha uandishi bora e) kufurahia kutumia maneno yanayoashiria vitendo katika mawasiliano.	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aweza kuigiza vitendo k.m. simama, tembea, andika, cheka n.k. • Mwanafunzi atunge sentensi zenye matumizi ya maneno yanayoashiria vitendo kwa mfano simama, oga, chana n.k. • Mwanafunzi asome sentensi zinazohusisha vitendo. • Mwanafunzi aweza kujaza mapengo kwa maneno yanayoashiria vitendo. • Mwanafunzi anakili sentensi kwa kutumia maneno yanayoashiria vitendo. • Wanafunzi watunge sentensi katika makundi. • Mwanafunzi aandike sentensi zinazohusisha vitendo. • Mwanafunzi aweza kupewa zoezi la kujaza mapengo kwa tarakilishi (mchezo wa kuburura na kutia kapuni). 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Je, unajua kutumia maneno yapi yanayowakilisha vitendo? 2) Je, unajua kutumia maneno yapi yanayowakilisha vitendo katika sentensi?
Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:				
mawasiliano na ushirikiano – kujadiliana kuhusu majukumu ya watu wa familia; kufanya kazi kwa makundi ujuzi wa kidijitali : kuna mapendekezo ya kutumia vifaa vya teknolojia kufunzia ubunifu: utunzi wa sentensi kwa kutumia huyu na nani .				
Uhusiano na masuala mtambuko: Uraia: uzalendo: kushirikiana katika vikundi; utangamano wa kijamii - mahusiano katika familia.			Mahusiano na Maadili: mapenzi katika familia heshima.	
Uhusiano na masomo mengine: Religious Studies, English Activities na Environmental Activities			Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji: kuwarejelea watu wa familia kwa majina yao mwafaka nyumbani kuwahamasisha wengine kuhusu umuhimu wa familia kuwatembelea mayatima.	

<p>Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji: kazi ya vikundi shughuli za vikundi vya ushirika shuleni michezo.</p>	<p>Mapendekezo ya Tathmini:</p> <ul style="list-style-type: none"> • kusikiliza jinsi anavyotamka sauti lengwa • kuchunguza jinsi anavyowatambua watu katika familia yake. • kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa • kumpa zoezi ili mwanafunzi atambue vitendo katika sentensi.
---	---

Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • anawaelezea watu wa familia. • anatumia majina ya watu wa familia kwa ubunifu katika sentensi • anatumia maneno ya heshima kwa ubunifu katika mazungumzo • anasoma kwa ufasaha • anafahamu kwa urahisi hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma na kusomewa • anatambua vitendo katika sentensi • anaandika kwa hati nadhifu na kwa haraka. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • anawataja watu wa familia • anatumia majina ya watu wa familia katika sentensi ifaavyo • anatumia maneno ya heshima ifaavyo katika mazungumzo. • anasoma ifaavyo • anafahamu hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma na kusomewa • anatambua vitendo katika sentensi • anaandika kwa hati bora. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • anawataja watu wa familia • ana changamoto katika kutumia baadhi ya majina ya watu wa familia katika sentensi • anasoma baadhi ya kazi anazopewa • anafahamu baadhi ya hadithi alizosimuliwa, aliyosoma au kusomewa • anatambua vitendo katika sentensi • anaandika kwa hati zinazosomeka. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • anawataja watu wa familia • ana changamoto katika kutumia majina ya watu wa familia katika sentensi • ana changamoto ya kusoma. • ana changamoto katika kufahamu hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma na kusomewa • ana changamoto nyingi katika kutambua vitendo katika sentensi • ana changamoto katika kuandika.

MADA	MADA NDOGO	MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA	MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI	MASWALI DADISI
Usalama Wangu	Sauti na herufi mbili za Kiswahili (Vipindi 4)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <ol style="list-style-type: none"> kutambua sauti za herufi mbili katika kuimarisha matamshi bora kutamka sauti za Kiswahili za herufi mbili katika kuimarisha matamshi bora kusoma silabi za sauti zinazoundwa kutokana na sauti mbili ili kuimarisha usomaji kuunda silabi na maneno kwa kutumia sauti lengwa katika kuimarisha umilisi wa kusoma maneno kusoma maneno kwa kutumia silabi zinazotokana na sauti lengwa ili kuimarisha stadi ya kusoma kusoma hadithi fupi zilizo na maneno yaliyo na sauti lengwa ili kuimarisha stadi ya kusoma kuandika maneno kutokana na herufi za sauti lengwa katika kuimarisha uandishi kufurahia kutumia sauti zilizofunzwa katika mawasiliano. 	<ul style="list-style-type: none"> Mwanafunzi atambue sauti /sh/na /th/ katika maneno Mwanafunzi asikilize sauti lengwa ikitamkwa na mwalimu kisha atamke pamoja na mwalimu na mwishowe atamke akiwa peke yake, wawili na kama darasa nzima. Mwanafunzi aweza kutumia vifaa vya kiteknolojia kama vile papaya, tarakilishi na projekta kusikiliza sauti lengwa ikitamkwa. Mwanafunzi atambue herufi zinazowakilisha sauti lengwa kwa kutumia kadi za herufi. Mwanafunzi aambatanishe silabi kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa. Mwanafunzi atenganishe silabi katika kutambua sehemu mbalimbali za maneno. Mwanafunzi aweza kumsikiliza mgeni mwalikwa mwenye umahiri katika kutamka sauti lengwa. Mwanafunzi asome maneno kwa kuyagawa maneno marefu katika sehemu ndogo ndogo. Mwanafunzi wasome hadithi zilizo na maneno yaliyobeba sauti lengwa wakiwa wawili wawili. Mwanafunzi aweza kufinyanga maumbo ya herufi inayowakilisha sauti lengwa. Mwanafunzi anakili herufi na maneno yanayotokana na sauti alizofunzwa. Mwanafunzi aandike herufi za sauti alizosoma hewani na vitabuni. 	<ol style="list-style-type: none"> Je, sauti /sh/ na /th/ hutamkwa vipi? Je, ni maneno kama gani ambayo yana sauti /sh/na /th/?

	Msamiati (<i>Vipindi 3</i>)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze; a) kutambua msamiati ambao hutumiwa katika usalama ili kuwasiliana kuhusu masuala yanayohusu usalama wake b) kueleza maana ya msamiati wa usalama katika kuimarisha mawasiliano c) kutumia msamiati wa usalama katika sentensi sahihi katika kuimarisha mawasiliano d) kuthamini usalama wake katika maisha ya kila siku.	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi atoe maana ya msamiati wa usalama. • Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati wa usalama kama vile, kivukio cha barabara, moto, vidaraja, ajali michezoni, kuzama majini na vita. • Wanafunzi waweza kuchora baadhi ya vifaa vinavyohusiana na usalama wao kama vile kivukio cha barabarani vidaraja. • Wanafunzi waweza kutazama video, michoro au picha zinazolenga usalama wao. • Wanafunzi wajadiliane kuhusu umuhimu wa usalama wao kwenye makundi. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Unaweza kutaja mambo gani yanayohusu usalama? 2) Ni ajali gani ambayo umewahi kushuhudia au kuelezewa? 3) Unawezaje kuepuka ajali?
	Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (<i>Vipindi 2</i>)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: a) kutambua jinsi ya kuepukana na baadhi za ajali katika mazingira yao b) kujiepusha na vitendo vinavyoweza kumdhuru maishani c) kusimulia kuhusu mambo yanayoweza kuhatarisha usalama wake ili kuimarisha stadi ya kuzungumza d) kusikiliza masimulizi kuhusu usalama wa watoto katika kujenga umakinifu e) kuthamini umuhimu wa usalama wake katika maisha ya kila siku.	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi asimulie baadhi ya mambo yanayoweza kuhatarisha usalama wake kupitia kwa mgeni mwalikwa. • Mwanafunzi aweza kutazama video, picha au michoro inayoashiria usalama wa watoto. • Wanafunzi wajadiliane kuhusu usalama wao katika vikundi. • Wanafunzi waigize namna ya kuepuka ajali mbalimbali kama vile moto, kuvunjika viungo, kugongwa barabarani na kupigana. • Mwanafunzi aandike baadhi ya mambo muhimu kuhusu usalama wake. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Ni nini maana ya ajali? 2) Je, ajali mbalimbali husababishwa na nini? 3) Ni ajali gani umewahi kushuhudia katika shughuli za kila siku? 4) Unawezaje kuepuka ajali?
	Kusoma: Hadithi (<i>Vipindi 3</i>)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: a) kutambua picha zinazohusu usalama ili	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi. • Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Je, umesoma hadithi ngapi? 2) Ni hadithi ipi

		<p>kuimarisha ufahamu wa hadithi</p> <p>b) kusoma hadithi kuhusu usalama ili kujenga stadi ya kusoma</p> <p>c) kusikiliza hadithi inayosomwa na mwalimu kuhusu usalama ili kujenga usikivu wake</p> <p>d) kufahamu hadithi aliyoisoma au kusomewa kuhusu usalama wake ili kupata ujumbe wa hadithi</p> <p>e) kuchangamkia kusoma hadithi kila siku.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi adhihirishe ufahamu wa matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi. • Mwanafunzi asikilize mwalimu anaposoma hadithi kisha asome na mwalimu na baadaye asome peke yake, wawili wawili au katika vikundi. • Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi ikisomwa kwa kutumia tarakilishi na projekta. • Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kutoka kwa jitabu mbele ya darasa. • Mwanafunzi athibitishie utabiri wake baada ya kusoma hadithi. • Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali kutokana na hadithi. • Mwanafunzi atoe muhtasari wa hadithi aliyosoma au kusomewa. 	<p>iliyokufurahisha zaidi?</p> <p>3) Unakumbuka nani katika hadithi iliyowahi kukufurahisha?</p>
	<p>Sarufi: Matumizi ya Huyo na Hao (Vipindi 2)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kufahamu matumizi ya huyo na hao katika mawasiliano</p> <p>b) kutumia huyo na hao katika sentensi kwa usahihi ili kuimarisha mawasiliano</p> <p>c) kusoma sentensi zinazojumuisha huyo na hao ili kujenga stadi ua kusoma</p> <p>d) kuandika sentensi zinazojumuisha huyo na hao katika kuimarisha uandishi</p> <p>e) kuchangamkia matumizi ya huyo na hao katika maawasiliano.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi asome sentensi zenye kudhihirisha matumizi ya huyo na hao kama vile: Huyo ni nani? • Mwanafunzi aandike sentensi zinadhihirisha matumizi ya huyo na hao kama vile: huyo ni nani?- huyo ni kaka. • Mwanafunzi aweza kujaza mapengo kwa kutumia huyo na hao. • Mwanafunzi aigize vitendo vya kuwaashiria watu mbalimbali kwa kutumia huyo na hao. • Mwanafunzi aweza kukamilisha mafungu yanayohusu matumizi ya huyo na nani wakiwa wawili wawili k.m. Mtoto ____ (huyo) Watoto ____ (hao). 	<p>1) Unatumia neno gani kuonyesha mwenzako akiwa mbali kidogo?</p> <p>2) Unatumia neno gani kuuliza swali kuhusu mwenzako?</p>

Umilisi wa kimsingi unaokuzwa: mawasiliano na ushirikiano – wanafunzi wanashiriki katika vikundi. ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza			
Uhusiano na masuala mtambuko na maadili: elimu ya maendeleo endelevu – somo la usalama: kueleza jinsi ya kujiepusha na vitendo vinavyoweza kumdhuru maishani.		Uhusiano na Maadili: uwajibikaji; mapenzi; uaminifu.	
Uhusiano na masomo mengine: Environmental Activities		Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji: kuwahamasisha wengine kuhusu usalama kufunza wengine katika jamii kuhusu ishara za barabarani.	
Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji: Kazi ya vikundi Shughuli za vikundi vya ushirika shuleni Michezo		Mapendekezo ya Tathmini: <ul style="list-style-type: none"> • kusikiliza jinsi anavyotamka sauti lengwa • kumwuliza maswali kuhusu usalama • kuchunguza anapotumia msamiati wa usalama katika sentensi • kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa • kumpa zoezi ili atumie huyo na hao katika sentensi. 	

Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
Mwanafunzi, <ul style="list-style-type: none"> • anatamka sauti lengwa kwa ufasaha • anaelezea njia mbalimbali za kudumisha usalama wake • anatumia msamiati wa usalama kwa ubunifu katika sentensi ifaavyo 	Mwanafunzi, <ul style="list-style-type: none"> • anatamka sauti lengwa ipasavyo • anataja njia mbalimbali za kudumisha usalama wake • anatumia msamiati wa usalama katika sentensi ifaavyo 	Mwanafunzi, <ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto katika kutamka baadhi ya sauti lengwa • anataja njia kadhaa za kudumisha usalama wake • ana changamoto za kutumia baadhi ya msamiati wa usalama katika sentensi • anasoma baadhi ya herufi, silabi na 	Mwanafunzi, <ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto katika kutamka sauti lengwa • ana changamoto katika kutaja njia za kudumisha usalama wake • ana changamoto za kutumia msamiati wa usalama katika sentensi

<ul style="list-style-type: none"> • anasoma kwa ufasaha • anafahamu kwa urahisi hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma na kusomewa • anatumia huyo na hao katika sentensi kwa usahihi kila wakati • anaandika kwa hati nadhifu na kwa haraka. 	<ul style="list-style-type: none"> • anasoma ifaavyo • anafahamu hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma na kusomewa • anatumia huyo na hao katika sentensi kwa usahihi • anaandika kwa hati bora. 	<p>maneno</p> <ul style="list-style-type: none"> • anafahamu baadhi ya hadithi alizosimuliwa, aliyosoma au kusomewa • ana changamoto katika kutumia huyo na hao katika sentensi kwa usahihi • anaandika kwa hati zinazosomeka. 	<ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto katika kusoma • ana changamoto katika kufahamu hadithi aliyosimuliwa, aliyosomoma na kusomewa • ana changamoto katika kutumia huyo na hao katika sentensi kwa usahihi • ana changamoto katika kuandika.
--	---	---	---

MADA	MADA NDOGO	MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA	MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI	MASWALI DADISI
Hali ya Anga	Alfabeti ya Kiswahili (<i>Vipindi 2</i>)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua alfabeti ya Kiswahili ili kuimarisha usomaji</p> <p>b) kusoma alfabeti ya Kiswahili kwa mfuatano ufao katika kuimarisha matumizi ya kamusi baadaye</p> <p>c) kubainisha irabu za Kiswahili ili kuelewa jinsi silabi huundwa</p> <p>d) kubainisha konsonanti za Kiswahili ili kuelewa jinsi silabi huundwa</p> <p>e) kuandika alfabeti ya Kiswahili katika kuimarisha uandishi bora</p> <p>f) kuthamini alfabeti katika</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi asome alfabeti ya Kiswahili kwa mfuatano: a, b, ch, d, dh, e, f, g, gh, h, i, j, k, l, m, n, ng', ny, o, p, r, s, sh, t, th, u, v, w, y, z. • Mwanafunzi aweza kusoma alfabeti kwenye chati. • Mwanafunzi aweza kuimba wimbo wa alfabeti. • Mwanafunzi aweza kusikiliza alfabeti ya Kiswahili ikikaririwa kwenye vifaa vya kiteknolojia kama vile kinasasauti. • Mwanafunzi ashiriki katika kikundi ili kutenganisha konsonanti na irabu akitumia kadi za herufi. • Mwanafunzi aandike alfabeti ya Kiswahili. • Wanafunzi washiriki katika mjadala kuhusu umuhimu wa alfabeti katika lugha. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Je, lugha ya Kiswahili ina herufi ngapi? 2) Je, ni herufi gani unazoweza kusoma? 3) Alfabeti ni nini? 4) Lugha ya Kiswahili ina konsonanti ngapi? 5) Lugha ya Kiswahili ina irabu ngapi? 6) Je, irabu na konsonanti hutofautianaje katika alfabeti? 7) Alfabeti ina umuhimu upi katika lugha?

		lugha.		
	Msamiati (Vipindi 2)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua msamiati ambao hutumiwa katika hali ya anga ili kuelezea hali ya anga ifaavyo</p> <p>b) kutambua hali ya anga ya siku husika ili kuimarisha mawasiliano</p> <p>c) kueleza maana ya msamiati unaohusu hali ya anga katika kuimarisha stadi ya kuzungumza na kuandika</p> <p>d) kutumia msamiati unaohusu hali ya anga katika sentensi sahihi ili kuimarisha stadi ya kuzungumza na kuandika</p> <p>e) kuthamini hali mbalimbali za anga ili kuelewa misimu.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi atoe maana ya msamiati unaohusu hali ya anga. • Mwanafunzi atunge sentensi sahihi akitumia msamiati unaohusu hali ya anga kama vile upepo, jua, mvua na mawingu. • Mwanafunzi aweza kutazama video inayoonyesha hali mbalimbali za anga. • Mwanafunzi atazame michoro na picha zinazolenga hali mbambali za anga. • Mwanafunzi achore baadhi ya michoro inayoashiria hali mbalimbali za hali ya anga kama vile mvua, mawingu na jua. • Mwanafunzi ashiriki katika mjadala kuhusu umuhimu wa hali mbalimbali za anga. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Je, ni vipi unavyoweza kuelezea upepo? 2) Ni hali ya anga ipi inayokufurahisha zaidi? 3) Mvua hutusaidia vipi?
	Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (Vipindi 2)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua msamiati unaotumika kuonyesha hali ya anga ili kuimarisha mawasiliano</p> <p>b) kubainisha hali mbalimbali za anga ili kuimarisha</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi asimulie visa kuhusu hali mbalimbali za anga. • Mwanafunzi aweza kutazama video inayohusu hali ya anga. • Mwanafunzi waweza kupewa nafasi kwenda nje ya darasa na kujadiliana kuhusu hali ya anga wakati huo. • Mwanafunzi ashiriki katika majadiliano kuhusu hali 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Anga ni nini? 2) Je, ni vitu vipi hupatikana angani? 3) Dalili ya mvua ni nini? 4) Mvua hutusaidiaje? 5) Unaona nini katika chati ya hali ya anga?

		<p>mawasiliano</p> <p>c) kusimulia kuhusu hali mbalimbali za anga ili kuimarisha stadi ya kuzungumza</p> <p>d) kusikiliza masimulizi kuhusu hali ya anga ili kujenga umakinifu</p> <p>e) kuthamini umuhimu wa hali ya anga katika maisha ya kila siku.</p>	<p>za anga tofauti kama vile upepo, jua, mvua na mawingu katika makundi.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aelezee hali mbalimbali za anga kwa kutumia michoro au picha . 	
	<p>Kusoma: Hadithi (Vipindi 3)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua picha za kuonyesha hali ya anga ili kuimarisha ufahamu</p> <p>b) kutambua maneno yanayohusiana na hali ya anga ili kuimarisha usomaji</p> <p>c) kusoma hadithi zinazohusu hali ya anga ili kuimarisha usomaji</p> <p>d) kusikiliza hadithi za mwalimu kuhusu hali ya anga ili kujenga stadi ya kusoma na kusikiliza</p> <p>e) kufahamu hadithi aliyoisoma kuhusu hali ya anga ili kupata ujumbe</p> <p>f) kuchangamkia kusoma hadithi katika maisha ya kila siku.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi. • Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi. • Mwanafunzi afahamu matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi. • Mwanafunzi asikilize mwalimu anaposoma hadithi kisha asome na mwalimu na baadaye asome peke yake, wawili wawili au katika vikundi. • Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi ikisomwa kwa kutumia tarakilishi na projekta. • Mwanafunzi asome hadithi kutoka kwa jitabu mbele ya darasa. • Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kutoka kwa kitabu cha hadithi. • Mwanafunzi athibitisha utabiri wake baada ya kusoma hadithi. • Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali kutokana na 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Je, ni hadithi zipi ambazo umewahi kusoma? 2) Kati ya hadithi hizo, ni ipi iliyokufurahisha zaidi? 3) Unakumbuka nani katika hadithi hiyo?

			hadithi. <ul style="list-style-type: none"> Mwanafunzi atoe muhtasari wa hadithi aliyosoma au kusomewa. 	
		<p>c) kufahamu hadithi aliyoisoma na aliyosomewa kuhusu miezi ya mwaka ili kupata ujumbe</p> <p>d) kuchangamkia kusoma hadithi katika maisha ya kila siku.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali kuhusu hadithi aliyosoma. • Mwanafunzi atoe muhtasari wa hadithi aliyosoma au kusomewa. 	
	Kuandika (Vipindi 3)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kuandika kisa kifupi kwa hati nadhifu kulingana na mada ili kujenga stadi ya uandishi</p> <p>b) kufurahia uandishi wa visa tofauti ili kuimarisha mawasiliano andishi.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi apewe hadithi yenye mapengo ajaze kwa maneno mwafaka • Mwanafunzi aeleze yaliyo muhimu katika uandishi k.v. mwandiko nadhifu, maudhui, mtiririko n.k. • Mwanafunzi asome kielelezo cha kisa kilichoandikwa. • Wanafunzi waweza kuandika kisa kifupi wakiwa wawili wawili • Mwanafunzi aandike kisa kifupi kinachohusiana na mada. Kisa hiki kifuata hatua tano za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, marejeleo, uhariri na uchapishaji. 	<p>1) Je, ni mambo yapi yanayofaa kuzingatiwa unapoandika kisa?</p> <p>2) Je, unaweza kuandika kisa kipi kuhusu jambo ulilofanya katika mwezi fulani wa mwaka?</p>
	Msamiati: Tarakimu 51-100 (Vipindi 3)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze;</p> <p>a) kutambua nambari 51-100 kwa maneno ili kuimarisha stadi ya kuzungumza</p> <p>b) kusoma nambari 51-100 kwa maneno ili kuimarisha usomaji bora</p> <p>c) kuandika nambari 51- 100 kwa maneno ili kuimarisha uandishi bora</p> <p>d) kuchangamkia kutumia nambari 51 – 100 kwa maneno katika mazungumzo yake.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi asome majina ya nambari 51-100 • Wanafunzi waweza kupatiwa kadi za nambari 51-100 na majina yake ili kuziambatanisha katika makundi. • Mwanafunzi aandike nambari 51-100. • Wanafunzi waweza kushirikishwa kupanga upya majina yaliparaganywa ya nambari 51-100. • Mwanafunzi atunge sentensi akitumia nambari 51-100. • Mwanafunzi aweza kuonyeshwa vibonzo vikihesabu hadi 100 kwenye tarakilishi. 	<p>1) Unaweza kuandika nambari zipi?</p> <p>2) Unaweza kutumia nambari gani kati ya 51-100 katika sentensi?</p>

	<p>Sarufi: Matumizi ya Kikomo (<i>Vipindi 2</i>)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze;</p> <p>a) kutambua matumizi ya kikomo (.) katika kuimarisha mawasiliano</p> <p>b) kuakifisha sentensi kwa kutumia kikomo(.) katika kuimarisha uandishi bora</p> <p>c) kuzingatia kikomo (.) anaposoma kifungu na sentensi ili kuimarisha usomaji bora</p> <p>d) kuthamini matumizi ya kikomo (.) katika mawasiliano.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi asome sentensi zenye kikomo (.) katika vikundi • Mwanafunzi aakifishe sentensi fupi kwa kutumia kikomo (.) • Mwanafunzi aandike sentensi ukitumia kikomo (.) 	<p>1) Unajua alama zipi za kuakifisha?</p> <p>2) Je, kikomo (.) huwekwa wapi katika sentensi?</p>
<p>Umilisi wa kimsingi unaokuzwa: mawasiliano na ushirikiano – kushirikiana pamoja darasani ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza.</p>				
<p>Uhusiano na masuala mtambuko: elimu ya kudumisha maendeleo: elimu ya maswala ya fedha: kujua kuratibu shughuli za kila siku.</p>		<p>Uhusiano na Maadili: uwajibikaji uzalendo (katika kukumbuka miezi na siku za sherehe za kitaifa).</p>		
<p>Uhusiano na masomo mengine: Mathematics Activities, Environmental Activities na English Activities</p>		<p>Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji: kushiriki katika kuratibu shughuli zinazoendeshwa katika jamii.</p>		
<p>Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji: kuzingatia ratiba ya shule inayoonyesha shughuli za miezi mbalimbali.</p>		<p>Mapendekezo ya Tathmini:</p> <ul style="list-style-type: none"> • kuhakiki matamshi ya sauti mbili zinazotamkwa pamoja • kuchunguza anavyotumia msamiati wa miezi ya mwaka na tarakimu katika mawasiliano • kuchunguza anavyotumia alama ya kikomo katika mawasiliano • kuchanganua anavyojibu maswali ya kusema na ya kuandika • kufuatilia mwandiko wake • kuchunguza anavyotumia lugha katika masimulizi. 		

Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
<p>Mwanafunzi;</p> <ul style="list-style-type: none"> • anatamka sauti kwa haraka na ipasavyo • anasimulia hadithi zinazojumuisha miezi ya mwaka kwa ubunifu • anasoma hadithi kwa ufasaha na ukakamavu • anafahamu kwa wepesi hadithi aliyosoma na kusomewa • anaandika sentensi akitumia kikomo kila siku • anaandika kisa kwa ubunifu, mtiririko na hati nadhifu na kwa haraka. 	<p>Mwanafunzi;</p> <ul style="list-style-type: none"> • anatamka sauti ipasavyo • anasimulia hadithi zinazojumuisha miezi ya mwaka kwa ubunifu • anasoma hadithi kwa ufasaha • anafahamu hadithi aliyosoma na kusomewa • anaandika sentensi akitumia kikomo • anaandika kisa kwa mtiririko na hati bora. 	<p>Mwanafunzi;</p> <ul style="list-style-type: none"> • anatamka baadhi ya sauti ipasavyo • anasimulia baadhi ya hadithi zinazojumuisha miezi ya mwaka • anasoma hadithi • anafahamu baadhi ya hadithi aliyosoma na kusomewa • anaandika baadhi ya sentensi akitumia kikomo • anaandika kisa kwa hati zinazosomeka. 	<p>Mwanafunzi;</p> <ul style="list-style-type: none"> • anatamka baadhi ya sauti • ana changamoto katika kusimulia hadithi zinazojumuisha miezi ya mwaka • anasoma baadhi ya hadithi japo bila ufasaha ufaao • ana changamoto katika kufahamu hadithi aliyosoma na kusomewa • ana changamoto katika kuandika sentensi akitumia kikomo • ana changamoto katika kuandika kisa.

MADA	MADA NDOGO	MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA	MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI	MASWALI DADISI
Kazi mbalimbali	Sauti mbili tofauti zinazotamkwa pamoja (<i>Vipindi 2</i>)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: a) kutambua sauti mbili zinazotamkwa pamoja ili kuimarisha matamshi bora b) kutamka sauti lengwa ili kuimarisha matamshi bora c) kusoma silabi za sauti lengwa ili	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi atambue sauti py na vy katika maneno • Mwanafunzi amsikilize mwalimu akitamka silabi zinazotokana na sauti lengwa kisha atamke pamoja na mwalimu na baadaye atamke akiwa pekee, wawili na darasa zima k.m pya, pye, vya na vye. • Mwanafunzi aweze kutumia teknolojia kama vile papaya, tarakilishi, projekta na kipazasauti ili kuimarisha 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Je, ni sauti zipi unazojua kutamka? 2) Je, ni sauti zipi zinazokutatiza kutamka? 3) Je, ni sauti zipi

		<p>kuimarisha usomaji</p> <p>d) kusoma maneno kwa kutumia silabi zinazotokana na sauti lengwa ili kuimarisha usomaji</p> <p>e) kusoma kwa sauti hadithi zilizo na maneno yaliyo na sauti lengwa ili kuimarisha matamshi na usomaji</p> <p>f) kuandika silabi zinazotokana na sauti lengwa ili kuimarisha uandishi bora</p> <p>g) kuandika maneno kutokana na silabi zilizofunzwa ili kuimarisha uandishi bora</p> <p>h) kuchangamkia kutamka sauti lengwa ili kuimarisha mawasiliano.</p>	<p>matamshi yake.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aweza kumsikiliza mgeni mwalikwa akitamka sauti lengwa. • Mwanafunzi atambue sauti alizosoma katika maneno kwa mfano k. m mpya, kipya, kompyuta, vyema, vyoo na vyote. • Mwanafunzi aandike maneno yanayojumuisha sauti lengwa. • Mwanafunzi asome maneno kwa kutumia silabi na kuyagawa yaliyo marefu zaidi katika sehemu ndogo ndogo. • Wanafunzi waweza kusoma hadithi zilizo na maneno yaliyobeba sauti lengwa darasani au wawili wawili. • Mwanafunzi asikilize imla ya maneno yaliyo na herufi za sauti lengwa na kuyaandika. 	<p>unazotamka bila shida?</p>
	<p>Msamiati (<i>Vipindi 3</i>)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua msamiati wa kazi mbalimbali ili kuimarisha mawasiliano</p> <p>b) kutunga sentensi akitumia msamiati wa kazi mbalimbali ili kujenga ubunifu</p> <p>c) kusoma maneno na sentensi kuhusu kazi mbalimbali ili kuimarisha usomaji</p> <p>d) kuandika maneno na sentensi kuhusu kazi mbalimbali ili kuimarisha uandishi</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi atazame picha, michoro au DVD inayoonyesha watu na kazi mbalimbali k.v ualimu, ukulima, udaktari, uyaya, unesi na ubawabu ili azitambue peke yake au katika vikundi. • Wanafunzi waweza kuambatanisha kadi za maneno na kazi mbalimbali wakiwa katika vikundi. • Mwanafunzi aeleze kazi mbalimbali. • Mwanafunzi aandike majina ya kazi mbalimbali. • Mwanafunzi asome msamiati wa kazi mbalimbali katika kadi, chati nk. • Mwanafunzi aandike sentensi kuhusu kazi mbalimbali • Mwanafunzi atunge na kusoma sentensi akitumia msamiati wa kazi mbalimbali. 	<p>1) Ni neno gani unaloweza kusoma kwenye kadi?</p> <p>2) Ni kazi ipi unayoipenda?</p> <p>3) Kwa nini watu hufanya kazi?</p>

		e) kuthamini kazi mbalimbali ili kutambua huduma zinazotolea na watu wanaofanya kazi mbalimbali.		
	Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (Vipindi 2)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: a) kusikiliza kwa makini masimulizi kuhusu kazi mbalimbali ili kuimarisha usikivu b) kuelezea kuhusu kazi mbalimbali ili kuimarisha stadi ya kuzungumza c) kutaja majina ya kazi mbalimbali na watu wanaozifanya ili kuimarisha stadi ya kuzungumza d) kuthamini kazi mbalimbali.	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi asimulie kuhusu kazi mbalimbali. • Mwanafunzi ashiriki katika mjadala kuhusu kazi mbalimbali. • Mwanafunzi eleze umuhimu wa kazi mbalimbali. • Mwanafunzi aweza kushiriki katika nyimbo au mashairi kuhusu kazi mbalimbali. • Mwanafunzi ashiriki katika kuigiza kazi inayofanywa na watu mbalimbali. • Mwanafunzi aweza kumsikiliza mgeni mwalikwa anapozungumzia kuhusu kazi mbalimbali. • Wanafunzi waweza kutazama picha au michoro inayoonyesha watu na kazi mbalimbali wjadiliane katika vikundi. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Ni kazi zipi unazozijua? 2) kazi unazozijua zina umuhimu gani?
	Kusoma: Hadithi (Vipindi 3)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: a) kutambua picha za watu na kazi mbalimbali ili kuimarisha ufahamu wa hadithi b) kusikiliza hadithi ikisomwa na mwalimu kuhusu kazi mbalimbali ili kuimarisha usomaji na usikivu c) kusoma hadithi kuhusu kazi mbalimbali ili kuimarisha stadi ya kusoma	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi. • Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi. • Mwanafunzi afahamu matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi. • Wanafunzi waweza kusoma katika darasa, wakiwa wawili na baadaye mwanafunzi asome peke yake. • Mwanafunzi anaweza kusikiliza hadithi ikisomwa kupitia vifaa vya kiteknolojia kama vile tarakilishi na projekta. • Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kwa kutumia jitabu mbele ya darasa. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Unaona nini kwenye picha? 2) Ni aina gani ya kazi ambayo imewasilishwa kwenye picha?

		<p>d) kufahamu hadithi aliyoisoma na aliyosomewa kuhusu kazi mbalimbali ili kupata ujumbe</p> <p>e) kuchangamkia kusoma hadithi.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi athibitisha utabiri wake baada ya kusoma hadithi. • Mwanafunzi ajibu na kuuliza kuhusu hadithi aliyosoma. 	
	<p>Kuandika (<i>Vipindi 3</i>)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kuandika kisa kifupi kwa hati nadhifu kulingana na mada ili kujenga stadi ya uandishi</p> <p>b) kufurahia uandishi wa visa tofauti ili kuimarisha mawasiliano andishi.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi apewe hadithi yenye mapengo ajaze kwa maneno mwafaka. • Mwanafunzi aeleze yaliyo muhimu katika uandishi k.v. mwandiko nadhifu, maudhui, mtiririko n.k. • Mwanafunzi asome kielelezo cha kisa kilichoandikwa. • Wanafunzi waweza wakaandika kisa kifupi wakiwa wawili wawili. • Mwanafunzi aandike kisa kifupi kinachohusiana na mada. Kisa hiki kifuata hatua tano za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, marejeleo, uhariri na uchapishaji. 	<p>1) Je, ni mambo yapi yanayofaa kuzingatiwa unapoandika kisa?</p> <p>2) Je, unaweza kuandika kisa gani kifupi kinachohusiana na kazi yoyote?</p>
	<p>Sarufi: Ukanusho wa nyakati (<i>Vipindi 2</i>)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze;</p> <p>a) kutambua ukanusho wa -li-; -na-; -ta- katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano</p> <p>b) kusoma ukanusho wa nyakati katika sentensi ili kuimarisha usomaji</p> <p>c) kuandika ukanusho wa nyakati katika sentensi ili kujenga ubunifu</p> <p>d) kuchangamkia matumizi ya nyakati katika mawasiliano.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Wanafunzi watumie -li-; -na-; -ta- kuelezea vitendo walivyofanya katika wakati uliopita (LI), ulipo (NA) na ujao (TA) wakiwa katika vikundi au wawili wawili. • Mwanafunzi akamilishe vifungu kwa kutumia -li-; -na-; -ta- na ukanusho wake. • Mwanafunzi asome vifungu vyenye matumizi -li-; -na-; -ta- na ukanusho wake. • Mwanafunzi aweza kupewa zoezi la ukanusho wa nyakati akiwa peke yake, wawili wawili au katika kikundi. • Mwanafunzi aweza kutazama jinsi nyakati zinavyokanushwa katika vifaa vya kiteknolojia na kufanyia zoezi kwenye mtandao. 	<p>1) Unafanya nini sasa?</p> <p>2) Ulifanya nini jana?</p> <p>3) Utafanya nini kesho?</p> <p>4) Je, ni nyakati zipi ambazo unajua kukanusha?</p>

Umilisi wa kimsingi unaokuzwa: mawasiliano na ushirikiano – kushirikiana kufanya kazi katika vikundi kujiamini/kujithamini – kuthamini na kutambua kazi mbalimbali; Kujibu maswali ya kisarufi vilivyo ubunifu – Katika utunzi wa sentensi na kujibu maswali ya ufahamu ambayo majibu yake si ya moja kwa moja ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza.			
Uhusiano na masuala mtambuko: shughuli zinazomsaidia mwanafunzi: mwongozo wa ajira – kuthamini kazi mbalimbali stadi za Maisha – ujuzi wa kazi mbalimbali na umuhimu wake.		Uhusiano na Maadili: uwajibikaji; uzalendo; umoja na heshima	
Uhusiano na masomo mengine: English Activities, Environmental Activities		Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji: kusaidia wazazi katika kazi za nyumbani na katika jamii kuthamini kazi zinazofanywa na wazazi, ndugu na watu wengine katika jamii.	
Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji: kushiriki katika kuigiza, kuimba nyimbo na kukariri mashairi katika tamasha mbalimbali.		Mapendekezo ya Tathmini: <ul style="list-style-type: none"> • kuhakiki matamshi ya sauti mbili zinazotamkwa pamoja • kuchunguza anavyotambua kazi mbalimbali • kuchunguza anavyotumia ukanusho wa nyakati katika mawasiliano • kuchunguza anavyosoma na kusimulia hadithi • kuchunguza ufahamu wake wa hadithi aliyosoma au kusomewa • kuchanganua anavyojibu maswali ya kusema na ya kuandika • kufuatilia mwandiko wake. 	

Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
Mwanafunzi, <ul style="list-style-type: none"> • anatamka sauti ipasavyo na kwa ufasaha • anaelezea kuhusu kazi mbalimbali kwa ufasaha. • anasoma maneno, sentensi na hadithi 	Mwanafunzi, <ul style="list-style-type: none"> • anatamka sauti ipasavyo. • anaelezea kuhusu kazi mbalimbali • anasoma maneno, sentensi na 	Mwanafunzi, <ul style="list-style-type: none"> • anatamka sauti ipasavyo • anataja kazi mbalimbali • anasoma baadhi ya maneno, sentensi na 	Mwanafunzi, <ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto kutamka sauti • ana changamoto kuelezea kuhusu kazi mbalimbali • ana changamoto katika kusoma

<p>kwa ufasaha na ukakamavu</p> <ul style="list-style-type: none"> • anafahamu kwa wepesi hadithi aliyosoma na kusomewa • anatomia kikomo ipasavyo • anaandika kisa kwa ubunifu, mtiririko, hati nadhifu na kwa kasi ifaayo. 	<p>hadithi kwa ufasaha</p> <ul style="list-style-type: none"> • anafahamu hadithi aliyosoma na kusomewa • anatomia kikomo ipasavyo • anaandika kisa kwa mtiririko na hati bora. 	<p>hadithi vilivyo</p> <ul style="list-style-type: none"> • anafahamu baadhi ya hadithi alizosoma au kusomewa. • anatomia kikomo • anaandika kisa kwa hati zinazosomeka. 	<p>maneno, sentensi na hadithi</p> <ul style="list-style-type: none"> • anachangamoto katika kufahamu hadithi aliyosoma au kusomewa • ana changamoto katika kutumia kikomo • ana changamoto katika kuandika kisa kuhusu mada aliyopewa.
---	--	---	--

MADA	MADA NDOGO	MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA	MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI	MASWALI DADISI
Usalama	Msamiati. (<i>Vipindi 3</i>)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua msamiati ambao hutumiwa katika usalama ili kuimarisha mawasiliano</p> <p>b) kusoma msamiati unaohusiana na usalama ili kujenga usomaji bora</p> <p>c) kueleza maana ya msamiati wa usalama ili kuimarisha ufahamu</p> <p>d) kutumia msamiati wa usalama katika sentensi ili kuimarisha ufahamu</p> <p>e) kuandika maneno yanayohusiana na usalama ili kujenga uandishi bora</p> <p>f) kuthamini usalama katika mazingira yake.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi asome maneno yanayohusiana na usalama kwa kutumia kadi za maneno. • Mwanafunzi aeleze maana ya msamiati wa usalama akiwa peke yake au katika vikundi. • Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati wa usalama. • Mwanafunzi aweza kutazama video kuhusu usalama k.m. utekaji nyara na moto na kisha kujadili jinsi ya kujilinda kutokana na hatari. • Mwanafunzi atazame michoro na picha inayolenga maana ya maneno kuhusu usalama. • Wanafunzi wajadiliane kuhusu umuhimu wa usalama. 	<p>1) Je, ni nini maana usalama?</p> <p>2) Usalama huhusisha mambo yapi?</p>

	<p>Kusikiliza na Kuzungumza: Maagano (Vipindi 2)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweza:</p> <ol style="list-style-type: none"> kutambua maneno yanayotumiwa katika maagano ili kuwezesha mazungumzo kutumia maneno yanayotumiwa katika maagano kwenye mawasiliano kujibu maagano kwa njia ifaayo ili kudhihirisha ufahamu kuthamini matumizi ya maagano katika mawasiliano ya kila siku. 	<ul style="list-style-type: none"> Mwanafunzi anaweza kueleza matumizi ya maagano kama vile: kwaheri; siku njema, mchana mwema, safiri salama na usiku mwema. Mwanafunzi atazame michoro inayoashiria vitendo vya kuagana. Mwanafunzi ashiriki katika maigizo ya kuagana. Mwanafunzi aweza kutazama vibonzo katika tarakilishi vikiigiza vitendo na maneno mbalimbali ya kuagana. Mwanafunzi aweza kutaja neno la kuagana linalofaa kutokana na maelezo mbalimbali akiwa peke yake, wawili wawili au katika vikundi. 	<ol style="list-style-type: none"> Je, ulipoagana na mzazi asubuhi alikwambiaje? Je, mzazi hukwambiaje unapoenda kulala? Mtu anaposafiri anaambiwaje?
	<p>Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (Vipindi 2)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <ol style="list-style-type: none"> kutambua mambo yanayoathiri usalama ili kujihakikishia usalama kutambua njia za kudumisha usalama katika mazingira yake ili kujihakikishia usalama kusimulia kuhusu mambo yanayoweza kuhatarisha usalama katika mazingira yake ili kuimarisha stadi ya kuzungumza kusikiliza masimulizi kuhusu usalama ili kujenga stadi ya kusikiliza kuthamini umuhimu wa usalama katika maisha ya kila siku. 	<ul style="list-style-type: none"> Mwanafunzi asimulie baadhi ya mambo. yanayoweza kuhatarisha usalama katika mazingira yake kupitia k.m. mgeni mwalikwa. Mwanafunzi aweza kutazama video inayoonyesha mambo yanayoathiri usalama katika mazingira yake. Mwanafunzi wajiadiliane namna ya kuepuka dhuluma k.m. kutozungumza na watu wasiwajua, kupiga ukelele anapokumbwa na hatari. Mwanafunzi aandike baadhi ya mambo yanayoathiri usalama katika mazingira yake. Mwanafunzi asimulie kisa alichokishuhudia kuhusu usalama. 	<ol style="list-style-type: none"> Usalama ni nini? Usalama unatusaidia na nini? Unaweza ukafanya nini unapovamiwa?

	Kusoma: Hadithi (<i>Vipindi 3</i>)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: a) kutambua picha zinazoonyesha usalama katika mazingira mbalimbali ili kurahisisha ufahamu b) kutambua maneno yanayohusiana na usalama ili kuyatumia katika mawasiliano c) kusikiliza hadithi za mwalimu kuhusu usalama ili kuimarisha ufahamu d) kusoma hadithi kuhusu usalama ili kujenga usikivu e) kufahamu hadithi aliyosoma na aliyosomewa kuhusu usalama ili kupata ujumbe f) kuthamini umuhimu wa usalama katika maisha ya kila siku.	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi. • Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi • Mwanafunzi afahamu matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi. • Mwanafunzi asome darasani, wakiwa wawili na baadaye asome peke yake. • Wanafunzi wasomeana hadithi wakiwa wawili wawili au katika vikundi. • Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi husika ikisomwa kupitia kinasa sauti. • Mwanafunzi aweza kutazama video ya mtu mzima au mtoto akisoma hadithi husika kwa ufasaha kisha aige usomi huo. • Mwanafunzi athibitisha utabiri wake baada ya kusoma hadithi. • Mwanafunzi aweza kusimulia hadithi kutokana na picha alizopewa kuhusu usalama. • Mwanafunzi atoe muhtasari wa hadithi aliyosoma au kusomewa. • Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali kutokana na hadithi. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Je, usalama unahusu nini? 2) Ukosefu wa salama husababishwa na nini? 3) Unapojipata kwenye hatari unafaa kufanya nini?
	Kuandika (<i>Vipindi 3</i>)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: a) kutambua kisa chenye mtiririko b) kuandika kisa kifupi kwa hati nadhifu kulingana na mada c) kufurahia uandishi wa visa tofauti	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aweza kupewa hadithi yenye mapengo ajaze kwa maneno mwafaka. • Mwanafunzi aongozwe kujadili yaliyo muhimu katika uandishi k.v. mwandiko nadhifu, maudhui, mtiririko n.k. • Mwanafunzi aweza kusoma kielelezo cha kisa 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Je, ni mambo yapi yanayofaa kuzingatiwa unapoandika kisa? 2) Je, unaweza kuandika kisa gani

		maishani.	kilichoandikwa. <ul style="list-style-type: none"> • Wanafunzi waweza kuandika kisa kifupi wakiwa wawili wawili. • Mwanafunzi apewe fursa ya kuandika kisa kifupi kinachohusiana na mada. Kisa hiki kifuatake hatua tano za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, marejeleo, uhariri na uchapishaji. 	kifupi kinachohusiana na usalama?
	Sarufi: Vinyume vya vitendo (<i>Vipindi 2</i>)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze; <ol style="list-style-type: none"> a) kutaja vinyume vya vitendo b) kusoma sentensi zilizo na vinyume vya vitendo c) kuandika vinyume vya vitendo d) kuchangamkia kutumia vitendo na vinyume vyake katika mawasiliano ya kila siku. 	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aweza kufafanuliwa juu ya vinyume vya vitendo kama vile lala-amka; keti- simama; cheka-lia; tabasamu – nuna; enda-rudi; panda – shuka nk. • Wanafunzi waweza kuigiza vinyume vya vitendo wakiwa wawili wawili. • Mwanafunzi aweza kushirikishwa kutunga na kusoma sentensi zilizo na vinyume vya vitendo. • Mwanafunzi aweza kuelekezwa kuandika vinyume vya vitendo. 	1) Je, unajua vinyume vya vitendo unavyofanya kila siku?
Umilisi wa kimsingi unaokuzwa: mawasiliano na ushirikiano - wanafunzi washiriki katika vikundi ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza ubunifu – unadhihirishwa na usimulizi na utungaji wa sentensi.				
Uhusiano na masuala mtambuko: Elimu ya maendeleo endelevu: elimu ya usalama – kupitia kwa kutambua umuhimu na mbinu za kujilinda na hali zinazohatarisha usalama Stadi za maisha – mbinu za kujilinda dhidi ya tisho kwa usalama wake.		Uhusiano na Maadili: uwajibikaji -kuwa na msimamo thabiti katika uamuzi wake haki za kijamii- kufuata haki zake anapodhulumiwa.		
Uhusiano na masomo mengine: Environmental Activities; Hygiene and Nutrition; English Activities.		Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji: kusaidia kuhamasisha jamii kuhusu usalama kushiriki katika kutetea haki za kijamii.		

<p>Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji: Kushiriki katika kuimba nyimbo na kukariri mashairi katika tamasha mbalimbali kuhusu usalama.</p>	<p>Mapendekezo ya Tathmini:</p> <ul style="list-style-type: none"> • kuchunguza anavyotumia msamiati wa usalama katika mawasiliano • kuchunguza anavyotumia vinyume vya vitendo katika mawasiliano • kuchanganua anavyojibu maswali ya kusema na ya kuandika • kuchunguza ufahamu wake wa hadithi aliyosoma au kusomewa • kuhakiki anavyosoma na kusimulia hadithi • kufuatilia mwandiko wake.
---	---

Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • anatambua na kutumia mbinu mbalimbali za kujiepusha na hali zinazoweza kuhatarisha usalama wake • anatumia maneno ya maagano ifaavyo kila wakati • anasimulia kisa alichokishuhudia kuhusu usalama kwa ubunifu na ufasaha • anasoma maneno, sentensi na hadithi kwa ufasaha na ukakamavu • anaandika vinyume vya vitendo kwa usahihi • anaandika kisa kwa ubunifu, mtiririko, kwa hati nadhifu na kwa kasi ifaayo. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • anatambua mbinu mbalimbali za kujiepusha na hali zinazoweza kuhatarisha usalama wake • anatumia maneno ya maagano ifaavyo • anasimulia kisa alichokishuhudia kuhusu usalama kwa ufasaha • anasoma maneno, sentensi na hadithi kwa ufasaha • anaandika vinyume vya vitendo kwa usahihi • anaandika kisa kwa mtiririko na hati bora. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • anatambua mbinu mbalimbali za kujiepusha na hali zinazoweza kuhatarisha usalama wake • anatumia maneno ya maagano ifaavyo • anaelezea kuhusu kisa alichoshuhudia bila mtiriko wenye mantiki • anasoma maneno, sentensi na baadhi ya hadithi kwa ufasaha • ana changamoto kuandika vinyume vya baadhi ya vitendo kwa usahihi • anaandika kisa kwa hati zinazosomeka. 	<p>Mwanafunzi,</p> <ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto kutambua mbinu mbalimbali za kujiepusha na hali zinazoweza kuhatarisha usalama wake • ana changamoto katika kutumia baadhi ya maneno ya maagano katika mawasiliano • ana changamoto kusimulia kisa alichokishuhudia kuhusu usalama • ana changamoto kusoma maneno, sentensi na hadithi kwa ufasaha • ana changamoto kuandika vinyume vya vitendo kwa usahihi • ana changamoto kuandika kisa.

MADA	MADA NDOGO	MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA	MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI	MASWALI DADISI
Usafi wa Mazingira	Msamiati (<i>Vipindi 3</i>)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: a) kutambua msamiati wa usafi wa mazingira b) kutumia msamiati wa usafi wa mazingira katika sentensi c) kubainisha mazingira safi na yale machafu d) kuthamini mazingira safi.	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aweza kuelekezwa kusoma maneno yanayohusiana na usalama kwa kutumia kadi za maneno. • Mwanafunzi aweza kuelekezwa kutoa maana ya msamiati unaohusiana na usafi wa mazingira. • Wanafunzi waweza kujadiliana kuhusu maana za maneno yanayohusiana na usafi wa mazingira. • Mwanafunzi aweza kutunga sentensi sahihi kwa kutumia msamiati unaohusiana na usafi wa mazingira. • Mwanafunzi aweza kutazama video kuhusu usafi wa mazingira k.m. kuokota na kuchoma taka, kufyeka nyasi n.k. • Mwanafunzi aweza kutazama michoro na picha zinazolenga maana ya maneno kuhusu usafi wa mazingira. • Wanafunzi waweza kujadiliana kuhusu umuhimu wa usafi wa mazingira wakiwa kwenye vikundi. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Je, unajua msamiati gani unaohusiana na usafi wa mazingira? 2) Unaweza kutumia msamiati gani unaohusiana na usafi wa mazingira sentensi? 3) Mazingira safi ni yapi?
	Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (<i>Vipindi 2</i>)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: a) kutofautisha mazingira safi na yasiyo safi b) kutambua umuhimu wa mazingira safi c) kusikiliza masimulizi kuhusu usafi wa mazingira d) kuelezea kuhusu usafi wa mazingira	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aweza kufahamu maana ya usafi wa mazingira. • Wanafunzi waongozwe katika vikundi kusimulia visa vinavyohusiana na usafi wa mazingira k.v. umuhimu na jinsi ya kutunza mazingira • Mwanafunzi aweza kuigiza jinsi ya kudumisha usafi katika mazingira yake • Wanafunzi waweza kutazama video inayohusu mazingira safi na chafu kisha wabainishe mazingira 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Ni nini maana ya mazingira? 2) Mazingira safi ni yapi? 3) Je, tunawezaje kuborasha mazingira?

		<p>e) kuelezea jinsi ya kutunza mazingira yake</p> <p>f) kufurahia mazingira safi maishani mwake.</p>	<p>wanayofurahia.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi anaweza kuchora vifaa vinavyotumiwa kusafisha mazingira. • Wanafunzi waweza kujadiliana kuhusu jinsi wanavyoweza kuchangia katika usafi wa mazingira. • Mgeni aweza kualikwa ili kusimulia kuhusu mazingira huku wanafunzi wakiandika yaliyo muhimu na kuuliza na kujibu maswali. 	
	<p>Kusoma: Hadithi (Vipindi 3)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze;</p> <p>a) kutambua msamiati uliotumiwa katika hadithi</p> <p>b) kusikiliza mwalimu kwa makini anaposoma hadithi kuhusu usafi wa mazingira</p> <p>c) kusoma hadithi kuhusu mazingira safi</p> <p>d) kufahamu hadithi aliyosoma na aliyosomewa kuhusu usafi wa mazingira</p> <p>e) kuthamini mazingira safi.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aweza kujadili kuhusu picha zilizojumuishwa kwenye hadithi. • Mwanafunzi aweza kutabiri kitakachotokea kwenye hadithi. • Mwanafunzi aweza kuthibitisha utabiri wake baada ya kusoma hadithi. • Mwanafunzi aweza kufahamu matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi. • Wanafunzi waweza kusoma kama darasa, wakiwa wawili na baadaye asome peke yake. • Mwanafunzi aweza kutoa muhtasari wa hadithi aliyosoma au kusomewa. • Mwanafunzi aweza kutabiri kitakachotokea katika hadithi katika kundi la wawili wawili au darasa zima. • Wanafunzi waweza kusomeana hadithi wakiwa wawili wawili. • Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi husika ikisomwa kupitia kinasasauti. • Mwanafunzi aweza kutazama video ya mtu au mtoto akisoma hadithi husika kwa ufasaha, kisha aige usomi 	<p>1) Je, unaweza kukumbuka hadithi gani uliyosoma?</p> <p>2) Je, hadithi unayoweza kukumbuka inahusu nini?</p> <p>3) Je, umeweza kusoma hadithi ngapi?</p>

			<p>u.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Wanafunzi waweza kusomeana hadithi katika vikundi. • Mwanafunzi aweza kusimulia hadithi kutokana na picha alizopewa kuhusu mazingira. • Mwanafunzi aweza kuuliza na kujibu maswali kudhihirisha ufahamu. 	
	Kuandika (<i>Vipindi 3</i>)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kuandika kisa kifupi kwa hati nadhifu kulingana na mada ili kujenga stadi ya uandishi</p> <p>b) kufurahia uandishi wa visa tofauti ili kuimarisha mawasiliano andishi.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi apewe hadithi yenye mapengo ajaze kwa maneno mwafaka. • Mwanafunzi aeleze yaliyo muhimu katika uandishi kama vile mwandiko nadhifu, maudhui, mtiririko n.k. • Mwanafunzi asome kielelezo cha kisa kilichoandikwa na mwanafunzi. • Wanafunzi waweza kuandika kisa kifupi wakiwa wawili wawili. • Mwanafunzi aandike kisa kifupi kinachohusiana na mada. Kisa hiki kifuata hatua tano za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, marejeleo, uhariri na uchapishaji. 	<p>1) Je, ni mambo yapi yanayofaa kuzingatiwa unapoandika kisa?</p> <p>2) Je, unaweza kuandika kisa kifupi kinachohusiana na usafi wa mazingira?</p>
	Sarufi: Matumizi ya haraka na polepole (<i>Vipindi 2</i>)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua matumizi ya haraka na polepole ili kuimarisha mawasiliano mwafaka</p> <p>b) kutumia haraka na polepole katika kutunga sentensi ili kuimarisha mawasiliano mwafaka</p> <p>c) kusoma sentensi zilizo na matumizi ya haraka na polepole ili kujenga usomaji bora</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aweza kujaza mapengo kwa kutumia haraka na polepole. • Mwanafunzi aweza kubainisha matumizi ya vielezi vya jinsi vinavyofunzwa kwa kutumia vifaa vya kiteknolojia. • Mwanafunzi atazame vitu mbalimbali na avirejeele kwa kutumia haraka na polepole k.m Mtoto anatembea polepole. • Wanafunzi washiriki katika maigizo wakitumia haraka na polepole wakiwa darasani. • Mwanafunzi aandike maneno na sentensi kwa kutumia haraka na polepole. 	<p>1) Unatumia maneno gani kuelezea namna mtu alivyofanya jambo?</p> <p>2) Unatumia maneno gani kuelezea namna mtu anavyotembea?</p>

		d) kuandika majina na sentensi kuhusu ndege ili kuimarisha uandishi bora e) Kuchangamkia matumizi ya haraka na polepole katika mawasiliano.		
Umilisi wa kimsingi unaokuzwa: mawasiliano na ushirikiano - wanafunzi washiriki katika vikundi ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza hamu ya kujifunza zaidi - kutambua umuhimu wa mazingira.				
Uhusiano na masuala mtambuko: Elimu ya maendeleo endelevu– kupitia kwa kutambua umuhimu wa kudumisha usafi katika mazingira yake.		Uhusiano na Maadili: uwajibikaji katika kuweka mazingira yakiwa safi.		
Uhusiano na masomo mengine: Environmental Activities na Hygiene and Nutrition Activities		Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji: kushiriki katika kusafisha mazingira k.m kuokota taka.		
Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji: Kuimba nyimbo na kukariri mashairi katika tamasha mbalimbali shuleni kuhamasisha kuhusu usafi wa mazingira.		Mapendekezo ya Tathmini: <ul style="list-style-type: none"> • kuchunguza anavyotumia msamiati wa usafi wa mazingira katika mawasiliano • kuchunguza anavyotumia haraka na polepole katika mawasiliano • kuchanganua anavyojibu maswali ya kusema na ya kuandika • kuchunguza ufahamu wake wa hadithi aliyosoma au kusomewa • kuhakiki anavyosoma na kusimulia hadithi • kufuatilia mwandiko wake. 		

Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
Mwanafunzi, <ul style="list-style-type: none"> • anasikiliza na kuzungumza kuhusu usafi wa mazingira kwa ufasaha na ubunifu • anasoma hadithi kuhusu usafi wa mazingira kwa ufasaha na ukakamavu 	Mwanafunzi, <ul style="list-style-type: none"> • anasikiliza na kuzungumza kuhusu usafi wa mazingira kwa ufasaha • anasoma hadithi kuhusu usafi 	Mwanafunzi, <ul style="list-style-type: none"> • anasikiliza na kuzungumza kuhusu usafi wa mazingira • anasoma baadhi ya hadithi vilivyo 	Mwanafunzi, <ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto katika kusikiliza na kuzungumza kuhusu usafi wa mazingira • ana changamoto katika kusoma

<ul style="list-style-type: none"> • anafahamu kwa wepesi aliyosoma na kusomewa • anatomia haraka na polepole kwa usahihi kila wakati • anaandika kisa kwa ubunifu, mtiririko, kwa hati nadhifu na kwa kasi ufaavyo. 	<p>wa mazingira kwa ufasaha</p> <ul style="list-style-type: none"> • anafahamu aliyosoma na kusomewa • anatomia haraka na polepole kwa usahihi • anaandika kisa kwa mtiririko na kwa hati bora. 	<ul style="list-style-type: none"> • anafahamu baadhi ya hadithi alizosoma na kusomewa • anatomia haraka na polepole kwa wastani • anaandika kisa kwa hati zinazosomeka. 	<p>hadithi</p> <ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto katika kufahamu aliyosoma na kusomewa • ana changamoto katika kutumia haraka na polepole katika sentensi • ana changamoto kuandika kisa.
---	--	---	--

MADA	MADA NDOGO	MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA	MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI	MASWALI DADISI
Dukani	Msamiati (<i>Vipindi 3</i>)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze</p> <p>a) kutambua msamiati wa dukani ili kuutumia katika mawasiliano</p> <p>b) kusoma maneno yanayohusiana na shughuli za dukani ili kujenga usomaji bora</p> <p>c) kueleza maana ya msamiati wa dukani ili kuimarisha stadi ya kuzungumza</p> <p>d) kutumia msamiati wa dukani katika sentensi sahihi ili kuimarisha stadi ya kuzungumza</p> <p>e) kuandika maneno yanayohusiana na uuzaji na ununuzi ili kuimarisha stadi ya kusoma</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi asome maneno yanayohusiana na shughuli za dukani kwa kutumia kadi za maneno kama vile nunua, uza, bei, kilo, mnunuzi, mwuzaji, hasara, faida, pesa, baki, sarafu na noti. • Mwanafunzi ashiriki katika majadiliano kuhusu maana ya maneno yanayohusiana na shughuli za dukani kwa kutumia picha au michoro. • Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati wa dukani. • Mwanafunzi aweza kutazama video kuhusu uuzaji na ununuzi. • Wafunzi washiriki katika majadiliano kuhusu umuhimu wa kufanya biashara wakiwa kwenye vikundi. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Mtu anayenunua kitu dukani huitwaje? 2) Mtu anayeua dukani huitwaje? 3) Pesa unazorudishiwa unaponunua kitu dukani huitwaje?

		f) kuthamini shughuli za biashara.		
	Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (Vipindi 2)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: a) kutambua maneno yanayotumiwa katika muktadha wa dukani ili kuimarisha ufahamu b) kueleza shughuli za dukani ili kuimarisha stadi ya kuzungumza c) kusikiliza masimulizi kuhusu uuzaji na ununuzi ili kujenga usikivu d) kuthamini biashara katika maisha ya kila siku.	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi asimulie kuhusu shughuli za dukani . • Mwanafunzi aweza kumsikiliza mgeni mwalikwa anapotoa wasilisho lake kuhusu shughuli za dukani. • Mwanafunzi atambue maneno yanayotumiwa katika muktadha wa dukani kama vile, uuzaji, bei, kilo, ununuzi, hasara, faida, pesa na baki. • Mwanafunzi asikilize kwa makini hadithi zinazosimuliwa kuhusu muktadha wa dukani kwa kutumia maneno. • Mwanafunzi aweza kutazama video inayoonyesha mambo yanayohusiana na ununuzi na uuzaji dukani. • Mwanafunzi ashiriki katika mjadala kuhusu shughuli za dukani katika vikundi. • Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kuhusu shughuli za dukani. • Mwanafunzi aweza kuigiza kuuza na kununua katika duka la darasani. 	<p>1) Je, umewahi kununua nini dukani?</p> <p>2) Je, ulitumia kiasi gani cha pesa kununua ulichotumwa?</p>
	Kusoma: Hadithi (Vipindi 3)	Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: a) kutambua msamiati uliotumiwa katika hadithi ili kuwezesha ufahamu b) kusikiliza hadithi ikisomwa na mwalimu kuhusu shughuli za dukani ili kuimarisha stadi ya kusikiliza c) kusoma hadithi kuhusu dukani kwa ufasaha ili kujenga usomaji bora d) kufahamu hadithi aliyoisoma na	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi asikilize mwalimu akisoma hadithi ya mwalimu na baadaye kuuliza na kujibu maswali. • Mwanafunzi asome pamoja na wengine darasani, kisha wasome wawili wawili na baadaye asome peke yake. • Mwanafunzi ajadili picha kwenye hadithi. • Mwanafunzi atabiri kuhusu kitakachotokea katika hadithi wakiwa wawili wawili. • Mwanafunzi ashirikiane na wengine kujadili msamiati uliotumika katika hadithi. • Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi husika ikisomwa 	<p>1) Umewahi kusoma hadithi gani kuhusu dukani?</p> <p>2) Je, ni hadithi gani iliyokufurahisha zaidi?</p>

		<p>aliyosomewa kuhusu shughuli za dukani ili kupata ujumbe</p> <p>g) kuthamini biashara maishani kama njia moja ya kujitegemea maishani.</p>	<p>kupitia kinasasauti na kisha kuijadili.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aweza kutazama video ya mtu mzima au mtoto akisoma hadithi husika kwa ufasaha kisha aige usomi ule. • Wanafunzi waweza kusomeana hadithi katika vikundi. • Mwanafunzi atoe muhtasari wa hadithi aliyosoma • Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali. • Mwanafunzi ashiriki kujadili baadhi ya maswali darasani, katika vikundi au wakiwa wawili wawili. 	
	<p>Kuandika (<i>Vipindi 3</i>)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kuandika kisa kifupi kwa hati nadhifu kulingana na mada ili kujenga stadi ya uandishi</p> <p>b) kufurahia uandishi wa visa tofauti ili kuimarisha mawasiliano andishi.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi apewe hadithi yenye mapengo ajaze kwa maneno mwafaka. • Mwanafunzi aeleze yaliyo muhimu katika uandishi k.v. mwandiko nadhifu, maudhui, mtiririko n.k. • Mwanafunzi asome kielelezo cha kisa kilichoandikwa na mwanafunzi. • Wanafunzi waweza kuandika kisa kifupi wakiwa wawili wawili. • Mwanafunzi aandike kisa kifupi kinachohusiana na mada. Kisa hiki kifuatake hatua tano za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, marejeleo, uhariri na uchapishaji. 	<p>1) Je, ni mambo yapi yanayofaa kuzingatiwa unapoandika kisa?</p> <p>2) Je, ni mambo gani utakayoshughuliki a katika ukiandika kuhusu dukani?</p>
	<p>Sarufi: Matumizi ya alama ya kuuliza(?) (<i>Vipindi 2</i>)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua matumizi ya alama ya kuuliza (?) katika kuimarisha mawasiliano</p> <p>b) kusoma sentensi zilizo na matumizi ya alama ya kuuliza (?) katika</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi aandike alama ya kuuliza (?). • Mwanafunzi afafanue matumizi ya alama ya kuuliza (?). • Mwanafunzi atunge sentensi akitumia alama ya kuuliza (?). • Mwanafunzi asome sentensi zilizo na alama ya kuuliza (?). 	<p>1) Je, alama (?) huitwaje?</p> <p>2) Je, utatumia alama (?) unapofanya nini?</p>

		kuimarisha stadi ya kusoma c) kuandika sentensi akitumia alama ya kuuliza (?) katika kuimarisha stadi ya kuandika d) kuthamini matumizi ya alama ya kuuliza (?) katika mawasiliano.	<ul style="list-style-type: none"> • Wanafunzi waweza kushirikishwa kusoma sentensi zinazotumia alama ya kuuliza (?) wakiwa wawili wawili au katika vikundi. • Mwanafunzi aandike sentensi akitumia alama ya kuuliza (?). 	
Umilisi wa kimsingi unaokuzwa: mawasiliano na ushirikiano - wanafunzi washiriki katika vikundi ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza ubunifu – unadhihirishwa na usimulizi na utungaji wa sentensi.				
Uhusiano na masuala mtambuko: Elimu ya maendeleo endelevu: elimu ya maswala ya kifedha katika ujuzi wa kutumia pesa vizuri. stadi za maisha – Kuwa na ujasiri wa kwenda na kufanya maamuzi mwafaka ya ununuzi.		Uhusiano na Maadili: uwajibikaji – Kuweza kuwa mwadilifu katika matumizi ya pesa dukani. ushirikiano – Kufanya kazi katika vikundi.		
Uhusiano na masomo mengine: Mathematics Activities, English Activities.		Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji: kuweza kutumwa dukani na wazazi na kutumia pesa inavyofaa.		
Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji: kushiriki katika maigizo ya shughuli za dukani shuleni kushiriki katika majadiliano kuhusu bidhaa zinazopatikana dukani.		Mapendekezo ya Tathmini: <ul style="list-style-type: none"> • kuchunguza anavyotumia msamiati wa dukani katika mawasiliano • kuchunguza anavyotumia alama ya kuuliza katika mawasiliano • kuchanganua anavyojibu maswali ya kusema na ya kuandika • kuchunguza ufahamu wake wa hadithi aliyosoma au kusomewa • kuhakiki anavyosoma na kusimulia hadithi • kufuatilia mwandiko wake. 		

Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
Mwanafunzi,	Mwanafunzi,	Mwanafunzi,	Mwanafunzi,

<ul style="list-style-type: none"> • anatambua na kutumia msamiati wa dukani ipasavyo • anasimulia kisa kuhusu shughuli za dukani kwa ubunifu na ufasaha • anasoma maneno, sentensi na hadithi kuhusu shughuli za dukani kwa ufasaha na ukakamavu • anafahamu kwa wepesi anayosoma au kusomewa • anatumia alama ya kuuliza katika maandishi kila inapohitajika • anaandika kisa kwa ubunifu, mtiririko, kwa hati nadhifu na kwa kasi ifaayo. 	<ul style="list-style-type: none"> • anatambua msamiati wa dukani • anasimulia kisa kuhusu shughuli za dukani kwa ufasaha • anasoma maneno, sentensi na hadithi kuhusu shughuli za dukani kwa ufasaha • anafahamu anayosoma au kusomewa • anatumia alama ya kuuliza katika maandishi • anaandika kisa kwa mtiririko na kwa hati bora. 	<ul style="list-style-type: none"> • anatambua baadhi ya msamiati wa dukani. • anasimulia kisa kuhusu shughuli za dukani • anasoma baadhi maneno, sentensi na hadithi kuhusu shughuli za dukani • anafahamu baadhi ya mambo anayosoma au kusomewa • anatumia alama ya kuuliza katika baadhi ya sentensi • anaandika kisa kwa hati zinazosomeka. 	<ul style="list-style-type: none"> • ana changamoto katika kutambua baadhi ya msamiati wa dukani • ana changamoto katika kusimulia kisa kuhusu shughuli za dukani • ana changamoto katika kusoma baadhi ya maneno, sentensi na hadithi kuhusu shughuli za dukani • ana changamoto katika kufahamu hadithi aliyosoma au kusomewa • ana changamoto katika kuakifisha sentensi kwa kutumia alama ya kuuliza • ana changamoto katika kuandika kisa kuhusu mada aliyofunzwa.
--	---	---	---

MADA	MADA NDOGO	MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA	MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI	MASWALI DADISI
Ndege Nimpendaye	Msamiati (Vipindi 3)	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutaja majina ya ndege mbalimbali ili kuimarisha stadi ya kuzungumza</p> <p>b) kutambua msamiati unaotumiwa katika kutunza ndege ili kuimarisha mawasiliano</p> <p>c) kutumia majina ya ndege katika sentensi sahihi ili kuwezesha mazungumzo</p> <p>d) kutumia msamiati wa kutunza</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi atazame picha na kuwatambua ndege tofauti tofauti. • Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati kuhusu ndege. • Mwanafunzi atoe maana ya msamiati unaotumiwa katika kutunza ndege. • Mwanafunzi achore baadhi ya ndege. • Mwanafunzi aweza kutazama video ya utunzaji wa ndege. • Mwanafunzi atazame michoro na picha za ndege wa nyumbani wakitunzwa. 	<p>1) Ni ndege wapi wanaofugwa?</p> <p>2) Unamtunzaje ndege umpendaye?</p>

		<p>ndege katika sentensi ili kuwezesha mazungumzo</p> <p>e) kusoma maneno na sentensi kuhusu ndege ampendaye ili kujenga usomaji bora</p> <p>f) kuandika maneno na sentensi kuhusu ndege ampendaye ili kujenga uandishi bora</p> <p>g) kuthamini utunzaji wa ndege ampendaye.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi asome maneno na sentensi katika kadi na chati kuhusu ndege. • Mwanafunzi aandike majina na sentensi kuhusu ndege. 	
	<p>Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (Vipindi 2)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutaja aina za ndege wa nyumbani anaowajua ili kujenga stadi ya kuzungumza</p> <p>b) kumtambua ndege ampendaye ili kujenga stadi ya kuzungumza</p> <p>c) kusimulia kuhusu ndege ampendaye ili kujenga stadi ya kuzungumza</p> <p>d) kusimulia kuhusu jinsi ndege ampendaye anavyotunzwa ili kujenga stadi ya kuzungumza</p> <p>e) kusikiliza kwa makini masimulizi kuhusu utunzaji wa ndege wa nyumbani ili kujenga usikivu</p> <p>f) kuthamini ndege wa nyumbani.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi ataje aina za ndege anaowajua. • Mwanafunzi atambue ndege ampendaye. • Mwanafunzi asimulie kuhusu ndege ampendaye katika darasa zima, wakiwa wawili wawili na katika vikundi. • Mwanafunzi atazame picha za ndege mbalimbali wa nyumbani ili awatambue. • Mwanafunzi aweza kutazama video na picha zinazoashiria utunzaji wa ndege mbalimbali. • Mwanafunzi asimulie jinsi ya kutunza ndege kupitia kwa mgeni mwalikwa. • Mwanafunzi ashiriki katika mjadala kuhusu jinsi ndege ampendaye anavyotunzwa. • Mwanafunzi waweza kushirikishwa kuimba nyimbo na kukariri mashairi kuhusu ndege wawapendao. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Ni ndege gani umpendaye? 2) Kwa nini unampenda ndege huyo? 3) Unamtunzaje ndege umpendaye?

	<p>Kusoma: Hadithi (<i>Vipindi 3</i>)</p>	<p>Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:</p> <p>a) kutambua msamiati uliotumiwa katika hadithi aliyosoma au kusomewa ili kuimarisha ufahamu</p> <p>b) kusoma hadithi zinazohusu ndege wa nyumbani ili kujenga usomaji bora</p> <p>c) kusikiliza hadithi zinazohusu ndege wa nyumbani zikisomwa ili kujenga usikivu</p> <p>d) kufahamu hadithi aliyosoma na aliyosomewa kuhusu ndege wanaofugwa ili kupata ujumbe</p> <p>e) kuchangamkia kusoma hadithi ili kuendeleza ari ya kusoma zaidi.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi. • Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi. • Mwanafunzi athibitishe utabiri wake baada ya kusoma hadithi. • Wanafunzi washiriki katika kusoma darasani, wakiwa wawili na baadaye asome peke yake. • Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi ya mwalimu au hadithi iliyorekodiwa. • Wanafunzi waweza kusomeana hadithi wakiwa wawili wawili au katika vikundi. • Wanafunzi waweza kusoma hadithi kwa kutumia vifaa vya kiteknolojia k.v. tarakilishi na projekta. • Mwanafunzi atunge sentensi akitumia msamiati uliotumiwa katika hadithi. • Mwanafunzi anakili majina na sentensi zinazojumuisha majina ndege wa nyumbani. • Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kwa kutumia jitabu mbele ya darasa. • Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali kutokana na hadithi. 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Ni nini unachokiona katika picha? 2) Unafikiri ni nini kitakachotokea katika hadithi? 3) Unakumbuka nini kutokana na hadithi uliyosoma? 4) Ni kwa nini unampenda ndege wako?
